

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 28 Aprili, 2020

*(Bunge lilianza Saa Nane Mchana)*

#### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, naomba tukae. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

#### MASWALI NA MAJIBU

*(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)*

Na. 163

**Gari la Wagonjwa Kituo cha Afya Ifumbula**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza:-

Kituo cha Afya Ifumbula kilichopo eneo la Mishemo hakina gari la kuhudumia wagonjwa:-

Je, ni lini kituo hicho kitapatiwa gari la wagonjwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibuu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Sulemaini Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijiini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Mishemo kilichopo katika Kijiji cha Ifumbula kina gari ya kubebea wagonjwa (*ambulance*) Land Cruiser DFPA 2170 ambayo ni nzima na inafanya kazi. Gari hii ilikabidhiwa katika Kituo hiki mwaka 2015.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Kwanza naishukuru Serikali kupitia TAMISEMI kwa kutupatia gari la wagonjwa Kituo cha Mishamo. Pamoja na jitihada zilizofanywa na Serikali juu ya kutupatia gari hilo bado katika Wilaya yangu ya Tanganyika, bado kunahitaji mkubwa wa gari katika Vituo vya Afya Karema na Mwese. Ukitingatia vituo hivyo viko mbali na Hospitali ya Wilaya na viko maeneo ya mpakani; Serikali ina mpango gani wa kupeleka *ambulance* katika vituo hivyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uhitaji wa magari ya kubebea wagonjwa katika Vituo vya Afya Karema na Mwese. Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari ya wagonjwa kwa ajili ya Vituo vya Afya nchini na itatoa kipaumbele kwa Vituo vya Afya Karema na Mwese.

Na.164

### **Kuongeza Bajeti ya Tarura Moshi**

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL** aliuliza:-

Utendaji wa TARURA katika Manispaa ya Moshi unakabiliwa na changamoto kubwa ya upungufu wa fedha kiasi kwamba hali ya barabara katika Manispaa ya Moshi imekuwa mbaya kuliko hata zilipokuwa zikisimamiwa na Halmashauri:-

(a) Je, Serikali haioni haja ya kuongeza bajeti ya *TARURA* ili iweze kukabiliana na changamoto ya uharibifu wa barabara katika Manispaa ya Moshi?

(b) Je, ni lini Serikali itafanya tathmini ya mafanikio na changamoto za *TARURA* ili kuona namna ya kuifanyia maboresho?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, Mbunge wa Moshi Mjini, lenye sehemu (a) na ((b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2015 hadi 2020, Serikali imeongeza fedha za Mfuko wa Barabara kutoka shilingi bilioni 218.55 hadi shilingi bilioni 251.73 ambapo kuna ongezeko la shilingi bilioni 33.18.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021 fedha za mfuko wa barabara zimeongezeka na kufikia shilingi bilioni 275.03 ambapo kipaumbele cha matumizi ya fedha hizo kitakuwa ni uboreshaji wa miundombinu iliyoharibiwa na mvua zinazoendelea kunyesha nchini.

Na.165

**Kuboresha Miundombinu ya Hospitali ya Wilaya ya Kahama**

**MHE. AZZA H. HAMAD** aliuliza:-

Hospitali ya Wilaya Kahama ina msongamano mkubwa wa wagonjwa:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kutosha ili kuongeza miundombinu katika Hospitali hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA  
NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Azza Hillay Hamad, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kuipanua Hospitali ya Wilaya ya Kahama kwa kujenga jengo la kisasa la wagonjwa wa nje ambalo litakamilika Julai, 2020. Usanifu wa jengo la ghorofa mbili la huduma ya afya ya mama na mtoto (*Maternity and Pediatric Block*) tayari umekamilika. Ujenzi utaanza katika mwaka wa fedha 2020/2021. Jengo hilo likikamilika litakuwa na vitanda 320 ambavyo vitasaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa kwa kiasi kikubwa.

Na.166

**Ukosefu wa Magari Wilaya ya Bunda**

**MHE. ESTER A. BULAYA** aliuliza:-

Kituo cha Bunda kina gari moja ambalo ni bovu na linahudumia Wilaya nzima ya Bunda yenyewe Majimbo matatu; Bunda, Bunda Mjini na Mwibara.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukipatia Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Bunda magari imara kwa ajili ya kuimarisha ulinzi Wilayani humo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia jeshi la Polisi inafahamu uhaba na uchakavu wa Magari ya kutendea kazi za Polisi Nchi nzima. Hata hivyo Jeshi la Polisi limekuwa likigawa magari kwenye himaya za Mikoa na Wilaya kwa

awamu na kadri hali ya bajeti inavyoruhusu ikiwemo Wilaya ya Bunda.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa *OCD* wa Bunda ana gari linalohudumia Wilaya nzima kama iliyyo katika Wilaya nyingi nchini. Ni kweli Wilaya ya Bunda ina Majimbo matatu ya uchaguzi, ambapo gari hilo limekuwa likitoa huduma katika Majimbo hayo na kwa sasa magari hugawiwa mpaka kwa *OCD* na siyo kwenye Majimbo ya Uchaguzi. Hali ya bajeti itakavyoruhusu ombi la Mheshimiwa Mbunge litazingatiwa la kupeleka mgao wa magari ya Polisi Majimboni nchi nzima lakini pia kwenye Halmashauri.

Na. 167

**Vigezo vya Kuajiriwa Jeshi la Polisi**

**MHE. HAMAD SALIM MAALIM** aliuliza:-

Jeshi la Polisi ni Taasisi ya Muungano na kwa kuwa ajira za Jeshi la Polisi husimamiwa na Taasisi ya Muungano.

Je, ni vigezo gani vinavyotumika katika kuwapata vijana wanaofaa kuajiriwa na Taasisi hii ya Muungano?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Hamad Salim Maalim, Mbunge wa Kojani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuajiriwa katika Jeshi la Polisi Tanzania unaelezwa vizuri katika kifungu Na. 12 cha Sheria ya Jeshi la Polisi na huduma saidizi na kanuni za kudumu za Jeshi la Polisi (*Police General Orders*) Na. 54(1) (a) hadi (g) imeelekeza wazi vigezo vinavyotakiwa kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, sifa/vigezo vinavyotakiwa kuzingatiwa kujunga na Jeshi la Polisi ni kama ifuatavyo:-

- (i) Awe Mtanzania wa kuzaliwa;
- (ii) Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi 25 kwa wenyewe elimu ya kidato cha nne, sita, astashahada na stashahada;
- (iii) Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi 28 kwa wenyewe elimu ya shahada;
- (iv) Awe na cheti halisi cha kuzaliwa, cha kuhitimu elimu ya sekondari na cha taaluma;
- (iv) Awe na tabia njema;
- (v) Asiwe na kumbukumbu za uhalifu;
- (vi) Awe na afya njema (kimwilli na kiakili) illyothibitishwa na daktari wa Serikali;
- (vii) Awe hajaoa/hajaolewa au kuwa na mtoto;
- (viii) Asiwe na alama za kuchora mwilini (tatuu);
- (ix) Awe tayari kufanya kazi za Polisi mahali popote katika Jamhuri ya Muungano ya Tanzania;
- (x) Awe na urefu usipungua futi tano inchi tano (5.5);
- (xii) Awe amefaulu usahili;
- (xi) Awe hajawahi kutumia madawa ya kulevyta;
- (xii) Awe tayari kuhudhuria mafunzo ya Polisi;
- (xiii) Awe hajaajiriwa na Taasisi nyingine; na
- (xiv) Awe katika Kambi za JKT/JKU na amemaliza mafunzo ya awali ya JKT/JKU.

Na.168

### **Kutumia Mto Mgeta Kusambaza Maji – Morogoro**

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA** aliuliza:-

Mito mingi na chemchemi zinazopeleka maji katika Bwala la Mindu hukauka wakati wa kiangazi kutokana na mabadiliko ya tabianchi na kusababisha kiwango cha maji kushuka sana na kusababisha adha kubwa ya maji kwa wananchi wa Manispaa ya Morogoro.

Je, Serikali haioni kuna haja ya kutumia Mto Mgeta uliopo Tarafa ya Mgeta – Mvomero kusambaza maji katika Manispaa ya Morogoro?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upungufu wa maji kwa mito inayotiririsha maji yake kuingiza Bwawa la Mindu pamoja na mabadiliko ya tabianchi, unasababishwa na shughuli za kibinadamu kwenye mlima Uluguru ambazo zinahitaji jitihada za pamoja ili kulinda uendelevu wa Bwawa hilo muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara kuititia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro imeanza mchakato wa kumtafuta Mtaalam Mshauri atakayefanya utafiti wa vyanzo mbadala vya maji katika Manispaa ya Morogoro (*Water Master plan*). Kazi hii inatarajiwaa kuanza mapema mwaka wa fedha 2020/2021 kwa kutumia fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ya Ufaransa (*AFD*). Mkataba wa fedha unatarajia kutiwa saini mwishoni mwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, utafiti utakapokamilika utaonesha uwezekano wa kutumia Mto Mgeta na vyanzo vingine kwa ajili ya Manispaa ya Morogoro na maeneo ya njiani ili kuhakikisha mizania ya maji inakuwa endelevu.

Na.169

**Utekelezaji wa Miradi ya Maji Buhigwe**

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA** aliuliza:-

Miradi ya maji ya Munanila, Mwayaya na Mkatanga, Buhigwe – Kibande Kasumo, Mugera/Migongo hajatekelzwa:-

Je, ni lini utekelezaji wa miradi hiyo itaanza na Mfadhilli wake ni nani?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Jimbo la Buhigwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Ubelgiji kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilionesha nia ya kufadhili ukarabati wa mradi wa maji wa pamoja wa Kata za Munanila, Mwayaya na Mkatanga kuititia Taasisi yake ya Maendeleo ya Enabel.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Novemba, 2017 kabla ya kuanza ujenzi ulifanyika upembuzi yakinifu na kubaini kuwa chanzo cha awali mradi huu kilikuwa kimekauka na miundombinu ya mradi ilikuwa imechakaa. Mapitio ya gharama ya mradi yalionesha kuwa fedha iliyokuwa imetengwa isingeweza kugharamia ujenzi wa mradi kwa Kata zote tatu.

Mheshimiwa Spika, baada ya upembuzi kubaini changamoto hizo, kilitafutwa chanzo mbadala na

kilipatikana katika Kijiji cha Mwayaya, ambapo chanzo hicho kinatosha kukidhi mahitaji ya kijiji hicho tu. Usanifu wa kina unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2020 na baada ya kukamilika taratibu za kumpata Mkandarasi zitaendelea.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa adha ya maji katika Kata za Mkatanga na Munanila, Serikali inashirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika ambapo ghamama za awali za mradi wa maji zimeshawasilishwa kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Na. 170

### **Madeni ya Wakandarasi wa Miradi ya Maji**

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Kwa muda mrefu kumekuwepo na malimbikizo makubwa ya madeni wanayodai Wakandarasi mbalimbali wa miradi ya maji:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inalipa madeni hayo?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Emanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha miradi ya maji nchini inakamilika kwa wakati, Serikali imeendelea kuwalipa Wakandarasi wanaotekeleza miradi ya maji nchini kadri hati za madai zinavyowasilishwa.

Katika mwaka 2018/2019, Serikali ililipa hati za madai zilizowasilishwa zenye thamani ya shilingi bilioni 88.5 na kwa mwaka 2019/2020 hati za madai zenye jumla shilingi bilioni 40 zimelelipwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Maji ambapo kwa kiwango kikubwa umekuwa chanzo cha uhakika katika utekelezaji wa miradi ya maji nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kulipa madeni ya Wakandarasi kwa kadri hati za madai zitakavyowasilishwa na kulingana na upatikanaji wa fedha ili miradi ya maji ikamilike kwa wakati.

Na. 171

### **Fursa Sawa ya Huduma za Afya**

**MHE. ANNE K. MALECELÀ** aliuliza:-

Kwa kuwa takwimu na *data* zinazoonyesha kuwa huduma za afya hazifanani na haziko sawa Mkoa kwa Mkoa, Wilaya kwa Wilaya na hata Vijiji kwa Vijiji:-

Je, Serikali inafanya jitihada gani ili kuondoa hali hiyo ili watu wote wa Mikoa yote, Wilaya zote, Mijini na Vijijini wapate fursa sawa ya huduma ya afya?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Kuteuliwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya katika maeneo yote nchini ili kuhakikisha huduma hizo zinapatikana kwa uwiano kwa wananchi wote. Aidha, Sera ya Afya ya mwaka 2007 inaelekeza kuwa huduma za afya zitatolewa kwa kuzingatia uwiano wa kijigrafia, mzigo wa magonjwa na idadi ya watu.

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika kutimiza azma hiyo, Serikali imeboresha au kujenga Vituo vya Afya 352, Hospitali za Rufaa za Wilaya 67 na Hospitali za Rufaa za Mikoa mitano katika mikoa mipyä mitano ya Songwe, Katavi, Simiyu, Njombe na Geita ili kuhakikisha huduma bora na za kibingwa zinawafikia wananchi kwa ujumla.

Na. 172

**Umuhimu wa Kutunza Wazee wetu Nchini**

**MHE. OSCAR R. MUKASA** aliuliza:-

Wazee ni moja ya makundi maalum ambayo kama Taifa hatuna budi kuyatazama kwa umuhimu wa kipekee na kwa kiwango stahili. Hii ni kwa sababu mbalimbali za kiafya na kijamii kwa ujumla

(a) Je, ni upi upungufu na changamoto kwa sasa kwenye Sheria ya Wazee kama ipo?

(b) Endapo Sheria ya Wazee haipo: Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya ombi hilo na kutokuwa na msingi huo muhimu wa kuhakikisha kuna nla ya dhati kushughulikia masuala yanayowahusu wazee wetu?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Oscar Rwegasira, Mbunge wa Bihamarulo Magharibi, lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa sasa hakuna Sheria ya Wazee hapa nchini. Hata hivyo, Serikali inatambua umuhimu wa kutungwa kwa Sheria ya Wazee nchini. Masuala ya wazee yanashughulikiwa kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 na Sera ya Afya ya mwaka 2007.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kuwezesha upatikanaji wa Sheria ya Wazee, Serikali kwa sasa inafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003. Aidha, kukamilika kwa mapitio ya Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 itawezesha kutungwa kwa Sheria ya Wazee itakayoshughulikia changamoto za wazee.

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 - Wizara ya Maji**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea ya hoja ambayo Mheshimiwa Waziri wa Maji, Profesa Mbarawa aliiwasilisha mbele yetu jana ya kutuomba tukubali kumpitishia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Sasa hatua ambayo tulikuwa tumefikia ni ya uchangiaji na tunaanza kama nilivyoahidi jana na wachangiaji, wale Katibu upande wa CCM wamekubaliana kwamba watachangia kwa dakika saba saba. Kwa hiyo, ikilia tu kengele moja ya dakika saba ndiyo basi tena, kwa hiyo utakuwa una-set saba inalia kengele mara moja tu, ahsante sana.

Tunaanza na Mheshimiwa Dkt. Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Masasi, karibu.

**MHE. DKT. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuzungumza kwa hoja iliyopo mbele yetu. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kwenda sambamba na llani ya Chama cha Mapinduzi katika kutatua kero za maji kwa wananchi wetu. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe pia pamoja na timu yako yote kwa kazi kubwa uliyoifanya ya kulisimaia Bunge katika kipindi hiki cha miaka mitano. Kwa namna ya kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri pamoja na timu yake ya Wizara ya Maji. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2006, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliandaa mpango wa maendeleo

ya sekta ya maji kwa miaka 20. Katika mpango ule waliweka bayana kwamba hadi kufika Mwaka 2020 takribani wananchi wanaoishi Vijijini milioni 37.1 ambao watakuwa ni asilimia 89 wanaopata maji ya uhakika watakuwa wamepata maji hayo. Ukiangalia hotuba ya Waziri anasema wako kwenye asilimia 85, hii maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba tunakwenda vizuri na ndiyo maana wamepishana kidogo tu na makisio ambayo walikuwa wameyakisia kwa mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa jumla walivyoamua kutenga fedha katika baadhi za Mamlaka za Maji ikiwemo Mamlaka ya Maji ya MANAWASA, lakini naomba niseme tu kwamba, sasa takribani kipindi cha miaka minne mfululizo fedha hizi zimekuwa zikitengwa na hazikuwa zinatolewa. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri tena kwa unyenyekevu, ajitahidi kadri atakavyoweza fedha alizotenga kwa ajili ya MANAWASA, shillingi billioni mbili, fedha hizo ziende kwa ajili ya kutatua changamoto ya kukamilisha ujenzi wa chujio pamoja na miundombinu ya mamlaka hii inayosambaza maji kwa Mji wa Masasi na Mji wa Nachingwea.

Mheshimiwa Spika, pia tunazo changamoto kadhaa ambazo zinazikabili Mamlaka zetu za Maji, nitazisema kwa jumla hapa. Changamoto ya kwanza inayoikabili sekta ya maji hasa upande wa mamlaka ni gharama kubwa za umeme. Gharama hizi za umeme zinapelekea gharama kubwa za maji kwa watumiaji wa kawaida wa chini kabisa. Nadhani huu sasa ni wakati wa Serikali kuona ni namna gani gharama za matumizi ya maji zinapungua kwa wananchi, lakini najua miongoni mwa mbinu ambayo inaweza kuwa inatusaidia sana ni mpango mkakati wa Serikali wa ujenzi wa Bwawa la umeme ambapo litakwenda kuzalisha umeme wa kutosha kwa ajili ya huduma kama hizi kupatikana kwa gharama ya chini.

Mheshimiwa Spika, ipo changamoto nyingine; Mamlaka zetu za Maji zinakabiliwa na madeni wanayodai kwa Taasisi mbalimbali hususani Taasisi za Serikali. Kwa hiyo naomba Serikali ione namna ambavyo inaweza ikaona

kwamba yenyewe inachangia kuzitorotesha hizi mamlaka kwa kutolipa madeni ya bili za maji kwa wakati. Natoa tu mfano mdogo; Mamlaka yetu ya MANAWASA inadai zaidi ya shilingi milioni 200 hadi kufikia Machi mwaka huu. Kwa hiyo naomba Serikali iliangularie hili jambo kwa ujumla wake kwamba ni muhimu Taasisi za Serikali zilipe bili ya maji kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa maamuzi yake ya kuunda *RUWASA* na nitumie fursa hii pia kumpongeza sana Injinia wetu wa Mkoa, Injinia Mbaraka Ally pamoja na Injinia wangu wa Wilaya, Juma Yahaya ambao wanafanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba hizi changamoto za maji zinatatuliwa. Hata hivyo, ipo changamoto inayoikabili sasa *RUWASA* na nadhani inaweza kuwa ni changamoto ambayo iko Wizarani, nayo ni utaratibu wa muda mrefu wa kufanya manunuvi ya vifaa vya ujenzi kwa miradi hii.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Masasi kuna miradi ambayo imetangazwa muda mrefu, kwa mfano; Mradi wa Maji wa kutoka Jimbo la Mheshimiwa Bwanausi pale Mpindimbi kuelekea Chipole hadi Namikunda A na Namikunda B. Mradi huu unashindwa kutekelezwa kwa sababu kila siku tunavyoulima tunaambiwa kwamba mabomba yananunuliwa kutoka Wizarani. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aangalie sasa namna ambavyo jambo hili tunaweza tukalitatua. Ni changamoto kubwa kwa kweli kwa sasa na wananchi wanahitaji miradi hii iweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2016 na 2017, Halmashauri ya Mji wa Masasi ilipata fedha kwa ajili ya kuwa na Mradi Mkubwa wa Maji, lakini kwa bahati mbaya sana baadhi ya fedha hazijatoka. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atueleze basi fedha hizi ambazo zilikuwa hazijakamilisha mradi huu zitatoka lini ili mradi uweze kuwa katika sura ambayo ilitarajwa.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa jumla kwa kupata fedha kwenye mradi

wa mwaka 2018/2019 mradi wa visima 11. Tayari visima nane vimeshachimbwa na maji mengi yamepatikana, lakini tunaomba sasa Serikali au tunaomba Wizara itoe kibali sasa kwa Injinia wetu wa Wilaya kufanya usanifu pamoja na ujenzi wa miundombinu ili visima vile nane vilivyokamilika wananchi wa vijiji vile waanze kupata maji wakati Mkandarasi anaendelea na uchimbaji wa visima vitatu vilivyobaki na utaratibu wake wa kudai fedha za Serikali uendelee huko, lakini huku tuendelee kuendeleza miradi hii.

Mheshimiwa Spika, naona kengele imelia naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Dkt. Rashid Chuachua. Mheshimiwa Richard Philip Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Injinia Edwin Ngonyani ambaye nadhani atakuwa Msekwa. Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi. Kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Profesa Mbarawa kwa kazi kubwa ambayo ameifanya ya kuzunguka nchi nzima akisaidiwa na Naibu wake, Mheshimiwa Jumaa Aweso, Mzee wa "maji safi na salama na yanayotosheleza". Pia niwapongeze Watendaji wote katika Wizara, Katibu Mkuu pamoja na Mtendaji Mkuu wa *RUWASA* na timu yake, Mhandisi Bwire na wengine kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kwa Taasisi mpya hii ambayo Serikali imeianzisha.

Mheshimiwa Spika, pia naomba niipongeze Serikali, ukiangalia miradi ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Bajeti ni bilioni 610 lakini kwenye Bajeti hii inayokuja ni bilioni 705. Kwa hiyo kuna ongezeko la takribani shilingi bilioni 95, ni hatua nzuri Serikali imefanya kuongeza bajeti.

Mheshimiwa Spika, hii ni Bajeti ya Wizara ya Maji, lakini naomba nigusie suala moja ambalo linahusiana na sukari maana sukari inakwenda kutengeneza chai ambayo inatokana na maji. Hivi karibuni Serikali ilitoa muongozo wa bei elekezi lakini kuna changamoto kidogo katika hizi bei.

Ukiangalia bei ya rejareja kwa Dar es salaam ni Sh.2,600 kwa kilo lakini kwa Mkoa wa Katavi tunaotoka sisi na Mkoa wa Rukwa, bei ya juu kabisa elekezi ambayo Serikali ilitoa ni Sh.3,200. Sasa tofauti ni shilingi 600, je, hii 600 ndiyo ambayo inatokana na usafiri? Wakati mfuko mmoja wa kilo 50 ukiusafirisa kutoka Dar es salaam mpaka unafika Mpanda-Katavi ni Sh.6,000, kwa hiyo maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba, kilo moja inasafirishwa kwa Sh.120. Hata ukichukua bei ya rejareja hiyo ya Dar es salaam 2,600 ukiongeza 120 bado haizidi 2,800.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali, kipindi hiki ni kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kwa hiyo bei kwa maeneo mengi ya nchi bado iko juu kutokana na bei elekezi iliyotolewa kuwa ya juu kuliko hata ile ya awali iliyokuwepo. Kwa mfano, kama bei elekezi Katavi ilikuwa 2,800 lakini sasa hivi kutokana na bei elekezi ni sawa sawa na chura ukimpiga teke umemwongezea hatua, kwa hiyo kwa mwongozo ule umefanya na wafanyabiashara waongeze bei. Kwa hiyo, niiombe Serikali, Waziri wa Kilimo na Waziri wa Viwanda na Biashara wapitie tena bei hizi na watoe bei ambayo inaendana na uhalsia ili wananchi wetu wapate unafuu katika hii sukari ambayo kipindi hiki inahitajika sana maana tunatumia sana tangawizi na limao tunaweka na sukari kutokana na janga hili la *corona*, lakini pia ni Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Kwa hiyo naiomba Serikali iliangularie na wachukue hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika baada ya dokezo hilo, naomba niende kwenye suala la miradi ya maji. Kwanza katika hotuba ya Waziri ameelleza kwamba kuna miradi ambayo inafanyiwa kazi katika Halmashauri zote Tanzania nzima. Niombe; miradi hii mingi ambayo kuna malipo yamefanyika kwa asilimia Fulani, tuna uhakika kwamba huenda itavuka mwaka huu wa fedha kwa sababu tayari tunakwenda mwezi wa tano. Kwa hiyo, niombe sasa Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Maji wajumuushe miradi yote ambayo ndiyo inamalizika na kwamba itavuka Mwaka wa Fedha na la msingi la kufanyika hapa ni tufanye *Budget reallocation*, kwa sababu Serikali imefanya vizuri katika utekelezaji, imetoa asilimia 74

ya fedha zote mpaka kufikia Machi, kwa hiyo hii robo moja iliyobaki ya mwaka basi fedha yake kwa ile miradi ambayo itakuwa hajakamilika, basi ifanyike *Budget reallocation* ili tuisiathiri Bajeti ambayo inakuja ya mwaka 2020/2021. Kwa kuwa mfumo wa Serikali ni *cash budget*, tuombe sana Waziri wa Fedha alichukue hilo na tunaomba na Waziri wa Maji katika majumuisho aweze kutupa hiyo *assurance*.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusiana na Mradi wa Ziwa Tanganyika kutoa maji Ziwa Tanganyika kuleta katika Mji wa Mpanda. Mheshimiwa Waziri tumekwishamweleza na Watendaji wa RUWASA tuliwaeleza kwamba Jimbo la Nsimbo liko ndani ya Wilaya ya Mpanda, kwa hiyo kuna umuhimu mkubwa sana Jimbo la Nsimbo kujumuishwa katika Mradi huo wa Kutoa Maji Ziwa Tanganyika.

Kwa hiyo, *reserve tank* ambayo inakwenda kujengwa iende ikachukue *population* ya Nsimbo na Mpanda Mjini kwa ujumla wake. Kwa mfano, kuna Kata ambazo huwezi ukaziacha katika mradi huu; Kata ya Machimboni, Ibindi, Stalike, Itenka, Nsimbo, Kapalala, Mtapenga. Kwa sasa hivi Mji wa Mpanda unalishwa maji kutoka katika Jimbo la Nsimbo, katika Bonde la Ikorongo. Liko la Nsimbo lakini hatunywi yale maji. Kwa hiyo, sasa tukishafanikisha hili tutahudumia hizi kata nyingi na maji ya Ikorongo sasa yatakwenda kuhudumia kata zingine.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusiana na miradi hii ambayo tumeipata kutokana na Serikali kutoa Dola 600,000 (*P4R*), kwa hiyo tuombe Serikali iendelee na kusimamia ipasavyo miradi hii na inafanyika kwa *Force account*...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbogo

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Tunakubali *Force account* tunapunguza...

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nashukuru.  
(*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Richard Philip Mbogo na namuunganisha sasa kutoka Msekwa, Mheshimiwa Injinia Edwin Armandus Ngonyani na atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma. Mheshimiwa Ngonyani kutoka Msekwa.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii ya kuongea mbele ya Bunge lako Tukufu. Pili, nikupongeze wewe kwa kweli kazi unayofanya ni kubwa sana ya kutulinda sisi Wabunge dhidi ya *corona*, lakini vilevile kutuhudumia sisi Wabunge katika kipindi chote ambacho tumekuwa hapa Dodoma. Nikupongeze sana na mimi binafsi nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa namna anavyoangalia watu wa kipato cha chini, wanyonge na Jimbo langu la Namtumbo ndiyo tulio wengi. Wengi sisi ni wanyonge na kwa kweli katika kipindi hiki cha Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika kila sekta ametusaidia sana na naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Profesa Makame Mnyaa Mbarawa. Kwa kweli Mzee Mnyaa ametuletea huyu Profesa Makame ambae mimi namfahamu. Ukiacha katika sekta aliyonayo ni mtu makini, ni mtu ambaye yuko tayari kuwatumikia watu na siyo kujitumikia yeye. Hongera sana na sasa naona katika sekta hii ya maji kazi kubwa anayoifanya pamoja na kwamba, naweza nikaungana na Mheshimiwa Spika hatujapata miradi mingi katika Wilaya yetu ya Namtumbo, lakini kwa ujumla kazi inayofanyika ni kubwa. Nina uhakika sasa ataangalia yale Majimbo ambayo alikuwa ameyasahau kidogo ikiwa ni pamoja na Kongwa na Jimbo la Namtumbo.

Mheshimiwa Spika, kwa Jimbo la Namtumbo kuanzia mwaka 2006 tulikuwa na Miradi ya Maji inayoitwa ya *World Bank* ya Vijiji 10. Nimwombe Profesa Makame Mnyaa

Mbarawa kama jina la Baba yake lilivyo atusaidie Wananamtumbo katika miradi ile 10 ya *World Bank*. Nimshukuru sana kwa miradi ile minne ambayo ameitengea fedha na nina uhakika ataikamilisha hiyo miradi katika mwaka huu ama ujao wa 2020/2021 kwa maana ya Mradi wa Ruhimbarilo na Ikesi ambao hadi sasa una asilimia 60 ya utekelezaji; Mradi wa Likuyuseka ambao umefikia asilimia 75, Mradi wa Kumbara-Litora nao umefikia asilimia 75; pamoja na Mradi wa Mkongo-Gulioni-Nahimba ambao umefikia asilimia 77. Nimwombe sana fedha hizo zilizotengwa sasa zikamilishwe.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa kuanzia mwaka 2006 mpaka leo mwaka 2020 kwa kweli siyo vizuri sana kuendelea kuuongelea na kwa kasi anayokwenda nayo, nina uhakika miradi hiyo ataikamilisha haraka. Nimwombe sana atuongezee mradi wa tano, mradi ambao nao ni wa siku nydingi, wa miaka mingi na umepitia mapito mengi sana, Mradi wa Maji wa Hanga-Mawa-Msindo ambao mwanzo ulipoanza ulikuwa unahudumia vijiji vitatu lakini sasa tunaongelea vijiji vitano. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri mradi huo autengee fedha ili uweze kutekelezwa, nao katika kipindi chake ahakikishe kwamba umekamilika.

Mheshimiwa Spika, ukija kwenye bajeti ya Wizara hii kwa ujumla, nadhani ni kilio cha watu wengi kwamba Wizara hii inatengewa fedha, lakini fedha zenyewe hazitoki ama hazitoki kwa ukamilifu. Niombe sana Serikali kwa ujumla hususan Wizara ya Fedha, Wizara hii ni muhimu sana, maji ndiyo uhai wetu. Niombe sana huyu Waziri tumsaidie apate hizi fedha ili miradi aliyopangia katika mwaka huu wa 2020/2021 aweze kuitekeleza. Fedha zote zitoke ili miradi iliyokusudiwa katika Halmashauri mbalimbali ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo aweze kuitekeleza kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, nikuombe sana, huyu Waziri tumsaidie apate hizi fedha ili miradi aliyopangia katika mwaka huu wa 2020/2021 aweze kuitekeleza. Fedha zote zitoke ili miradi iliyokusudiwa katika Halmashauri mbalimbali

ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo aweze kuitekeleza kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunaongelea *TARURA* au *RUWASA*; *RUWASA* ni chombo kizuri tumeikiunda hivi karibuni lakini hakina wataalamu na rasilimali watu na kwa kweli rasilimali fedha zilizoko nazo hazitoshi.

Mheshimiwa Spika, niombe chombo hiki kiweze kupata rasilimali fedha na rasilimali watu ili hatimaye kazi inayokusudiwa kutekelezwa chini ya *RUWASA* iweze kukamilishwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa ni Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, mkumbuke ni dakika saba saba.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda sana kumpa pongezi Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya. Pongezi sana kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji, Naibu wake pamoja na Wizara nzima kwa ujumla kwa kazi nzuri wanaoifanya.

Mheshimiwa Spika, nakupa pongezi wewe kwa kuendelea kutulinda humu Bungeni pia na Naibu Spika kwa kazi nzuri mnayoifanya. Nawapa pongezi na nasema Mwenyezi Mungu azidi kuwalinda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pole sana kwa familia ya ndugu zetu Mchungaji Dkt. Rwakatare nikiwa Mbunge wa Morogoro pamoja na Naibu Meya ambaye na ye ye ametutoka jana na marehemu wote waliotangulia. Namwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwani imetekeleza miradi mingi kwenye Mkoa wetu wa Morogoro. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, Prof. Mbarawa pamoja na Mheshimiwa Aweso wamefanya ziara kwenye mkoa wetu na kuna miradi mikubwa na midogo ambayo inatekelezwa kwenye wilaya zote za Morogoro. Kwa hiyo, nawapa pongezi sana na nasema ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, pia natoa shukrani kwa mradi wetu wa magadi ambao mara kwa mara nilikuwa nausemea sana kwenye Bunge hili pamoja na mradi wa Kihondo ambayo yote inapatikana kwenye Manispaa ya Morogoro. Manispaa ya Morogoro huwa tuna tatizo la maji kwani mpaka sasa hivi hayatoshelezi, tunapata kwa mgao. Naamini kuwa miradi hii ikikamilika maji yataweza kuongezeka kwenye Manispaa yetu ya Morogoro.

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza Serikali kwa mradi wa Gairo kwani Wilaya ya Gairo tulikuwa tuna maji ya chumvi lakini sasa kwa kutumia mashine ya kisasa imeweza kuchuja chumvi kwa sasa hivi kata za mjini tunapata maji safi na salama kwenye Wilaya yetu ya Gairo. Hata hivyo, bado kuna kata ambazo hazijapata maji lakini niliposoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri nimeona wametengewa fedha na wenyewe wataweza kupata maji kadri fedha zitakavyotoka kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kushukuru kwa mradi wa kulinda vyanzo vyta maji kwa Milima ya Uluguru kwani ilikuwa imepoteza uhai na uoto wake. Sasa hivi tumetengewa dola za Kimarekani 27.65 ambazo zitawezza kukamilisha na kuendesha mradi katika Milima ya Uluguru ambapo kuna miziga, *VICOBA* na ujasiriamali kwa akina mama. Kwa kweli naishukuru Serikali kwa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee Bwawa la Mindu. Bwawa hili ni la muda mrefu, Morogoro Manispaa hatuna maji ya kutosha na sisi tunategemea kupata maji ya kutosha kutoka kwenye bwawa hili. Mpaka sasa hivi maji hayatoshi na narudia kusema kuwa tunapata maji kwa mgao. Kwa hiyo,

naomba kufahamu hayo mazungumzo mnayoendelea kuzungumza na wahisani wetu yatakamilika lini Mheshimiwa Waziri? Tumesubiri kwa muda mrefu na kwenye Manispaa ya Morogoro bado hatupati maji ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Kidunda ni kweli fidia ambayo ni shilingi bilioni 11.4 zimelipwa kwa wananchi lakini mpaka sasa hivi bado halijaanza kutengenezwa. Jambo zuri ambalo nimeona kwenye bajeti hii ya 2020/2021 ni kuwa wametengewa shilingi bilioni 3. Hizi fedha zikitoka, naomba sana zisimamiwe vizuri kusudi Bwawa la Kidunda liweze kufanya kazi yake kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji Chalinze III. Mradi huu utahudumia Mkoa wa Pwani ikiwemo Chalinze pamoja na Kibaha lakini kwa Mkoa wa Morogoro unahudumia Vijiji vya Kidugalo, Ngerengere, Gwata, Maseyu na Lubungo. Kwa muda mrefu ulikuwa umesimama lakini kwa sasa hivi nimeona kuwa umetengewa fedha mwaka huu 2020/2021 shilingi bilioni 4.5. Mradi huu umesimama kwa muda mrefu, kwa hiyo, hizi fedha zikitoka uwepo usimamizi wa karibu kusudi wananchi waweze kupata maji na mradi uweze kukamilika kwenye Mkoa wa Morogoro kwa vijiji nilivyovitaja ikiwa ni pamoja na Pwani, Chalinze na Kibaha.

Mheshimiwa Spika, miradi ya miji 28. Naisemea miradi hii kwa sababu kuna Mji Mdogo wa Ifakara ambao upo Kilombero, kwenye Mkoa wetu wa Morogoro. Kwa kweli naomba uangaliwe kwa makini, Wabunge wengi wamezungumzia hili. Nimesoma kwenye hotuba nimeona kuna mazuri, kama kweli yapo naomba yakinoteka yatekelezwe kama yalivyoordheshwa kwenye mradi huu.

Mheshimiwa Spika, nisimalize bila kuongelea kuhusu *Corona*. Kwa kweli unatujali na unatulinda, naomba Wabunge tufuate kama Spika wetu anavyosema na hasa kama viongozi wetu wanavyotushauri. Tuchukue ushauri wa wataalam wa afya, tuzidi kuomba Mwenyezi Mungu azidi kutulinda na kwa sababu tuko hapa Mwenyezi Mungu anatulinda. Watu wote wanaokufa sasa hivi hata Naibu Meya

wangu, samahani sikukusudia hilo lakini wanaokwenda sasa hivi inaonekana ni hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utafiti unaendelea kuhusu kutibu Corona, tufuate ushauri wa tiba mbadala. Sisi kwetu Kagera ni kweli tunafukizia siyo mara ya kwanza na siyo ajabu. Mafua yakiwa makubwa lakini siyo *Corona* huwa tunachukua miti shamba unajifunika unajifukizia. Hata jana mimi mwenyewe nimejifukizia; nimechukua mwarobaini, mpera na miembe kwa sababu mkaratusi sikuuona. Kwa hiyo, naomba tufuate maelekezo na Mwenyezi Mungu atatulinda.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Tayari kengele.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ila ulikuwa unaongea jambo la maana ndiyo maana nikamezea kidogo.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Mwenyezi Mungu akubariki kwa kunipatia nafasi hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma. Kwa wale ambao hawajui utaratibu wa kujifukizia basi mumuone ili awape *consultation* ya bure.

Tunarudi Msekwa kwa Mheshimiwa Edward Mwalongo na atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu ambaye yuko hapa ukumbini. Mheshimiwa Mwalongo.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika bajeti hii ya Wizara ya Maji ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai mpaka siku hii ya leo nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu nikitoa mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali yake kwa jinsi anavyofanya kazi na anavyotuhudumia Watanzania. Wengi tumeridhika, miaka mitano ya uongozi wake tumeona mengi mapya na tunaimani kabisa atatuwezesha Watanzania kusonga mbele katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe kwa umahiri mkubwa ulioonesha katika kuliendesha Bunge letu kwa miaka mitano. Sisi wengine tulikuwa ni Wabunge wapya lakini umetulea vizuri, tumeishi vizuri Bungeni, umetufundisha na tumefanya kazi yetu ya uwakilishi kwa wananchi wetu vizuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, katika hii hatua ya mwisho umeleta huu mfumo wa kidigitali ambao umewezesha Bunge leo pamoja na *Corona* kazi inakwenda vizuri sana. Hongera sana, tunakupongeza sana kwa hili na Mwenyezi Mungu akujalie afya njema na uwezo zaidi na zaidi katika kuitumikia nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa hotuba yake nzuri na watendaji wote wa Wizara ya Maji. Maji hayana mbadala, panapohitajika maji lazima yawepo, huwezi ukatumia chochote kile badala ya maji. Maji ni uhai maji ni afya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wanajitahidi sana kufanya kazi nzuri, tumeona wanazunguka nchi nzima hata katika Jimbo langu la Njombe wamefika mara kwa mara na tukatembelea miradi mbalimbali ya maji lakini miradi hii mingi imeharibiwa na Serikali. Tunasema wakandarasi wameharibu miradi ya maji lakini imeharibiwa na Serikali kwa sababu mkandarasi anapewa kazi kwa

utaratibu ambao Serikali imeweka; analeta vifaa anaanza kufanya kazi lakini malipo yanachelewa zaidi ya miezi sita toka ameanza kutekeleza mradi huo na inawezekana mradi wenyewe usikamilike lakini malipo hakuna. Kwa hiyo, kwa utaratibu huo unaona kabisa kwamba Wizara yenyewe na wataalamu wake ndiyo wanaharibu miradi hii, inafika mahali inashindikana kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi katika Wizara hii kulikuwa na ukiritimba mkubwa sana ambao sasa nafikiri Mheshimiwa Waziri amejitahidi sana kuuondoa lakini bado upo. Watu wanaohusika na mambo ya *designing*, kule kwangu kuna Mradi wa Maji wa Igongo, umefanyiwa *designing* zaidi ya mara nne, kwanza tumekaa na Mheshimiwa Kamwele tumejadiliana wanasema *designing*, amekuja Mheshimiwa Prof. Mbarawa tumekaa tumejadiliana ni *design, design*, mradi ulishapitishwa na ulishatekelezwa zaidi ya asilimia 50 lakini leo inakuja hoja ya *designing*. Sasa unajiliza, hawa wataalam wetu wanatupeleka wapi? Hivi ni kweli nchi imesomesha watu walete maendeleo katika nchi au imesomesha watu wadumaze maendeleo katika nchi? Wanachukulia kigezo cha *designing*, wanazuia miradi haiendelei na miradi inakwamalakini pia hawa wakandarasi wanafilisika kwa sababu wanakuwa wamefanya kazi halafu hawalipwi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, mimi ningeshauri kabisa kwamba Serikali na watendaji wote wa Serikali wafahamu kwamba fedha hizi tunazopitisha Bungeni kama fedha za bajeti ni fedha za maendeleo. Ndiyo fedha hizo zikizunguka huko kwenye miradi na kwa wananchi ndiyo zinazoleta maendelo. Mwisho wa siku fedha hizo zinaingia kwa wafanyabiashara ambao wanafanya kazi hizi na wengine wanalipa kodi halafu Serikali inapata fedha tena. Kwa hiyo, wanapokuwa na ukiritimba mkubwa maana yake wanazuia maendeleo kwa wananchi lakini wanazuia Serikali isipate fedha. Kwa hiyo, hili ni jambo la msingi sana lazima waangalie.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri sana kwamba anaenda kutumia vizuri *Force Account* katika

miradi hii ya maji lakini kama kwa *speed* iliyokuwepo hapo nyuma na *designing* za siku za nyuma ambazo zilikuwa zinasanifu miradi halafu haifanikiwi kwa kweli hata hii Force Account haiwezi kusaidia chochote. *Force Account* itafanya kazi vizuri ikiwa kama taratibu za manunuzi na za utekelezaji wa miradi zitakwenda vizuri. Siyo asilimia 25 tu ya fedha za mradi ndiyo inatolewa halafu mradi unakwama, hiyo *Force Account* na yenyewe haitazaa matunda tunayokusudia. Wananchi wanahitaji maji na sisi Wabunge wao tunaomba Serikali itoe maji lakini siyo wanahitaji mkandarasi awepo pale *site* wakati hana nguvu yoyote ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, upo mradi wa Miji 28 ukiwemo Mji wangu wa Njombe Mjini. Ni jambo la kusikitisha sana, leo ni mwaka wa tano Serikali inatuambia kwamba imekopa fedha kutoka India itatekeleza mradi huo. Huu mradi nashindwa hata kuelewa, hiyo ni *negotiation* ya alia gani miaka mitano wanajadiliana juu ya kupata fedha kwa ajili ya mradi wa maji? Ni jambo la kusikitisha sana, tumewaaahidi wananchi wale miaka mitano mfululizo kwamba kuna mradi utatekelezwa kutoka Mto wa Gafilo kwa ajili ya maji ya Njombe Mjini.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine wananchi wetu wanapata hasira kwa sababu tunaahidi lakini miradi haitekelezeki na unakuja kuona katika maeneo mengine maji yanasafrishwa kilometra 200, tunaambiwa maji yanatoka Ziwa Victoria mpaka Tabora. Kwa Mji kama wa Njombe unajuliza, maji yako chini ya kilometra moja kutoka mjini lakini mji hauna maji, ni jambo la kusikitisha sana. Kwa hiyo, niombe Wizara ya Maji iangalie kama kuna maeneo vyanzo viko jirani itekeleze hiyo miradi shida hiyo iwe imeisha. Haiwezekani watu wa Njombe ambapo kila bonde lina maji tulalamikie maji safi na wananchi wanaishi sehemu zenye ukame na wenyewe wanalamikia maji na Wizara ipo, ina maana kwamba Wizara haiweki mambo vizuri ikaona kwamba mahali ambapo inatekeleza kwa urahisi itekeleze mara moja shida iwe imekwisha. Kwa hiyo, niombe sana Mradi huu wa Miji 28 ikiwemo Mji wa Njombe utekelezwe ili kusudi wananchi wawezee kupata maji.

Mheshimiwa Spika, nipongeze Wizara kuanzisha RUWASA. RUWASA inafanya kazi nzuri katika Jimbo la Njombe Mjini na katika Mkoa wa Njombe. Wako wahandisi makini sana pale wanajitahidi lakini wahandisi hawa watavunjika moyo ikiwa fedha haitakwenda.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Edward Mwalongo, ahsante.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikwishakutaja Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, atafutiwa na Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. Nami kama wengine nikupongeze hasa mimi ninayekufahamu muda mrefu, kwa kweli, umeongoza Bunge hili kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kutoa kipaumbele kwa maji na sasa tunaona kutokana na *Corona* jinsi maji yatakavyotusaidia kama tutayatumia vizuri na pale ambapo hayapo mjue kuna shida kubwa sana. Nampongeza Waziri wetu, anajitahidi muda aliokaa ni mfupi na ametembea sana na ni kweli kwamba kuna wengine hawana maji. Si Waziri peke yake namshukuru pia Naibu Waziri na Katibu Mkuu ametoka Hanang juzi na watendaji wengine wote katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana viongozi katika wilaya yangu tunashirikiana nao vizuri, wilaya ambayo maji ni kidogo sana. Vilevile niwashukuru sana wana-Hanang kwa kuwa na ushirikiano na mapenzi makubwa na Mbunge wao mimi na Mungu awajalie sana twende vizuri na tuendelee vizuri pamoja na wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wabunge tumeshirikiana sana, najua maji ni tatizo kubwa kwa Hanang, maji ni uhai kama walivyosema wengi, maji ni maendeleo, maji ni biashara vilevile lakini maji ni siasa. Naomba sana Waziri uone kule ambako kuna matatizo makubwa unayaendea hasa kwa ugonjwa huu wa Corona.

Mheshimiwa Spika, wilaya yangu ni wilaya moja ambayo ina matatizo makubwa ya maji na mpaka sasa tuna asilimia 57 ya maji. Najua Serikali inajitahidi sana, mwaka 2005 tulikuwa na visima 8; mwaka 2010 tulikuwa na visima 36, mwaka 2015 tuna visima 44 na mwaka huu 2020 takribani visima 75. Kwa hiyo, utaona kwamba Serikali inajitahidi lakini ni wilaya ambayo haina mito wala maziwa. Nashukuru sana tuna Ziwa moja la Basotu ambapo sasa tumeanza kutoa maji kwenda vijijini ingawa wananchi wanaogopa Mungu kule atakasirika lakini naona wananchi wetu wamepewa elimu wameelewa.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme ndugu zangu ni kata 12 tu kati ya 33 ambazo zina maji. Mwaka huu unaoisha tumejitahidi sana kupata maji ya Katesh lakini mpaka sasa hatujapata. Naomba Waziri uwahimize wale wenye jukumu hili Katesh Makao Makuu ya Hanang yapate maji.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba maeneo ambayo yalijaribiwa lakini mpaka sasa hayana maji kama Gehandu, Lalaji, Dumbeka, Gidehababie na Gaulol. Tumejaribu kuyachimba, pale ni *Rift Valley*, muwe mnatuletea mashine zinazoweza kwenda mbali zile ambazo zinazoenda hapa karibu hatuwezi kupata maji.

Mheshimiwa Spika, sisi tuna visima vya *solar* lakini kwa sababu Wilaya ya Hanang ni baridi, mara nyngi sana maji hayapatikani. Naomba tufikishe umeme kwenye visima hivyo ili watu waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, Matangarimo pamoja na Kwachele hamna maji. Tumejaribu makorongo yale yanapopitisha maji tumeweka makinga maji na sasa tuna

maji mengi na hata wanalima mboga na kufanya mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, maji ya Endasak yamepatikana lakini maji ya vijiji vingine vinavyozunguka Endasak hajapatikana. Masakta walipangiwa shilingi milioni 1.3 na Endasak shilingi milioni 1.5, Katesh shilingi bilioni 2.5, naomba hela hizo zitumike vizuri ili maeneo yale ambayo yana watu wengi na hayana maji yaweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Hanang tumepongiwa shilingi bilioni 2.6, fedha hizi ni kidogo sana. Naishukuru Serikali kwamba tumepongiwa fedha hiyo lakini kwa kweli kwa matatizo na changamoto tulizonazo na nimewaambia tumejata asilimia 57, naomba muangalie kama mnawenza mkaongeza hela kwa ajili ya maeneo ambayo yana matatizo makubwa hasa ukizingatia ugonjwa huu ambao utaumiza watu.

Mheshimiwa Spika, na vilevile Masakta walipangiwa bilioni 1.3 na sasa Endasaki bilioni 1.5, Kateshi bilioni 2.5 ninaomba hela hizo zitumike vizuri ili maeneo yale ambayo yana watu wengi na ambayo hayana maji yaweze kupata maji. Tumepongiwa shilingi bilioni 2.6 kwa Wilaya ya Hanang ni kidogo sana naishukuru Serikali kwamba tumepongiwa hiyo lakini kwa kweli kwa matatizo na changamoto na nimewaambia tumejata asilimia 57, muangalie kama mnawenza mkaongeza hela kwa ajili ya maeneo ambayo yana matatizo makubwa hasa ukizingatia ugonjwa huu ambao utaumiza watu.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru Spika, tuendeleee kwa ushirikiano mkubwa wewe ni mtu ambaye tunapaswa kukuiga ulinikuta nikiwa Mbunge wa Viti maalum na wewe ukaanza kuwa Mbunge wa Jimbo baadaye nyuma yako nikawa Mbunge wa Jimbo kwa hiyo naomba tusaidiane ili tuendeleee na Ubunge wetu tufikishe mahali tukiwa na Rais wetu na watu wetu waweze kupata maendeleo zaidi Mungu awabariki Wabunge, Mungu akubariki wewe, Mungu

ambariki Rais wetu na sisi wote kwa pamoja tuweze kupita kwa usalama ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu kwa dua zako tunasema Amina nilishakutaja Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela dakika 10 atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta aliyoko Msekwa

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante lakini name pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kunipa uhai lakini pia nimshukuru Mwenyekiti wa Chama Mheshimiwa Freeman Mboge kuweza kunteua na kuniamini katika nafasi ya Baraza Kivuli kwa maana ya Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikipiga kelee sana kuhusiana na uhaba wa maji katika Mkoa wa Katavi katika Manispaa ya Mpanda, lakini ziko changamoto kubwa ambazo nimekuwa nikielezea baadhi ya miradi ambayo imechukua muda mrefu lakini Serikali hii ya Awamu ya Tano imeshindwa kutatua changamoto hizi. Kuna mradi wa umwagilaji ambao uko katika Jimbo la Kavuu katika Kata ya Mamba, mradi huu umechukua zaidi ya milioni 740. Lakini mpaka hivi tunavyoongea huu mradi umesimama haueleweki maana yake baada ya uzinduzi wa ule mradi kwamba umekamilika ulitoa maji siku mbili tu mpaka sasa ule mradi umesimama.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa jimbo hilo wanapata tabu wanasantu zaidi ya kilometra 20 kufata maji ambayo Serikali hii ya Awamu ya Tano mmeshindwa kutekeleza sera hiyo mnayosema kwamba asilimia 85 wananchi wa vijijini wapate maji safi na salama. Lakini ninyi mmeshindwa na asilimia 95 ambayo mnasema ni katika miji kwa hiyo sera hii imefeli na niombe sasa Serikali Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri umefanya ziara sana katika Mkoa wa Katavi lakini mpaka sasa hakuna kinachoeleweka mueleze watanzania aliyepiga hizi pesa ni nani na muwachukulie hatua kwasababu wananchi wanalamika, malalamiko yako mengi mnashindwa kuchukua hatua. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuna mradi wa maji ambao uko katika Jimbo la Tanganyika, mradi ambao upo katika Kata ya Kalema. Tunashangaa kabisa katika Kata ya Kalema kuna Ziwa Tanganyika lakini ziwa hilo nashangaa vijiji vinavyozunguka ukiangalia Kata ya Isengula ukienda Kapala Msenga, ukienda Kata ya Kalema na Ikola bado hakuna maji, yaani watu wapo katika Jimbo Ziwa Tanganyika kilometra chache tatu mpaka tano lakini kata hizi hazipati maji. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri nimepitia hotuba yako nimeona kabisa kuna mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba unawezesha huu mradi ambao wafadhili wake wanasema ni India tuombe muweze kulisukuma jambo hili haiwezekani watu wakaa pembezoni mwa Ziwa Tanganyika halifu wanakosa maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, maji ni roho ya uchumi, takwimu mbalimbali zimekuwa ziklelezea wanasema asilimia 19 zina matumizi umuhimu na uhitaji wa zaidi ya asilimia 19 wanakwenda kwenye viwanda lakini asilimia 70 inajikita katika uzalishaji wa kilimo na tunaelewa kabisa zaidi ya asilimia 70 ya watanzania wetu wengi wanajikita katika masuala ya kilimo.

Kwa hiyo, niombe kabisa Mheshimiwa Waziri miradi iliyokwama ukiangalia karibuni asilimia 80 ya watanzania walioko katika Mkoa wa Katavi wengi ni wakulima na wafugaji, tunahitaji maji kwa ajili ya majosho mengi ambayo yamesimama hayana maji ya kutosha na miradi ya umwagiliaji kwa ajili ya kilimo imefeli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini uhitaji wa maji katika Manispaa na Jimbo la Mpanda Mjini kwa takwimu ni kwamba tulikuwa tunahitaji zaidi ya lita 10,000 lakini mpaka sasa tunapata lita 4000 kwa hiyo, unawenza ukaangalia katika Jimbo ambalo lina wakazi zaidi ya 200,000 linapata maji kwa hizo lita 4000. Kwa hiyo, niombe Serikali kuhakikisha kwamba miradi mbalimbali ambayo tayari *RUWASA* pamoja na *MUWASA* wameshaanza kufanya michakato ya kuhakikisha kwamba wanaongeza visima, wanachimba visima tuweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, Iakini kuna miradi ambayo imesimama kwa muda mrefu masuala ya visima katika Jimbo la Katavi au Jimbo la Mpanda Mjini na Manispaa tuna visima zaidi ya 33 lakini visima 10 katika Kata ya Kakese ukienda Mwamkulu, ukienda Kasokola, ukienda Milala, ukienda Illembwe na maeneo mengine ambayo visima hivi havitoi maji. Kwa hiyo, wananchi wengi unakuta wanasaafiri ambao mnasema ni vijiji sera yenu mmeshindwa kuitekeleza wananchi katika Mkoa wa Katavi wanapata tabu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ulifika Katavi, Katavi hakuna ambacho tunajivunia katika Serikali hii kwasaababu hata barabara hizo za lami hatuna mpaka sasa kwa hiyo, mtu kama anaweza kusafiri umbali mrefu kwenda kutafuta maji na tunaamini kabisa kundi kubwa ni la wanawake ambao wanatafuta maji usiku na mchana na maji yenye wanayokwenda kuyapata ni maji machafu. Kwa hiyo, niombe kabisa Serikali mkakati wenu wa kuwezesha kuona kwamba mnamtua mama ndo kichwani utekelezwe japo umefeli na tutawashangaa watanzania kuwapa kura katika jambo hili mmeshindwa kutatua changamoto ya maji katika Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani tumetoa mawazo mbalimbali suala la dili za maji ambayo imekuwa ni changamoto inatakiwa tujifunze tuangalie nchi mbalimbali ambazo tumeona wameweza angalau kupunguza kodi na kuwapunguzia mzigo watanzania nchi ya Ghana, Kenya pamoja na China. Wao angalau kuititia janga hili la Corona ambalo tunahitaji maji safi na salama, maji yanayotiririka tuna vyanzo vya maji vingi kiasi kwamba Serikali tungeweza kujikita kuhakikisha kwamba tunazalisha na kutatua changamoto hizi za maji wananchi wangepata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika masoko yetu kuna mkusanyiko mkubwa wa watu kwenye masoko, hospitali, maofisi kwa hiyo, niombe Serikali kama mna mkakati dhabitii wa kutenga bajeti na kusaidia haya maeneo makubwa ambayo yana watu wengi, ukiangalia katika

Manispaa ya Jimbo la Mpanda tungehitaji tupate maji katika masoko yetu.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rhoda kunchela nakushukuru, asante mtaongea na *chief whip* atakuelezea vizuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta atafatiwa na Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi aliyeko humu ndani.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie hoja iliyoko mezani. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai wa kusimama mbele ya Bunge lako tukufu. Pia nawashukuru sana wapiga kura, wananchi wa Urambo kwa ushirikiano wanaonipa na naomba waendelee kunipa ushirikiano ili tuendeleze Rambo yetu.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwa niaba ya *TWPG* yaani Umoja wa Wanawake Bungeni kutoa pole kwa familia ya marehemu Mheshimiwa Dkt. Rwakatare alikuwa Mjumbe wa Umoja wa Wanawake wa Bunge hapa Bungeni. Pia nichukue nafasi hii kwa niaba ya Umoja wa Wanawake Bungeni kukushukuru sana kwa jinsi ambavyo unatutunza sisi kama Wabunge hasa kwa upande wa afya pia unatusaidia sana kuendeleza shule ya itakayokuwa Bunge *Girls High School* kazi inaendelea sasa hivi wanaezeka Mwenyezi Mungu akubariki kwasababu kazi inakwenda *speed and standards* na tayari maji yameshavutwa pale Mungu akibariki sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kuipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Tano jitihada kubwa inafanyika kwa lengo la kupunguza na hatimaye kumaliza tatizo la maji nchini na nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Prof. Mbarawa akisaidiwa na Mheshimiwa Aweso, Prof. Mkumbo na watendaji wote katika wizara hii kwa kweli kazi wanaifanya hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Prof. Mbarawa alikuja Urambo akawa na mukutano mzuri sana na wananchi wa Urambo lakini jambo ambalo wanaendelea kumkumbuka ni pale ambapo alitamka wazi kwamba kutokana na maji kwenda chini sana yaani *water table* iko chini sana maji kupatikana ni shida na hata yakipatikana hayadumu kwa muda mrefu aliwaahidi kwamba maji yatakuja kutoka *Lake Victoria*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Prof. Mbarawa tunakushukuru sana kwa niaba ya Serikali kwamba ultamka ahadi hii nakuomba leo utakapokuwa unahitimisha hotuba yako basi uendelee kuwapa moyo watu wa Urambo kwamba kweli maji yatafika kutoka *Lake Victoria* na kuwakomboa wananchi wa Urambo ambao wana shida kubwa sana ya maji.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kuishukuru Serikali mwaka 2017/2018 ilioa idhini ya kupata visima 30 vijiji ni kwasababu tuna shida kubwa sana ya maji basi na wakandarasi wengine wameshindwa kuendeleza miradi ya maji kwa kuchimba na kuacha kazi hiyo na kujiuzulu kabisa. Kwa hiyo, wizara naishukuru kwamba iliruhusu sasa chombo chake wenyewe *DDCA* wachimbe visima na wakatiliana mkataba tarehe 26 Machi, 2018 kwamba watachimba visima 30 katika Usoke Mjini, Usoke Mlimani, Ugala, Kiloleni, Kalembera, Katunguru, Kasisi, Itundu, Urassa, Mchinjioni, Kapilula, Tulieni, Vumilia, Uyogo, Usenga, Unzali na Ifuta. Wananchi hawa wanashubiri maji kwa hamu, tunakuomba Mheshimiwa Prof. Mbarawa utakuwa unahitimisha hotuba yako basi uagize hawa *DDCA* waende wakachimbe maji ili wananchi wa maeneo haya wapate maji ambayo ni muhimu sana katika maisha.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kuomba Wizara ya Maji kwa niaba ya wananchi wa Urambo tuna maeneo mazuri sana katika Kata ya Songambele na Kata ya Muungano maeneo ya Kalemela tuna maeneo mazuri sana ambayo wanaweza kujenga mabwawa makubwa yakahifadhi maji kwa sababu nimeona katika hotuba Serikali

ina nia ya kujenga mabwawa. Tunaomba na sisi maeneo hayo mawili katika Urambo yafikiriwe na sisi tupate maji.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nimeona ni la muhimu na wenzangu walichangia jana maji mengi sana yanapotea, naomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu kama ataona inafaa angeweka kama kipengele kimojawapo katika wale wanaojenga shule kwamba waweke tayari miundo ya kuvuna maji ya mvua kwasababu maji mengi yapotea bure kukiwa na miundombinu katika maeneo ya shule kama moja ya masharti ya kujenga shule itasaidia shule kuwa na maji kwasababu tunahimiza suala la usafi na utunzaji wa mazingira kwa kupanda mimea bila maji haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nafikiria kwamba kitu kikubwa ni kuwashukuru vlongozi wa wizara ya Maji kwa kweli wanafanya kazi na sisi wananchi wa Urambo tunawategemea, tunategemea kwamba mambo hayo mawili Mheshimiwa Mbarawa atawahakikishia kupata maji kutoka *Lake Victoria* pia kutuletea milioni 620,885, 000 ili *DDCA* wajenge au wachimbe visima katika maeneo hayo ambayo nimeyataja.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana naomba hayo yatekelezwe ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta kama nilivyokwisha kusema Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi atafatiwa na Mheshimiwa Ntimizi aliyeko Msekwa, Mheshimiwa Kapufi.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, awali ya yote kama wazungumzaji wengine walivyoanza nimshukuru Waziri najua kwa nyakati tofauti ameweza kufika Mpanda na anaijua jiografia ya Mpanda ameiona miradi mbalimbali ya Mpanda na kwa ujumla wake niendelee kusema tu kile ambacho tumekwisha kufanya kwa pamoja mkwamo haukosekani. Najua kuna zaidi ya visima 15 Mheshimiwa Waziri kuna fedha ambayo kwa

maana ya mamlaka wanaendelea kujikusanya taratibu ili kuweza kufunga pampu.

Mheshimiwa Spika, nilichokuwa naomba kutoka kwako Mheshimiwa Waziri msukumo wa wizara ni muhimu kwa kuwa kazi nzuri imekwishafanyika na wananchi wana imani kubwa. Mheshimiwa Waziri ukienda maeneo ya Milalashongo, ukienda Mpanda *Girls* kote huko visima vimechimbwa na vina maji ya kutosha. Najua ukisikiliza watu wengine wanaongolea habari ya uhaba ya maji katika maeneo yao sisi kwa maana ya Mkoa wa Katavi tuna bahati moja, vyanzo vya maji tunavyo vingi, tunazungukwa na vyanzo vingi vya maji. Kwa hiyo, nilichokuwa nakuomba sana Waziri kazi nzuri ambayo imefanyika manake kuna maeneo watu wanaona kisima kipo iliyobaki ni kufunga pampu tu kwa hiyo tusipoteze imani nzuri ambayo tumewajengea wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo kuna mradi wa Manga, Manga kasokola najua fedha zimeendelea kutolewa na wizara ambapo utekelezaji uko asilimia 68 zimetoka zaidi ya milioni 146 kati ya milioni 523 nauomba tena msukumo wa wizara ili tukamilishe mradi huo wa maji ya mserereko.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Mpanda kwa ujumla wake chanzo cha Ikorongo ni chanzo ambacho kinaendelea kutusaidia najua asilimia za maji kwa Mji wetu wa Mpanda ni asilimia 41 bado tuko chini naamini fedha ambayo imetolewa; na nikushukuru Mheshimiwa Waziri umeweza kutoa msukumo mabomba yamenunuliwa kutoka kiwandani kazi iliyobaki ni kuhakikisha mabomba hayo yanafika maeneo husika na kazi iendelee.

Mheshimiwa Spika, kutoka hapo tuna chanzo kizuri cha bwawa la Milala nimekuwa mara nyngi nikiongea hapa kile chanzo kinachohitaji ni kutunzwa na ni chanzo chenye gharama nafuu. Kwa hiyo, wakati wengine wanaangalia wakajenge mabwawa sisi bwawa tunalo iliyobaki tu ni kulitunza na kuhakikisha maji yale yanachujwa vizuri wananchi waweze kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, nimeona kwa kupitia hotuba ya waziri kuna eneo moja ambalo nimefarijika sana ukurasa wake wa 96 kwa maana ya mpango wa kuanzisha mfumo wa Taifa wa usambazaji maji kwa maana ya *National Water Grade* wataalamu wametupa mifano wametoa mfano wa China, wametoa mfano wa India, wametoa mfano wa Lesotho kwamba kwa kupitia huu mto mmoja wa Youngs uko china maji wanaweza kuyatoa kusini yakapelekwa kaskazini yanakwenda mpaka umbali wa kilometra 1150 kutoka kusini kwenda kaskazini. Ukiangalia kilometra 1150 mtu ametoka Dar es Salaam atataka kukaribia Mpanda.

Kwa hiyo, maana yake ni nini bado tuna uwezo wan chi hii kuiunganisha kwa mtandao wa maji kwa kupitia vyanzo tulivyo navyo, chanzo cha Victoria, chanzo cha Tanganyika na katika hili mradi wa India kama kwa mifano hii ambayo wataalam wako katika wizara wanatuambia kumbe uwezekano huo upo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wametaja hata mto mwengine huu wa Telugu Ganga ambao unapeleka mpaka umbali wa kilometra 406 sasa ukizungumzia 406 hawa watu wanalalamika kwamba ni mwambao wa Tanganyika, mwambao wa Victoria. Kwa kukopi mifano ya wenzetu walofanikiwa maana yake tuna uwezo wa kufanya kazi nzuri. Kwa hiyo, niendelee kuliomba hilo Mheshimiwa Waziri kwa mpango huu wa kuiunganisha nchi na twende mbali zaidi sisi vyanzo vya maji baridi tunavyo kuna nchi wanafanya kazi ya kubadilisha maji ya bahari, sasa sisi hatujafika huko kwamba twende kwenye maji ya bahari ya Indi tuyabadilishe kuja huku kwetu hatujafika huko lakini nchi nyingine zinafanya hilo na ni gharama yake kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi niombe hilo tulizingatie baada ya kusema hayo tuna mradi mmoja wa Kakese nilikuwa naomba sana hili eneo la Kakese lina watu wengi na kuna maji ya kutosha ni maji mengi tukiweza pale ni suala tu la kukamilisha mradi na hawa watu ukiwaliza wataalamu wanakwambia ndio katika ile miradi ambayo wanategemea fedha ya kutoka wizarani kwa maana ya

*force account.* Nilikuwa nakuomba Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri sana ambayo imeifanya kwetu ushatutembelea zaidi ya mara mbili mara tatu hilo tulilisahau.

Mheshimiwa Spika, na la mwisho si kwa umuhimu kuna suala la mradi wa Kanoge namba mbili ambao takribani ni wa milioni 780 tukifanikisha mradi huu tutaweza kuzungukia maeneo yote yamerukwa na maeneo mengine ambapo Mji wetu wa Mpanda unaendelea kukua kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sebastian Salmon Kapufi nilishakujataja Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi kule Msekwa na utafatiwa na Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi nami niweze kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa ahadi ya Ziwa Victoria alioahidi alipokuja katika Kata yangu ya Kigwa. Leo shughuli imeanza ya kuleta maji Kigwa na kupeleka kwenye Kata nne za Goweko, Igalula, Nsololo na Kigwa. Mradi wa takribani shilingi billioni 12 umeanza kutekelezwa katika Kijiji cha Kigwa.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa siku zote nikisimama na kulalamikia mradi huu kwa sababu ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Kwa usikivu mkubwa Mheshimiwa Waziri alikuja Jimboni kwangu akatembelea baadhi ya vyanzo vya maji, tukaenda mpaka Kigwa akafanya mkutano mkubwa wa hadhara, mwisho wa siku akaagiza mradi huu uanze kutekelezwa na sasa unaanza kutekelezwa. Kwa niaba ya wananchi wa Igalula, nashukuru sana. Tunaomba mradi huu uende kwa kasi kubwa ili uweze kuwanufaisha wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukurani kwa Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, mdogo wangu na Profesa Kitila na wataalam wote wa Wizara kwa kushughulika na tatizo la maji katika Jimbo letu la Igalula. Baada ya kilio cha miaka mine, sasa Igalula tuna miradi takribani sita inayoendelea na sasa wananchi wameshaanza kupata maji safi na salama kwenye baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, kabla ya hapo, tulikuwa tunapata maji kwa asilimia 20 kwa wananchi wote takribani 300,000 wa Jimbo la Igalula, lakini sasa tunaelekea kupata takribani asilimia 70 ya maji safi na salama kwa wananchi wenzangu wa Jimbo la Igalula.

Mheshimiwa Spika, iko miradi inaendelea, nashukuru inaelekea kukamilika na mingine imekamilika. Mradi wa chanzo cha maji cha Igalula tulipata *almost* shilingi milioni 500 na wananchi sasa wanapata maji. Kazi kubwa imefanyika pale, namshukuru pia Mheshimiwa Waziri wa Nishati, alinipelekea transfoma ya umeme pale na maji yanapatikana vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, ambacho nakiomba kwa Mheshimiwa Waziri, pale wananchi wanakunywa maji moja kwa moja kutoka kwenye bwawa, tunaomba sasa ijengwe pale *treatment plan* ili yale maji yaweze kuchujwa na wananchi wapate maji safi na salama ili kuondoa maradhi na magonjwa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, uko Mradi wa Maji wa Loya. Nilimsumbuwa Prof. Kitila sana kwa mradi huu, lakini leo nashukuru kusema kwa asilimia 90 mradi ule umekamilika. Tumepata takribani shilingi milioni 200 na wananchi wametengenezewa chemba takribani 20, sasa wanakunywa maji ya bomba toka dunia imeanza. Kwa hiyo, nashukuru pia kwa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, pia upo upungufu kidogo nataka niombe tuweze kusaidia pale. Kwanza tumejenga mradi ule

kwa kutumia sola ambayo ni vizuri lakini kwa sababu sasa umeme umefika pale, naomba pale kwenye chanzo tuweze kuweka umeme ili sasa chanzo kile cha sola kikisumbua ule umeme uweze kusaidia ili wananchi hawa takribani 12,000 wasiwe wanapata taabu ya maji.

Mheshimiwa Spika, pia kuna maombi ya takribani shilingi milioni 38, kwamba zile *center* za maji zimepungua pale *center*, kwa hiyo, wameomba shilingi milioni 38 ili kuongeza chemba nne, tano ili wananchi pale Kata ya Loya wote waweze kunufaika na maji.

Mheshimiwa Spika, pia tuna mradi mkubwa wa Tura. Tura tulikuwa tuna bwawa kubwa la maji ambalo lilikuwa halitumiki, lakini Mheshimiwa Waziri alikuja akaliona. Kwanza alistaajabu kwamba wananchi kwa nini wanapata taabu ya maji? Hapo hapo alitoa maelekezo na akatoa fedha za kuanzia shilingi milioni 100. Leo ninavyozungumza *treatment plant* inajengwa. Wanachokiomba sasa ni kupata fedha za mabomba na fedha za matenki ili mradi huu uende kwa pamoja kusiwe kuna kusuasua, kwa sababu kile chanzo ni cha uhakika kama Mheshimiwa Waziri alivyoona. Namshukuru pia Mheshimiwa Waziri aliweza kutoa fedha haraka za kusaidia upatikanaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho nizungumzie Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria ambao sasa unaendelea kutekelezeka. Kama nilivyosema nampongeza Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri kwa kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais, kwa sababu alivyofika siku ile Kigwa alitoa maelekezo hapo hapo. Leo mkataba kati ya *TSP* na mamlaka umeshasainiwa kwa ajili ya kuleta mabomba kuanza kuyatoa katika Jimbo la Tabora Kaskazini kuleta pale Kigwa.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kama nilivyosema; Tura mradi huu kwa sababu ya kwenda haraka nashauri fedha ya ujenzi wa tenki kubwa ambalo litajengwa pale Kigwa viendane sambamba. Tunapoanza kulaza mabomba kutoka kwenye chanzo kuja Kigwa, yakute basi tenki limeshakuwa tayari ili sasa na pesa za mabomba ya

kutawanya kwenye maeneo mbalimbali viweze kuwa vinakwenda *simultaneously*.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa sababu mradi huu utasaidia Kata nne, takribani watu 50,000, utakwenda katika vijiji vyote yya hizi Kata nne, naomba *speed* yake iongezeke kidogo ili kama alivyokuja Mheshimiwa Waziri kuahidi kwamba mradi huu utaanza haraka, wananchi waone kinachofanyika. Kwa sababu Mheshimiwa Waziri alipokuja pale wananchi walimwonesha mabomba na matenki yaliyojengwa takribani miaka kumi nyuma na hayajawahi kutoa maji. Wakasema isije ikawa mchezo huo huo wakadanganywa kwa sababu uchaguzi umekaribia.

Mheshimiwa Spika, naomba mradi huu uende kwa *speed* inayotakiwa ili mwisho wa siku wananchi waone kazi inayofanyika na mwisho wa siku manufaa ya maji haya ya kutoka Ziwa Victoria yawafikie wananchi hawa takribani 50,000 wa hizi Kata nne wanaotarajiwa kunufaisha vijiji takribani 20 katika hizi Kata nne.

Mheshimiwa Spika, leo mimi tofauti na siku nyingine, kikubwa nataka niishukuru Serikali sikivu kwa kazi kubwa ambayo imefanya, miaka minne nimekuwa nalalamika shida kubwa ya maji katika Jimbo la Igalula, Mradi wa Ziwa Victoria ulikuwa unakwenda kwenye Majimbo yote kasoro Jimbo langu, lakini leo Serikali imetekeleza kwa asilimia kubwa. Sasa inaonekana kabisa yale ambayo nimeyaomba, yanafanyiwa kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nashukuru, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi. Sasa Mheshimiwa Magdalena Hamisi Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko, dakika saba saba.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nakushukuru kwa nafasi uliyonipatia. Pia niendelee

kutoa pole kwa Watanzania kwa gonjwa hili la *Corona* ambalo limeendelea kutukumba.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri kidogo kwenye suala la *Corona*. Tunaomba Serikali iweke utaratibu wa kutoa *current information* kwa maana ya mwendelezo mzima wa hatua inayotokea kila siku kwenye suala la *Corona*, ule mwendelezo mzima wa kila siku.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo pia naona halijaangaliwa kwenye suala la *Corona* ni usafiri (*public transport*). Bado watu wanabanana, wanashikana huko kwenye magari mpaka wanakaliana, lakini pia hakuna *treatment* yoyote kwenye vile vyombo na inaweza ikawa ni njia moja kubwa sana kwa ajili ya kuweza kuangamiliza watu wengi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kwenye ushauri, Serikali itoe fedha ya kutosha na kuweka kipaumbele hiki kikubwa sasa hivi kwenye Taifa, suala la *Corona*. Ikiwezekana tu-scale down activities zile ambazo ni za miradi mikubwa ili tuelekeze nguvu kubwa kuweka fedha ya kutosha kwenye suala la *Corona*.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunaona Manesi wanakimbia mpaka wagonjwa. Tuangularie vile vifaa va kujikinga wapate vya kutosha, mazingra wanayofanyia kazi yawekwe vizuri, kwa sababu fedha bado ni kidogo kutokana na suala hili kuwa ni kubwa, tatizo ni...

**SPIKA:** Mheshimiwa Sakaya, siyo nia yangu kukukata, lakini nilitaka kukwambia tu kwamba Bajeti ya Afya ni kesho.

Pili, Waheshimiwa Wabunge mpaka sasa hivi mmekula *kobisi* (mmekaa kimya), hamjachangia chochote katika juhudzi za *Corona*, kupambana nayo. Kwa hiyo, nalo muwe mnalikumbuka. Nilitaka kukumbusha kwamba kuna nafasi pia kesho ukihitaji kusema utanipa taarifa tu.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Niende kwenye bajeti muhimu sana iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Maji ya Mwaka 2002 ni kupeleka maji vijini kwa wananchi chini ya mita 400. Pia Dira ya Taifa 2025 ni kuhakikisha kwamba Tanzania asilimia 95 ya vijiji vinapata maji. Dira fupi kwa maana ya malengo mafupi kuhakikisha kwamba vijijini tunapata asilimia 85 ya maji ifikapo mwaka 2020. Leo ni mwaka 2020, Wilaya ya Kaliua tuna asilimia 27 ya maji. Kwa hiyo, bado kwa maeneo ya vijijini hatujaweza kufikia hata yale malengo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, zipo juhudhi ambazo zimefanyika na kwa upande wa Mkoa wa Tabora na Wilaya ya Kaliua kutokana na jiografia, mradi ambao tunautegemea sana uondoe changamoto kubwa za maji ni Mradi wa Ziwa Victoria. Pamoja na changamoto ambazo zimefanyika, bado mradi huu umechukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, najua sasa hivi Serikali wako kwenye mchakato wa kutafuta Wakandarasi. Hebu mchakato huu ukamilike mapema tupate haya maji. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri *a-speed up activities* hizi ili kuhakikisha kwamba watu wanapata maji.

Mheshimiwa Spika, fedha nyingi ambayo imekuwa inatolewa kwenye maji ni fedha ya wafadhili lakini fedha ya Mfuko wa Maji haitolewi kwa kiasi kikubwa. Mwaka 2019 Wilaya ya Kaliua tulipata mradi mmoja wa maji ambapo ulikuwa unategemea Mfuko wa Maji kwenye Kata moja ya pale Usenye, kwenye Kijiji cha Maboa na Kijiji cha Mitimitano; walipangia shilingi milioni 600 pamoja na Kijiji kimoja cha Kazanaupate. Mpaka tunavyoongea leo, hawajapewa hata shilingi moja.

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi wa Kijiji cha Kazanaupate amekamilisha mradi kwa fedha yake mwenyewe lakini mpaka leo hajalipwa hata shilingi moja. Mradi ule mkubwa ambapo eneo la Usenye na Usinge kuna

shida kubwa sana ya maji, hawana namna nyingine; hata huu Mradi wa Ziwa Victoria haufiki kule, lakini mpaka leo hawajapewa hata shilingi.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri ajitahidi, anapokuja ku-*wind up* atuambie huu mradi wa Mitimitano na Maboa, ile fedha ambayo walitengewa inatoka lini kuweza kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanaweza kupata maji?

Mheshimiwa Spika, pia tulikuwa na visima 24 vya maji Wilaya ya Kaliua. Kutokana na Mkandarasi aliyekuwa ameletwa na Halmashauri kushindwa kugundua maji kutokana na ardhi yetu ilivyo, Mheshimiwa Waziri alivyokuja kututembelea mwaka 2019 Novemba, akasema kwamba ule mradi wa vijiji 24 utatekeleza na *EDCI*, lakini mpaka leo hakuna utaratibu wowote ambao umefanywa tuone kwamba wanatuchimbia.

Mheshimiwa Spika, vijiji hivi 24 ni maeneo ambayo hayana mradi wowote na pia Mradi wa Ziwa Victoria hautafika. Ni Kata ambazo ziko mbali sana na mjini. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* atuambie ni lini sasa mamlaka ya kuchimba visima hivi 24 kwa upande wa Kaliua itaanza kufanya kazi ili kuhakikisha kwamba Wana-Kaliua wanapata maji?

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba pale Kaliua tumeputa maji kwenye Kata ya Kaliua MJini. Maji yale yanatakiwa yapelekwe Ushokora pia ili waweze kupata maji. Tunaomba Serikali itusaidie kuhakikisha kwamba tunapata fedha ya kusogeza maji yale pale Kata ya Ushokora ili wananchi wa Ushokora pia waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mengine ambapo tualimbiwa tutapata mabwawa ya maji kutokana na kwamba kule hakuna kisima, hatuna chochote. Kama mnavyojua, Mkoa wa Tabora hatuna mto, hatuna chemchemi na maji yako chini sana; kwa hiyo, ukiweza kupata kisima ni cha kubahatisha. Tunaomba sasa Serikali

ituambie kwamba ni lini yale mabwawa ambayo yalikuwa yameainishwa kwenye Kata ya Ibwisi na Kata ya Usimba yataanza kuchimbwa ili wananchi wa maeneo yale waweze kupata maji?

Mheshimiwa Spika, kiukweli bado shida ya maji ni kubwa. Pamoja na juhudzi zinazofanywa na Serikali lakini bado shida ya maji ni kubwa sana. Wakati wa mvua sasa hivi unaweza kuona watu wana amani, mvua ikiisha ni kilio, ni maumivu, ni mateso kwa wanawake. Mbaya zaidi ni kwamba wanawake na watoto ndiyo ambao tunaathirika sana na kukosa maji.

Mheshimiwa Spika, ili dira hii iweze kufikiwa; na nashukuru kwamba mwaka 2019 tumeanzisha Mamlaka ya Maji. Nashukuru sana, wanafanya kazi kubwa, tatizo ni kwamba fedha haitolewi.

Mheshimiwa Spika, kwanza wale ni wataalam, ni ma-engineerna kiukweli wakipewa fedha wanafanya kazi. Tatizo ni kwamba fedha haitolewi kwa wakati. Tusipowapa fedha tutabaki tunawalaumu. Wana elimu zao za kutosha, wana ujuzi wa kutosha, lakini kama fedha haitolewi na Serikali kwa muda wa mwaka mzima wanakuwa *idle* kwa hiyo, wanashindwa kufanya kazi ambayo wamepang'iwa. Bahati nzuri wanatumia *force account*, kwa hiyo, wanaokoa sana fedha ambayo ingekwenda kwa wakandarasi, wanatumia vizuri, inatengeneza miradi mingi kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Unyamwezini kuna vijiji huko, maana yake kimoja amekitaja kinaitwa Kazanaupate, halafu kingine kinaitwa Mitimitano.

Mheshimiwa Esther Matiko, utafuatiwa na Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, dakika saba saba.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa nami nichangie kwenye Wizara hii muhimu sana kwa ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, maji ni uhai, maji ni uchumi. Tusipokuwa na maji safi na salama kwa mujibu wa Sera ya Maji ina maana tutakuwa na Watanzania wengi ambaao wataugua magonjwa yanayotokana na kutumia maji ambayo siyo salama, maji ambayo siyo masafi; kupata magojwa kama Kichocco, Amiba na mengine. Kwa kufanya hivyo, ina maana Serikali itaingia gharama kubwa sana katika kugharamia Watanzania ambaao watakuwa wameugua haya magonjwa, pia hawatakuwa na muda wa kwenda kuzalisha na hivyo kupoteza nguvu ambayo ingezalisha na kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile kukosekana kwa maji safi na salama tumeona kunasababisha Watanzania hasa akina mama kutembea umbali mrefu kutafuta maji. Tunaona akina mama wanapata madhara makubwa sana, siyo tu ya kubakwa, talaka, lakini pia wanavamiwa na wanyama wakali. Kwa hiyo, tumeendelea kupoteza akina mama wakiliwa na mamba kwa sababu ya kutafuta maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia kutembea umbali mrefu inapoteza nguvukazi ambayo ingeweza kwenda kuzalisha. Zaidi na la kusikitisha tumeshuhudia kukosekana kwa maji safi na salama kwa mujibu wa sera, watoto wetu wa shule wanatembea umbali mrefu sana kwenda kutafuta maji na hivyo kupoteza muda ambaao wangeweza kukaa darasanii na kujisomea.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali ione umuhimu wa kuwekeza kwenye maji, elimu na afya. Usipokuwa na maji safi usitegemee Taifa litakwenda kutamalaki kiuchumi. Tungeamua kutenga fedha tu kuhakikisha kwamba tunaboresha maji kwenye miji na vijiji.

Mheshimiwa Spika, hizi takwimu ambazo mmezitoa kwamba mmefikia hizo asilimia kwenye miji na vijiji ni uongo

kabisa. Wewe mwenyewe ni shuhuda, hata jana umelalamika. Hata mimi nikisoma, kwangu ni mji na hizi takwimu ambazo wanazitoa ni uongo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutoe uhalsia kwa Watanzania. Kweli tunapata maji kwa zile asilimia ambazo mmezi-*document* kwenye hotuba hii ya Waziri! Ni uongo mtupu! Ukweli ni kwamba bado kuna adha kubwa sana ya maji, akina mama wanatembea, maji ni machafu na kila kitu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye Jimbo langu la Tarime na Mkoa wangu wa Mara. Mkoa wa Mara ni kati ya mikoa ambayo inachangia pato kubwa sana kwenye Mfuko wa Taifa. Tuna Mbuga ya Serengeti ambayo katika mbuga zote Tanzania ndiyo inatoa pato kubwa sana kwenda kwenye Mfuko wa Taifa. Tuna Ziwa Victoria, tuna mgodi wa *North Mara* pale Tarime, lakini pia tuna mpaka wa Sirari. Mbaya zaidi tuna Ziwa Victoria ambalo ni karibu kabisa lakini asilimia kubwa ya Majimbo yote ya Mkoa wa Mara hayana maji safi na salama. Ni aibu!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukikaa hapa tukichangia hata mtu akija kutembelea Mara kwamba Ziwa Victoria, ukirusha tu kama kilometra moja au mbili, kwa mfano Rarya, Bunda na kwingineko, tumeshhindwa kupata maji safi na salama na mpaka leo watu wanatembea kutafuta maji *despite* kwamba tunachangia pato kubwa sana kwenye Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, Mji wangu wa Tarime tangu mwaka 2018/2019 Serikali iliahidi kupeleka visima 23 kwa ajili ya kutatua matatizo ya maji. Alikuja Mheshimiwa Waziri Mkuu na baadaye akaja Katibu wa Wizara hii, akaahidi kwamba wangepeleka visima 23. Mpaka ninavyoongea leo, nimeuliza maswali mengi hapa, Naibu Waziri Mheshimiwa Aweso anaahidi anasema ameshawaelekeza *DDCA* lakini mpaka ninavyoongea hakuna dalili yoyote ya hivi visima 23.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kujuwa wanavyokuja ku-*wind up* hapa waambie wananchi wa Tarime Mjini lini watapata hivi visima 23 ili kuweza kutatua changamoto ya maji kwenye zile kata za pembezoni?

Mheshimiwa Spika, pia tuna Bwawa la Nyandruma tangu enzi za Mjerumani ambapo Mheshimiwa Waziri angepeleka fedha pale wakaboresha lile bwawa lingeweza kuwa na mtandao wa maji angalau kwenye Kata za Kenyemanyori, Kitale na baadhi ya Mji wa Tarime pale.

Mheshimiwa Spika, kuna mradi wa Gamasara na Mheshimiwa Naibu Waziri ulitembelea pale. Mpaka leo ule Mradi wa Gamasara haujakamilika kabisa. Ninapenda kujuwa ni nini kinakwamisha ule mradi kukamilika?

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi kuliko yote ni huu mradi wa miji 28, Mji wa Tarime nao ulikuwemo kwenye huo mradi wa miji 28 na kwa kweli tulivyoona tulifurahi sana. Serikali ikasema, kufikia Septemba wangkuwa wamemaliza huo mradi wa kupeleka maji kutoka Ziwa Victoria ambapo ungeenda Tarime Mjini, ungepita; ina maana wananchi wa Ranya wangepata maji, Tarime Mjini yote ingepata maji kwa suluhisho la muda mrefu na baadhi ya Kata za Halmashauri ya Wilaya ya Tarime na zenyewe zingepata maji.

Mheshimiwa Spika, mara ya mwisho nimeuliza swalii hapa Bungeni, Serikali walisema wameshamalizia, matatizo yaliyokuwepo yamekamilika na kwamba. kufikia Septemba mradi utakuwa unakamilika. Mpaka sasa hivi ninavyoongea hakuna dalili yoyote kwenye hizi fedha za kukopa kutoka India.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kujuwa, tumeshindwa kutekeleza hata mpango wa muda mfupi wa visima 23 wa Bwawa la Gamasara? Sasa hata huu wa muda mrefu ambao tayari na mkopo kutoka India, mnashindwa kutekeleza ambalo lingekuwa ni suluhisho la kudumu la kupeleka maji katika Mji wa Tarime?

Mheshimiwa Spika, jana watu wameongea kwa hisia sana na tumekuwa tukiliongea hili kwa muda mrefu kwamba kunakuwa kuna ujisadi mkubwa sana kwenye miradi hii ya maji.

Mheshimiwa Spika, jana watu wameongea kwa hisia sana na tumekuwa tukiliongea hili kwa muda mrefu, kwamba kunakuwa kuna ujisadi mkubwa sana kwenye miradi hii ya maji. Pamoja na kwamba tunatoa hela kidogo sehemu nyingine hayafiki kabisa, lakini hata pale wanapopeleka hizo fedha napo unakuta miradi ambayo imetekelizwa mingine haitoi maji kabisa, mingine imepewa mradi wa fedha nyingi wakati imetumia hata robo au nusu ya hizo fedha hajifika.

Mheshimiwa Spika, kuititia Bunge lako, tunaomba sasa tui-take into task hii Wizara na Serikali kwa ujumla; kwanza ituambie upotevu wote wa fedha ambao tumeongelea, hata mwaka juzi nillongelea, wamechukua hatua gani *so far*? Hao watu ambao wamesababisha huo ujisadi wamechukuliwa hatua gani *so far*?

Mheshimiwa Spika, lakini pili, wana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Matiko. Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer na Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajabu atafuatia.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti iliyoko mbele yetu. Niendelee kuungana na Watanzania kuwapa pole familia ambazo zimepoteza wapendwa wao katika tatizo hili lililoko mbele yetu, janga la *corona*.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na kwamba, umesema kesho ni Wizara ya Afya, lakini sisi Wakristo tumefundishwa kuishi kwa imani hasa katika jambo ambalo katika akili ya kibinadamu tunaona kwamba, hatutaweza peke yetu bila Mungu. Wakati fulani ukisoma katika Kitabu

cha Samuel, Mungu aliwaambia Wana wa Israel na wakati fulani walisema kwamba, Hezekiah aliambiwa utakufa, lakini Hezekiah alivyomgeukia Mungu, Mungu akampa neema akamwongezea miaka 15 ya kuishi.

Mheshimiwa Spika, ukiendelea kusoma katika maandiko maeneo mengine tunaambiwa enyi wenye kumkumbusha bwana msimuache akae kimya mpaka atakapoifanya Yerusalem imara. Hatutakaa kimya tutaendelea kumuomba Mungu kwa sababu, jambo hili limewashinda binadamu, lakini kwa Mungu hakuna lisilowezekana. Mussa aliwaondoa Wana wa Israel alivyozungumza na Mungu wakati wote wanadamu walipata ujumbe. Mlango wa nchi yetu katika Mungu kutushauri na kututia moyo ni kupitia Rais wetu ni lazima tuendelee kumsikiliza kiongozi wa nchi katika ushauri ambaao anatupa kwa nia njema ya kututia moyo, illi tusonge mbele na tuongeze nguvu katika mapambano dhidi ya jambo hili ambalo naamini Mungu atatuepusha na tutakuwa salama. (*Makofii*).

Mheshimiwa Spika, mimi nashangaa kidogo, kila Mbunge anavyosimama hapa kusema eti hakuna chochote kilichofanyika katika tatizo la maji wakati kila mahali tunaona kuna mabadiliko angalau na nafuu ya mafanikio. Miaka hii mitano hakuna mahali hatuoni mradi wa maji ukitoa maji, Serikali imefanya juhudhi na nitasema maeneo machache ambayo kwa kweli, tutaipongeza Serikali sana.

Mheshimiwa Spika, tumeunda *RUVASA*, tumeanzisha *Force Account*, ukiangalia katika Kitabu cha Waziri maeneo mengi ukiangalia bajeti ya Wizara wakati wanatumia wakandarasi na bajeti wakati wanatumia *Force Account* kuna mabadiliko makubwa sana. Nafikiri Bunge hili lingetumika zaidi kushauri nini tufanye na mimi naomba nianze kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ifanye *auditing* ya miradi yote nchi nzima ya hali halisi ya maji. Inawezekana takwimu zinaonekana tumepata maji 85%, 95%, lakini

tunafahamu kuna miradi ambayo imetekelvezwa miaka mitatu, minne iliyopita sasda haitoi maji. Ni lazima tujifunze wapi tulipokosea ili tutakapotekeliza miradi mingine tusipate tena tatizo la kuwekeza fedha nyingi katika miradi, lakini wakati mwingine miradi hiyo haitoi maji. Naomba na limekuwa ni ombi langu kwa miaka yote nikiwa katika Bunge hili, Serikali ifanye *auditing* na kutupa *status* ya miradi yote ya maji nchi nzima kwamba, hali ikoje na kwa nini hali imefikia kiwango hiki. Serikali inaleta fedha nyingi sana katika miradi ya maji. Leo tusingekuwa tunalia tatizo la maji, lakini matokeo ya fedha tunazowekeza na mafanikio ya maji tunayoyapata hayalingani kabisa ni muhimu tukafanya utafiti tukaona wapi tulipokosea.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine naomba Serikali ifanye juhudhi ya kuajiri wataalam, kwa sababu sasa tumeanzisha *RUWASA*, kama hatutapata wataalam wa kutosha hata hiyo *Force Account* haitaleta matokeo kwa sababu tutakuwa hatuna wataalam wa kusimamia utekelezaji wa miradi yetu katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme mawili katika eneo la jimbo langu. Nimekuwa nikilalamika suala la maji katika Jimbo la Monduli kwa miaka yote minne ndani ya Bunge hili, lakini mnyonge mnyongeni haki yake mpeni; leo nazungumza nikiwa na faraja kubwa sana ya hatua kubwa ambayo Serikali imechukua katika jimbo letu. Nataka niwaambie na nimshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waziri wa Maji pamoja na Katibu Mkuu na Naibu Waziri wa Maji na wataalam wote wa Wizara ya Maji. Nashukuru mmeniletea kijana mzuri anayesimamia *RUWASA* ameleta mabadiliko makubwa sana katika jimbo letu kwa muda mchache. Nawaomba wawasimamie hawa wajamaa na wawathibitishe ili wasiwe makaimu, ili waweze kutimiza majukumu yao katika utaratibu uliokubaliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kuanzia Waziri alivyokuja juzi tumefanikiwa kupata zaidi ya milioni 400 ya harakaharaka katika kutekeleza miradi ifuatayo katika jimbo

letu: Mradi wa Monduli kwenda Enguiki, Mradi wa Lendikinya ambaao Naibu Waziri alifika na anaufahamu na Mradi wa Meserani Juu kwenda Meserani Chini. Miradi hii tayari fedha ziko kwenye *account* na naamini mpaka mwezi Mei au Juni tutakuwa na mafanikio makubwa sana. Ni kwa nini nisisimame kifua mbele kusema utekelezaji wa ilani katika eneo la maji imefanyika kwa kiwango kikubwa sana? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hao wanaobeza ndio haohao wanaotumia maji hayo. Hao wanaobeza ndio haohao wanaotamka miradi ambayo iko katika maeneo yao. Naiomba Serikali iendelee kusonga mbele, mafanikio ni makubwa sana.

Hata hivyo, katika eneo hili Mheshimiwa Waziri Monduli hatujawahi kupata kisima kwa sababu, maeneo mengine hatuna vyanzo vya maji, lakini maji yako karibu mita 100 kwenda chini maeneo ya Lemooti, Makuyuni, Lolakisare na Mswakini. Naamini wakitupa visima katika maeneo hayo tatizo la maji katika maeneo ambayo hatuwezi kuyafikia kwa maji ya mtiririko katika jimbo letu yatakuwa yamefikiwa kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ombi maalum kwa wananchi wa Monduli ni kwamba, tuna Mradi mkubwa wa Maji wa Arusha, bilioni 520. Uzalishaji wa yale maji ni mengi sana kulingana na uwezo wa uhitaji wa maji. Kwa hiyo, maana yake tuna maji mengi yanayobaki ya ziada. Naomba, kama ambavyo tumemwomba Waziri, ifanyike *studyili* maji yale yatoke Arusha Mjini yapite Kisongo, yapite Meserani, yapite Arkatan, yaende Lepruko, maeneo yote hayo ya barabarani yatapata maji na tutakuwa tumetatua tatizo la maji katika Jimbo la Monduli kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge wa Monduli. Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii kuchangia kwenye hoja hii muhimu sana ya maji. Maji ni muhimu sana na kwa kweli, kwanza ningependa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na Maafisa wote wa Wizara ya Maji. Kazi ambayo wanaifanya kwa kweli inaonekana na Mawaziri hawa wamezunguka karibu nchi nzima, sidhani kama kuna mradi ambao Mheshimiwa Profesa Mbarawa au Ndugu yangu Mheshimiwa Aweso hawaujui, lakini kwangu tu Muheza Mawaziri hawa pamoja na Katibu Mkuu wamekuja zaidi ya mara nne, hivyo, nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Rais alipopita Muheza mara ya mwisho alisema Muheza lazima mtapata maji na sasa hivi Muheza inanukia kupata maji na naamini mpaka mwezi ujao Muheza tutapata maji. Nasema hivyo kwa sababu, Mradi wa Pongwe ambao Mheshimiwa Waziri alikuwepo wiki iliyopita umefikia karibu 95%. Sasa mradi ule naamini kabisa maji yatakapoanza kutoka Pongwe, basi yatapunguza kwa kadiri kubwa sana tatizo la maji katika Mji wa Muheza.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu, Waziri alipokuwa pale na mpaka tunavyozungumza tanki ambalo limejengwa la lita laki saba limejaa maji na limejaa maji pale karibu mwezi sasa tangu alipotoka Waziri Mkuu. Sasa naamini kabisa kwamba, tatizo ambalo liko pale *pump* ambazo zipo zimekwishanunuliwa na zimefika Muheza tatizo ni kwamba, zinashindwa kufungwa kwa sababu, wataalam wa kufunga zile *pump* wanatoka *South Africa*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alifika na alitoa maagizo kwamba, *pump* zile zifungwe kwa njia ya teknolojia ili mafundi wetu waweze kufunga kwa sababu, wale wataalam wa kufunga zile *pump* wameshindwa kuja nchini kwa sababu ya tatizo la *corona*. Namshukuru sana, lakini mpaka sasa hivi bado agizo hilo halijatekelezwa na naomba alichukulie umuhimu wake na atoe *deadline* kuhakikisha kwamba, kweli *pump* hizo zinafungwa na maji yanaanza

kutiririka. Mabomba yote yameshafungwa kama alivyoona na kila kitu kiko tayari, ni *pump* kufungwa tu maji yaanze kutiririka kwenda Muheza, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, palepale tulisahau kumlipa mkandarasi mmoja wa kuunganisha bomba la Moa mpaka Pongwe. Alilipwa, lakini zile fedha zote zimechukuliwa na benki kwa hiyo anaomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuangalia namna gani anaweza kumlipa kwa sababu, tutakapounganisha bomba lile Moa mpaka Pongwe, basi tutaweza kuchukua maji yale ya Zigi moja kwa moja bila kuingilia maji ya Pongwe. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na naomba suala hilo aweze kulishughulikia inavyopaswa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwenye Mradi huohuo wa Pongwe, kwenye vitongoji bomba ambalo linapita kuna fedha karibu milioni 285. Naomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe fedha hizo tunazipata ili basi bomba hilo maji hayo yatakafunguliwa na bomba linapopita kwenye vile vitongoji basi, vitongoji vyote viweze kupata maji kwenye lile eneo. Naambiwa kwamba, kuna hela karibu milioni 150 ameshaziidhinisha, namshukuru sana, ili kazi hiyo ianzé kufanyika mara moja.

Mheshimiwa Spika, lingine, najua kuna *projects* nyingine ambazo ziko Muheza, kuna Mradi wa Kwemdimu, Kata ya Kisiwani na kuna Mradi wa Kiwanda, Kata ya Tongwe na kuna Mradi wa Zenet, Kata ya Pongwe, pamoja na Mradi wa Kirongo. Sasa nafurahi kusema kwamba, Mheshimiwa Waziri ameamuru kwamba, atalata milioni 150 kwa ajili ya Mradi wa Kirongo, lakini bado hazijafika. Pia kwenye hii miradi mingine mitatu Kwemdimu, Kiwanda na huu Mradi wa Zenet ambaao bado umerukwa, nilikuja kulalamikia kwamba, huu umerukwa labda kwa sababu ya majina Pongwe, Tongwe, Potwe sasa ikabadilishwa kidogo, lakini naomba kwamba, alirekebishe ili tuweze kupata.

Mheshimiwa Spika, miradi hii Mheshimiwa Waziri aliamuru iende kwa *Force Account*, lakini miradi hii tangu

aamuru iende kwa *Force Account* vifaa vyake bado havijanunuliwa. Sasa nishauri tu kwamba, *Force Account* ni nzuri sana, lakini inacheleweshwa sana na hiki kitengo kinachoitwa *Procurement*. *Procurement* tangu ameamuru ameambiwa kwamba, vifaa vinanunuliwa, basi hiyo *Procurement Department* imekalia tu, imekalia; sasa naomba kwamba, hii na yenyewe uangaliwe utaratibu wa kupewa *deadline* vinginevyo itaharibu mantiki yote ya kuona kwamba, *Force Account* haiwezi kufanya kazi vizuri bila ya hiki.

Mheshimiwa Spika, hiki kitengo lazima kiangaliwe kwa sababu kinaleta mkanganyiko mbaya kwa sababu, Mheshimiwa Waziri ameamuru tangu Novemba *last year*, lakini mpaka sasa hivi tunaingia Mei, bado vifaa havijanunuliwa kutoka hiyo *Department* ya *Procurement*. Sasa ni suala ambalo linatakiwa liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie sana ni kwamba, pamoja na kununuliwa vifaa kwenye *Force Account* bado hawapewi bajeti nyengine ya kuangalia kununua vifaa vingine vya kuchimbia mitaro, kuangalia *labour* watakaochimba na kuangalia vifaa vingine kama simenti ambayo inaweza kusaidia kuona mantiki hasa ya *Force Account*.

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa *RUWASA* pia umesaidia sana na umeweza kufanya kazi nzuri, tunaye Mkurugenzi Mkuu ambaye kwa kweli anafanya kazi nzuri sana. Sasa tatizo ni fedha, wapewe fedha kwa wingi ili waweze kufanya kazi hiyo kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, suala la Mradi wa India miji 28 Muheza ni mojawapo na mradi huu tumekuwa tunausubiria sana Mheshimiwa Waziri. Mradi huu naamini kwamba, miji hii 28 kama tutafanikiwa na kazi hii ikaanza, basi itapunguza tatizo la maji kwenye nchi nzima. Sisi Muheza mradi huu tunausubiri sana kwa sababu mradi huu ambao tutachukua kutoka Pangani utanufaisha karibu Kata 20 na zaidi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga hoja mkono. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Balozi. Mheshimiwa Kunti Majala utafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer Ramo Makani* ambaye yuko kule Msekwa. Dakika saba.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii muhimu. Naomba nianze na suala zima la kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutujalia uhai na hatimaye leo tunaweza kuzungumza kwenye bajeti hii ya maji na ni bajeti yetu ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, napata shida sana na takwimu za Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri kwenye suala zima la upatikanaji wa maji ametuambia kwamba, ni 70% kwa vijijini na 80% kwa mijini.

Mheshimiwa Spika, suala la upatikanaji wa takwimu hizo *RUWASA* ilipanga 2019/2020 ilipanga kutekeleza miradi ya maji 652. Katika hii miradi 652 *RUWASA* imeteketeza miradi 94 tu. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, 70% ya upatikanaji wa maji vijijini ameipata wapi? Mheshimiwa Spika, lakini wewe mwenyewe shahidi kwako una kamradi kamoja tu, sasa hiyo 70% Mheshimiwa Mbarawa ameipata wapi?

Mheshimiwa Spika, ni sisi tu Tanzania ambao bado Watanzania tunakunywa maji na mbwa, tunakunywa maji na ng'ombe, tunakunywa maji na tembo, tunakunywa maji na fisi, sisi Watanzania. Nchi iliyojaалиwa milima, mito, mabonde, maziwa, bahari na maporomoko, Iakini Watanzania wa nchi hii bado tunakunywa maji machafu tena yanayopatikana kwa shida. Kaka yangu Mheshimiwa Mbarawa kwa kweli, mimi nasikitika sana na sijui anamdanganya nani na ili iwe nini na apate kitu gani? Kwa nini asiseme ukweli hali halisi ya maji?

Mheshimiwa Spika, sisi tunatoka huko vijijini hali halisi ya maji tunajua; tangu dunia imeumbwa, mfano tu natolea

kwenye Jimbo la Chemba, tuna vijiji 114, tuna vijiji 48 tu ndio vyenye maji, vijiji 66 havina maji, Mheshimiwa Waziri anatuambia ana 70% ya maji vijiji. Mheshimiwa Waziri aweke wazi mambo hadharani, ili tujadili kwa pamoja tuone ni namna gani njema ya kuweza kulisaidia Taifa letu na sio kutuletea takwimu ambazo zinakwenda kufurahisha...

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti kuna Taarifa, inatokea wapi? Endelea, Taarifa.

## T A R I F A

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, nimwombe tu Mheshimiwa mchangiaji aache kutumia hayo maneno makali ya kusema Watanzania wanakunywa maji na mbwa, hili sio neno zuri kwa Mheshimiwa Mbunge kwa sababu, wananchi wanasikia. Niombe tu kwa ustaarabu wake, najua ni mstaarabu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwamoto anaomba maneno ya kunywa na mbwa na unaelewa Mheshimiwa Mwamoto anatoka Iringa, utoe tu hayo maneno ili uweze kuendelea Mheshimiwa kwa nia njema tu. (*Kicheko*)

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na najua tu baada ya mimi kusema kambwa na vimate vimemtoka na alikuwa anachungulichungulia kule chini akifikiri mbwa kaingia humu chini.

**SPIKA:** Ahsante sana, muhimu sana kwa sababu, huu Mwezi wa Ramadhan basi...

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, lakini niseme Watanzania bado tunakunywa maji na wanyama wa aina mbalimbali tuna-share nao. Sasa nilitaka niliweke hilo sawa, lakini...

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Nasikia kuna Taarifa, sjui inatokea upande gani hii? Ni Msekwa eeh?

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Ndio ni huku huku Msekwa.

**SPIKA:** Haya basi, mkiwa Msekwa muwe mnaniambia ni Msekwa. Ahsante, Mheshimwia Juma Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe Taarifa tu mdogo wangu Mheshimiwa Kunti. Kuwaambia Chemba vijiji 114 *almost* 57% hawana maji na ukisema Watanzania wanakunyuwa maji pamoja na mbwa na tembo maana yake anawachanganya na watu wa Chemba kwa sababu, nao ni Watanzania. Hii ni kashfa kubwa sana kwa Watanzania na ni kashfa kubwa sana kwa Wananchi wa Chemba pia kuwaambia wanakunyuwa maji na mbwa. Namwomba Mheshimiwa atumie lugha ya staha, awe makini na anapozungumza ajue anazungumza na watu gani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nkamia nakushukuru sana kwa Taarifa yako, lakini pia hili la mbwa tulishalifuta kwa hiyo, tusiliendeleze. Mheshimiwa Kunti hilo la mbwa usilijibu, unaweza ukajibu mengine kama unahitaji; Taarifa yako hiyo, ipokee.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nashukuru kaka yangu amekiri kwamba, Watanzania wananchi wa Chemba wana uhaba wa maji zaidi ya 57%, namshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee. Mheshimiwa Waziri kwenye Wilaya hiyo ya Chemba, alipeleka watu wa Bonde la Kati, akaahidi kuchimba visima kwenye vijiji vifuatavyo Cheku A, Mbarada, Churuku, Muungano, Tumbakose, Dirise, Ndoroboni, Manantu na Mpendo. Mheshimiwa Waziri ni miezi zaidi ya tisa tangu ametoa hayo maelekezo, *survey* imekamilika, lakini wananchi wale

wanaendelea kusubiri tu kila siku, hawaelewi hatma ya hivyo visima kwenye hivyo visima nilivyovitaja. Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anakuja kufanya majumuisho na kuhitimisha hoja yake nitaomba awaeleze Watanzania wa Jimbo la Chemba kwamba ni lini vijiji hivi vitakwenda...

Mheshimiwa Spika, ni miezi zaidi ya tisa tangu ametoa maelekezo hayo, *survey* imekamilika lakini wananchi wale wanaendelea kusubiri tu kila siku hawaelewi hatma ya hivyo visima kwenye hivyo vijiji nilivyovitaja. Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anakuja kufanya majumuisho na kuhitimisha hoja yake nitaomba awaeleze Watanzania wa Jimbo la Chemba kwamba ni lini vijiji hivi vitakwenda...

## TAARIFA

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa tena taarifa dada yangu na mdogo wangu Kunti. Manantu kuna kisima cha maji kirefu chenye mita 114, Kimetumika hata mimi nimekikuta kisima hicho alichimba Mzee Degera. Kina matatizo ya miundombinu ambayo tayari yanafanyiwa kazi. Birise kuna kisima kina matatizo kwa sababu kisima kile kina maji yenye chumvi. Handa kuna kisima cha maji cha muda mrefu, Serikali imezuia watu wasikitumie kwa sababu kina madini ya Urani. Mpendo kuna kisima na sasa hivi wanaanza kuki-*develop* kwa sababu kilikuwa cha muda mrefu, miundombinu yake ndiyo ina matatizo. Hamia hapo hapo Mpendo kuna kisima ambacho kina uwezo wa kutoa maji lita 25,000 *per hour* kama alikuwa hajui.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Juma Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, asilite maneno ambayo hayapo na sio ya ukweli.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, shughuli mnayoiona hii inawaelezea Oktoba inakuja. Hayo ni mambo ya Chemba hayo. Mheshimiwa Kunti Majala acha uongo.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nashukuru amesema visima hivyo ni vya siku nyingi na havitoi maji, ndiyo maana tunahitaji visima vipya na Waziri akasema vitachimbwa visima vipya. Kwa kuwa haendi kule, ndiyo maana hajui nini kinachoendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naomba niendelee na suala zima la majitaka katika Jiji la Dodoma. Suala la majitaka kwenye Mji wa Dodoma nimekuwa nikilisemea sana lakini naona mwendo wake ni wa kobe kama sio wa kinyonga.

Mheshimiwa Spika, watu waliokuwepo Dodoma awali na sasa ni vitu viwili tofauti. Ongezeko limekuwa kubwa lakini tunaona miundombinu mbalimbali Serikali ikiendelea kuiendeleza, hatuoni mpango mkakati na madhubuti wa kuhakikisha miundombinu inayoeendelezwa leo kwa mfano barabara, usambazaji wa maji safi, uwekaji wa maji takaa miundombinu yake inakuwaje. Nyumba zinaendelea kujengwa, miundombinu ya maji takaa haipo. Mheshimiwa Waziri hajaweza kulisemea hili vizuri, ongezeko la Dodoma na ujenzi wa kasi unaondelea kwa kasi kwenye Jiji la Dodoma, mkakati wa Wizara ni nini kuhusiana na kurekebisha ama kuweka sasa mipango thabiti ya kuweza kutuwekea miundombinu ya majitaka katika Jiji la Dodoma ni ipi?

Mheshimiwa Spika, kwenye suala zima la majisafi na salama kwenye Jiji la Dodoma, hali kadhalika nalo nimekuwa nikilisemea sana kwamba tumepata ongezeko la watu. Leo Dodoma tuna mgao wa maji Mheshimiwa Waziri, uko hapa hapa na Wabunge wote tuko hapa hapa, tuna mgao wa maji ambaeo hauna taarifa. Kisasa maji yanatoka saa 2 ikifika saa 11 yanakatika. Ilazo kuanzia saa 11 jioni, ikifika saa nne hamna maji. Nzuguni, hali kadhalika, Nkuhungu na maeneo kadha wa kadha. Kwa hiyo, Dodoma tuna mgao wa maji ambaeo hatujatangaziwa lakini bado sijaona dhamira yako

Mheshimiwa Waziri au dhamira ya Serikali ya ongezeko la watu Dodoma na upatikanaji wa maji safi na salama katika Jiji la Dodoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye suala zima la mabwawa. Tuna Bwawa la Farkwa ambalo tulikuwa tunatarajia kwenye bajeti hii tuweze kuona sasa ni lini bwawa hilo linakwenda kuanza lakini sijaona chochote kwenye hotuba yako Mheshimiwa Waziri, umelipa fidia baada ya kulipa fidia nini kinaendelea? Ujenzi unaanza lini? Hilo bwawa ndiyo mlituambia kwamba pia litapunguza kero ya maji kwenye Jiji la Dodoma, Bahi, Chemba pamoja na Chamwino. Sasa tunaomba utusaidie Mheshimiwa Waziri, Bwawa la Farkwa ambalo ndilo mkombozi wa Wilaya nne za Mkoa wa Dodoma, ni lini linafanyiwa kazi?

Mheshimiwa Spika, la mwisho. Dodoma ndiyo Makao Makuu ya nchi hii. Dodoma hii Waziri amekiri kwenye kitabu chake kwamba ni mkoa kame sana na hauna maji lakini ukija kwenye kiambatanisho namba 8 Mkoa wa Dodoma umepewa shilingi billioni 6 tu kwa ajili ya maji kwenye Mkoa wa Dodoma ambao ni kame. Tukienda kwenye mikoa mingine watu wana shilingi billioni 10, 12, huu upendeleo wa namna hii ni mpaka lini?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti muda hauko upande wako, tunakushukuru sana.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie na za kwako kwa sababu nasemea na Kongwa. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Eng. Ramo Makani ukiwa kule Msekwa ni wakati wako na utafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere ambaye yuko humu ndani. Mheshimiwa Ramo.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa ajili ya fursa hii. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya uzima na afya. Naipongeza Serikali ikiongozwa na Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. J. J. P Magufuli.

Mheshimiwa Spika, napongeza hata mhimili wa Mahakama pia kwa sababu utekelezaji wa majukumu ya Serikali unakumbana na changamoto nyingi za kisheria ambazo pengine nyingi huishia hata Mahakamani ikiwemo hata utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo tunayoizungumzia. Kwa hiyo, Mahakama kama mhimili kupitia Profesa Juma kama kiongozi na wenyewe pia nwapongeza.

Mheshimiwa Spika, nalipongeza Bunge chini ya uongozi wako. Siachi kupongeza chama changu, Chama cha Mapinduzi chenye llani ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu yote tunayoyazungumza hapa ni utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, upande wa Wizara, timu nzima ikiongozwa na Prof. Mbarawa akisaidiana na kwa karibu na Mheshimiwa Juma Aweso, upande wa wataalam Prof. Kitila Mkumbo na wataalam wote wa Wizara, wote nawapongeza.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo za jumla nitoe pongezi sasa kwa Wizara lakini nyuma yake ikiwemo Serikali kwa ujumla, kupitia bajeti hii ambayo tunajadili katika mambo manne. La kwanza, ni pongezi zangu katika upatikanaji wa fedha za maendeleo. Tumekuwa tukisuasua siku za nyuma lakini safari hii nimeona katika miaka hii miwili mfululizo tumeweza kupiga hatua. Fedha za maendeleo asilimia 74 si jambo dogo, zimeweza kupatikana na zimepatikana kwa wakati. Mwaka jana tulikuwa na asilimia 51, mwaka huu tumekuwa na asilimia 74, ni hatua kubwa, kwa hiyo tunapaswa kujipongeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili, ni hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kama ilivyoainishwa kwenye Sera ya Taifa

ya Maji, tunaelekeza huko kwenye mita 400. Pia tunaeendelea kusogea kwenye Dira ya Taifa kwa sababu tunavyotekeleza vizuri mipango ya muda mfupi ndio tunaelekea kutekeleza mipango ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, pia nisiache kuipongeza Wizara kwa kuokoa takriban shilingi bilioni 21 kwa kupitia utekelezaji wa miradi kwa njia ya *force account*. Nikiwa na muda hapo baadaye nitasema ubora wa *force account* na mapungufu yake machache ambayo yakirekebishwa tutapata *value* zaidi.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya maendeleo mwaka huu ni shilingi bilioni 705 ambapo asilimia 49.6 ni fedha za ndani. Nalo hili pia ni jambo la kuipongeza kama Taifa kwa sababu fedha za nje ni asilimia 50.4 lakini kisayansi maana yake ni kwamba hapa ni 50 kwa 50 kwa sababu kwa kukaribisha mahesabu 49.6 ni 50 na 50.4 ni 50. Hongera sana kama Serikali na kama Taifa kuendelea kutekeleza maelekezo ya llani ya Chama cha Mapinduzi ya kuendelea kupunguza utegemezi wa fedha kutoka nje katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo na mambo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, fedha hizi za maendeleo ambazo zinakwenda kutekeleza miradi 558 kwa bajeti hiyo ya shilingi bilioni 705 inajumuisha miradi ambayo ni ya Jimbo la Tunduru Kaskazini. Naishukuru sana Serikali kwamba miradi iliyopo kwa ajili ya Jimbo la Tunduru Kaskazini inaenda kutekelezwa barabara lakini nisisitize kwa miradi ambayo inaendelea kutekelezwa sasa hivi iweze kutekelezwa kwa kasi na ikamilike ili wananchi wa Jimbo la Tunduru Kaskazini waweze kunufaika na utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa kwanza ni wa visima vya maji virefu katika vijiji vya Huria, Darajambili, Namwinyu, Majala, Chileweni, Sisi kwa Sisi, Muhuwesi, Majimaji, Mtanya, Namakambale, Nakapanya na Nangapa. Maeneo haya Mheshimiwa Waziri atakumbuka tumezungumza na alisema ndani ya wiki mbili tangu tulipozungumza juzi kwamba fedha zitakwenda. Nashukuru sana alisema tutatekeleza miradi hii

kupitia Taasisi ya *DDCA*. Namkumbusha tu kwamba ndani ya kipindi hicho basi tuweze kuona utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, pia ipo taasisi binafsi ya *HUC* inatekeleza miradi ya visima 72 kwenye vijiji 42. Nao pia tunawashukuru na kuwapongeza kupitia Bunge lako Tukufu na nawaomba watekeleze miradi ile ili kuweza kusogeza karibu huduma ya maji kama ambavyo mipango ya Serikali imeelekeza.

Mheshimiwa Spika, uko Mradi wa Matemanga ambapo jumla ya fedha shilingi milioni 101 inaenda kukamilisha mradi ambao tayari umeshafikia asilimia 98 ya utekelezaji. Ningeweza kusema fedha ziende haraka lakini nimezungumza leo asubuhi kutoka nyumbani naambiwa fedha shilingi milioni 101 tayari zimekwishafika. Kupitia kwako na Bunge lako, naishukuru sana Serikali kwa kupeleka fedha hizo kwa wakati na kwamba sasa mradi huu unaenda kukamilika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, upo mradi wa usambazaji maji Tunduru Mjini ambako fedha za kuweza kuendelea kupiga hatua shilingi milioni 222, ambazo hizi sasa zinakwenda kutekeleza mradi kwa utaratibu wa *force account*, wakati nimepiga simu nilikuwa bado sijaweza kumpata mhusika lakini ninazo fununu kwamba na zenyewe zimekwishafika. Kwa hili nalo pia naishukuru Serikali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, haraka haraka niende upande wa changamoto. Ziko kadhaa lakini kama muda utaniruhusu nitazungumzia idadi kubwa kidogo lakini kwa sasa nizungumzie mbili ambazo ni kama kaka na dada. Ya kwanza ni ya upatikanaji mdogo wa fedha katika utekelezaji wa miradi. Nimesema kule tumepiga hatua lakini ukipiga hatua ni vizuri, ukipiga hatua kubwa zaidi ni vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakati Serikali inajipanga kutenga fedha nydingi zaidi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi, changamoto inayotajwa iko katika uwezo mdogo wa utekelezaji, usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji.

Hii ndiyo changamoto ambayo nataka niizungumzie zaidi kwa sababu kuwa na fedha ni jambo moja lakini namna ya kutumia hizo fedha ni jambo lingine.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Ooh!

**SPIKA:** Ahsante sana Eng. Ramo.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nakushukuru na naunga mkono hoja katika hatua hii nafikiri huo ndiyo utaratibu wakati wa bajeti kuu nitakuja kuona namna ambavyo maoni haya yatakavyokuwa yamefanyiwa kazi ili niweze kufanya maamuzi katika kura yangu. Ahsante sana. *(Makof)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Eng. Ramo Makani. Sasa ni Mheshimiwa Mwita Getere na atafuatiwa na Mheshimiwa Qambalo.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Maji. Kwanza nimshukuru Mungu kwa kutupa nafasi hii ya kukaa hapa miaka mitano na sasa tunaenda kuhitimisha na wewe ukiwepo hapa na sisi wote tumejaaliwa kuwa na afya nzuri. Tunaomba Mungu atusaidie kuepukana na hili janga ambalo liko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, niwaombe Watanzania wale ambao wanawaza kwamba siku zote katika nchi yetu huwa tuna vita yetu ambayo huwa tunapigana wenyewe, hata tulipopata uhuru sisi hatukuchukua panga wala bunduki kwenda porini, tulikaa tukawaza kwa kupitia Mwalimu tukapata uhuru kwa amani na leo tuna uhuru wetu. Hata tulipokwenda kwenye Vita ya Uganda tulitumia Watanzania kwa kuchanga mbuzi na kondoo vita ile ikaisha. Vita hii ya Corona kwa kutumia Mungu ambaye Rais wetu anatuongoza, tutaimaliza, haitakuwa na matatizo yoyote.

Kwa hiyo, watu wasitulazimishe twende kwenye sera ambayo wanaitaka wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Bunda, unajua jitihada inafanyika. Kuna mtu akizungumza hapa yaani *as if*kama sasa hii Serikali haifanyi jambo lolote la maji. Hata maji yanayotoka Dodoma hapa kwa wingi mtu anaona kama hayapo lakini wenyewe uchungu wa kuzungumza vitu ambavyo havifanyiki, sera hazitekelezeki ni wale wanaokataa bajeti. *Term* hii tujue kwamba nani anakataa bajeti halafu anasema amepeleka maji kwenye Jimbo lake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Bunda, matatizo makubwa ya maji yapo lakini jitihada imefanyika...

## TAARIFA

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Getere kuna taarifa, Mheshimiwa Ester.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Getere anasema wanaokataa bajeti ndio wanalalamika kuhusu maji na kwamba maji yameenda kote.

Mheshimiwa Spika, nafikiri wewe mwenyewe ni shahidi, jana pia ulilalamika kwamba hujapata maji, umepata kwenye kitongoji kimoja tu na ikakupelekea kusema wawe na *equal distribution* kwa Taifa zima, *wasi-concentrate* eneo moja moja. Kwa hiyo, nimpe tu taarifa kaka yangu, kama hajajiandaa kuchangia ni bora anyamaze kuliko kupotosha umma. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere, taarifa hiyo.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, siipokei kwa sababu mimi sijasema kuchangia ni kosa, nasema kukataa bajeti ni kosa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika Jimbo langu Serikali imefanya kazi. Amekuja Mheshimiwa Rais, tarehe 6 Septemba, 2018, ameagiza maeneo ya Nyamuswa kufanyiwa kuhusiana na suala la maji. Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri wamefika pale, nawapongeza sana kwa kufika. Waliagizwa maeneo haya yafanyiwe kazi vizuri, maji yapatikane kwenye Mji wa Nyamuswa, kwa hiyo kazi inafanyika ili maji yapatikane.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na mradi wa maji mkubwa wa kutoka Ziwa Victoria kuja Bunda na lengo lake ilikuwa ufile Bunda Mjini na uende Bunda Vijiji. Maadam mradi ule sasa umeshafika Bunda Mjini, naomba sasa uende Bunda Vijiji, tuna kata saba zenye hali mbaya sana ya maji. Kwa kuwa Waziri ameshatuma watu wa *survey* na wameshafanya *survey* ya kilometra 45 kutoka Ziwa Victoria kupeleka maji kwenye Jimbo langu, naomba sasa hiyo bajeti na hiyo tathmini iliyoanyika iingie kwenye bajeti ya mwaka huu ili wananchi wa Jimbo la Bunda wajue kwamba sasa wako mbioni kupata maji ya Ziwa Victoria na kwa sababu ni kilometra 45.

Mheshimiwa Spika, niseme neno moja tu. Tunaposema *REA* Vijiji hatuna maana kwamba kijiji A watu wote wana umeme, inawezekana katika kijiji hicho kina kaya 45 lakini watu wenye umeme ni kaya 20. Kwa nini tuisitengeneze aina ya maji kama ya *REA*? Kwani kuna shida maji yakinika Ziwa Victoria yakapita kwenye barabara yakaingia *centre* zote za viji vinavyohusika *at least* mwanakijiji wa eneo hilo awe anapata maji ambayo ana uhakika nayo?

Mheshimiwa Spika, kwa *style* hii tuliyonayo sidhani kama maji yanaweza kufika viji vyote. Mimi naomba kwenye Jimbo langu la Bunda iwe mfano, maji yapite kwenye maeneo ya barabarani, yaingie kwenye *centre* maalum za maji ili kila mahali mtu anapopata maji aweze kupata maji kwenye eneo lake. Tusianze kutengeneza mradi wa kupeleka kila mahali, kila kitongoji, itakuwa ngumu sana kupata maji kwenye nchi hii. Kwa hiyo, kwenye maji tufanye kama *REA*, *REA* imeenda vijiini, kuna watu wana umeme na wengine

hawana lakini yule anayehitaji kuwa na mashine ya kusaga atapata kwa urahisi. Kwa hiyo, niwaombe watu wa maji watengeneze *style* kama za *REA* za kupeleka maji vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba yale mabwawa yale sita ambayo wamefanya-survey na watu wa *DCCA* wameshaenda kuyaona basi kwa mwaka huu waanze kuyatekeleza ili watu wa Bunda waweze kupata maji. Tunataka yale mabwawa yatumike kama visima kwa sababu visima nya maeneo hayo huwa vinakauka. Maeneo ya Tingirima, Mihingo, Rakana, Nyaburundu, Kambugu, Salama A na wenyewe wapate yale mabwawa ambayo wameahidi kuwatengeneza ili waweze kupata maji kiurahisi.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu nimekiona hapa amezungumza Waziri vizuri kwamba changamoto kubwa tuliyonayo ni wakandarasi tulionao. Wakandarasi wetu wana uwezo mdogo, hili tatizo ni kubwa mno katika nchi yetu. Mheshimiwa Waziri kama inawezekana chunguza watumishi wote wa Wizara ya Maji na kama inawezekana watoe wote leta watu wapya, wengine waende vijijini na wengine wapumzike. Haiwezekani kuwe na idadi kubwa sana ya miradi ya maji ambayo haiendi na ukienda kuangalia wakandarasi, mtu anapewa mradi wa maji ya shilingi bilioni 20 wakati yeye hana hata huo uwezo.

Mheshimiwa Spika, najiuliza, kama mabomba ya maji, tunajua bei yake, kama vitu vyote nya maji tunajua bei yake kwa nini tusiweke bei elekezi kwenye vifaa nya maji? Haiwezekani tukawa na miradi mikubwa ya maji ambayo haimaliziki. Kila mahali kuna miradi ya maji na ya kisima haimaliziki. Pale Bunda tuna mradi wa maji wa *World Bank* toka 2013 mpaka leo haujamalizika. Waziri amekuja pale akafukuza mkandarasi, sijui walimrudisha bado anaendelea kufanya kazi pale, hauishi, wakachimba visima havikumalizika.

Mheshimiwa Spika, nafikiri imefika wakati sasa Mheshimiwa Waziri ukaweka bei elekezi kwenye miradi ya maji ili tujue bomba hili ni bei gani. Sasa hivi kuna kitu tunaita

*force account*, ukienda kwenye mradi wa maji bei halisi ya bomba ni Sh.240,000 lakini kwenye *force account* tunayoizungumza ni Sh.400,000/500,000. Sasa hiyo *force account* mbona haina maana inarudi ileile, ni *force account* jina lakini kwenye utekelezaji hali inakuwa ileile. Kwa hiyo, niombe sasa tuwe na bei elekezi kwenye shughuli za maji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, viongozi wa maji waliopo wanafanya kazi vizuri sana. Namshukuru sana Waziri, Naibu na Katibu Mkuu wanafanya kazi nzuri lakini bado watu wengine kwenye Wizara ya Maji wanawaza mambo ya *deal*. Kwa hiyo, tunaomba Waziri awachukulie hatua kadiri inavyofaa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwita Getere, nilishakutaja Mheshimiwa Qambalo Qulwi.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi jioni hii ili na nichangie hoja hii ambayo ipo mbele yetu. Nimshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na ardhi kwa kunipa uzima hadi muda huu.

Mheshimiwa Spika, tangu nimekuwa Mbunge kwenye Bunge hili sijaacha kuongea juu ya miradi ya maji iliyojengwa chini ya kiwango katika Wilaya ya Karatu. Miradi ya Vijiji ya Bugeri, Kansai, Getamok na Endonyawet. Leo naomba niongee tofauti kidogo, wananchi wa vijiji hivyo sasa wameanza kupata matumaini ya kupata huduma ya maji safi na salama. Mheshimiwa Waziri Prof. Mbarawa ulikuja Karatu mwezi wa tatu na tulitembelea baadhi ya miradi hiyo na uliwaahidi wananchi kwamba kabla hujarudi Dar es Salaam, fedha za baadhi ya miradi hiyo itakuwa imefika.

Mheshimiwa Spika, na hivi tunavyoongea tayari fedha za mradi wa Getamog zimekuja na mradi unafanyiwa ukarabati. na tumeambiwa wakandarasi hao wakitoka Getamog wanakwenda Endonyawet na nimeona kwenye

kitabu hiki utaratibu umeandaliwa na fedha za mwazo zimeshafika kwa miradi ya Kansei na Buger.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kwa hatua hii nishukuru kwa jitihada zako za kuja Karatu kwa sababu watangulizi wako wote wawili hakuna aliyethubutu kukanyaga Karatu kwa sababu wanajua tatizo lilivyokuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, tumefika hapo kwasababu tumefikishwa na watendaji walipo ama kwenye halmashauri zetu au Wizarani. Nadhani sasa ni muda mzuri wa kujaribu kufukua makaburi ili hao walitufikisha mahali hapo waweze kuwajibika. Hizi ni fedha za wananchi au ni fedha ambazo tumekopa, zinapotumika vibaya na baadaye tunapopata fedha kama hizi za Mfuko wa Maji au fedha kutoka EP4R tunazielekeza huko bado tunanyima vijiji vingine kupata huduma ya maji kama ambavyo ipo kwenye mikangu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Waziri jaribu kuangalia huko tulipotoka hivi ni nani wametufikisha mahala hapo, wapo wapi sasa hivi na wanafanya nini, warudishe hizo fedha kwasababu sio fedha zao, miradi wamejenga chini ya kiwango ndiyo maana ilikuwa haitoi maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamini Mheshimiwa Waziri uliahidi, wananchi walikuomba kwenye maeneo tuliyopita mradi wa maji wa Kijiji cha Mang'ora Juu na Mang'ora Chini. Eneo la Mang'ola Chini lipo kandokando ya Ziwa Eyasi, ziwa la maji ya chumvi kwa hiyo, linahitaji huduma ya majisafi na salama, wananchi walikuomba na tulipofanya kikao cha majumuisho pia tulikuomba kama viongozi tunaomba uweke kwenye mpango wako.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia kwenye kitabu miradi hiyo yote miwili haipo, naomba sasa iwe ni nafasi ya Vijiji vya Mang'ola Juu, Kijiji cha Mang'ola Juu kilichimbiwa kisima katika ule mpango wa vijiji 10 lakini mpaka leo zaidi ya miaka 10 bado wananchi hawapati huduma, kisima kina maji mengi

ya kutosha zaidi ya lita 40,000 kwa saa lakini bado maji yale yapo chini na wananchi wanateseka. Watu binafsi waliochimba maji karibu na hapo sasa hivi wanatumia maji yao.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye jambo la pili la kisera. Tulikaa kama nchi tukatengeneza Sera ya Maji mwaka 2002, Sera ambayo kwangu naiona ilikuwa *ambitious* tukasema tunawapelekea wananchi maji katika umbali wa mita 400 kutoka kwenye makazi yao. Nilitegemea hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri walau ingetaja hivi katika hizo mita 400 tulizokusudia leo mwaka 2020 tuko wastani wa mita ngapi kwasababu tunaweza kusema tumepeleka maji asilimia 85 kwa wananchi lakini bado wanakwenda ule mwendo mrefu. Hebu tuambiwe tufanyiwe tathmini katika ile mita 400 tuliyotarajia leo tupo kwenye 1,000 kwenye 800 au ndio tumefika kwenye hiyo 400 ambayo tulikuwa tumeilenga lakini tukipita vijijini maeneo mengi ya nchi hii bado tunaona safari ni ndefu ya kufika kwenye hizo mita 400.

Mheshimiwa Spika, wizara pia ina lengo na natarajia Waziri yupo makini kuhakikisha lengo lake hili analifkia la kuhakikisha walau asilimia 85 ya Watanzania wanaoishi vijijini watapata huduma ya majisafi na salama ifikapo mwishoni mwa mwaka huu. Tumeambiwa kwenye kitabu hiki ilikuwa 47 mwaka 2015, leo tunavyoongea ipo kwenye 70 na Waziri anategemea Desemba itakuwa 85. Kama takwimu zake zipo sahihi basi naomba nimpongeze kwasababu kazi kubwa itakuwa imefanyika.

Mheshimiwa Spika, pia nilikuwa ninajiuliza kama kwa hii miaka mitano tume-*parachute* kiasi hiki karibu asilimia 30, ile miaka mingine kule nyuma tulikuwa tunafanya nini na hawa ambaa tulikuwa tumewapa dhamana ya kuhakikisha tunapata majisafi na salama, kwa nini hawajafanya kazi hii na wengine bado tunao. Kwa hiyo, nadhani narudi kwenye hoja yangu ileile ya kufukua makaburi ili kila mtu ambaye kwa namna moja au nyingine amesababisha Watanzania wasipate huduma hii nzuri achukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la *RUWASA*, limeongelewa sana, *RUWASA* bado ni changa, ina changamoto nyingi, ina upungufu wa watumishi lakini pia ina upungufu mkubwa wa miundombinu ya majengo lakini pia zana za kufanya kazi. Niishauri Serikali huyu mtoto mchanga tumpe nguvu, tumsaidie na tumjengee uwezo, anaweza akatusaidia huko mbele tunapoenda kwasababu hata katika Sera ya Maji/Sheria za Maji ambazo tumezipitisha hivi majuzi, *RUWASA* amekuwa na nafasi kubwa sana lakini bila kumuwezesha akapata fedha za kutosha na akapata na rasilimali watu ya kutosha tutakuwa tunamuonea baadaye vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la tatu, Mheshimiwa Waziri vijana wako wa Bonde la Kati, Singida wamesababisha mgogoro ambaao mpaka sasa unaendelea kwenye Bonde la Eyasi. Bonde la Ziwa Eyasi ni maarufu sana kwa kilimo cha vitunguu lakini pia tumekuwa na mgogoro wetu wa muda mrefu wa chanzo cha maji cha Anged na Mto Mang'ola ambaao unapeleka maji kwenye Ziwa Eyasi.

Mheshimiwa Spika, vijana wako walipewa kazi ya kuja kuweka mipaka kwenye chanzo hicho cha maji na kwenye Mto Mang'ola unaoingia Ziwa Eyasi lakini walivyokuja wakiwa kabisa na hadidu za rejea za kazi hiyo badala ya kufuata Mto Mang'ola unaotoka kwenye chanzo hicho cha Anged na kwenda ziwani, wametoka pembeni na wakaenda kuweka *beacon* kwenye korongo la msimu kabisa ambalo halibusiani na mipaka ya Mto Mang'ola; jambo hilo limeleta mgogoro...

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Qambalo, muda haupo upande wako.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Paul Mzava atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Suleiman Kakoso aliyepo kule Msekwa.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kutoa mchango wangu kwenye bajeti muhimu ya Wizara ya Maji. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Wizara ya Maji mnafanya kazi nzuri; Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu mnafanya kazi nzuri sana na sisi tunawapongeza kwa kazi njema mnayoifanya.

Mheshimiwa Spika, moja ya mafanikio makubwa tunayoweza kujivunia kwenye Serikali ya Awamu ya Tano ni kuanzishwa kwa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira kwa maana ya *RUWASA* na namna ambavyo *RUWASA* imeanza kufanya kazi. Ukiangalia wizara inavyofanya kazi sasa hivi kuna mabadiliko makubwa sana kabla ya kuwepo kwa *RUWASA* na sasa hivi baada ya kuanzishwa kwa *RUWASA*.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali kwa kuanzisha *RUWASA* lakini pia tunawapongeza *RUWASA* kwa kazi nzuri ambayo wameanza kuifanya. Ni bahati nzuri kwamba pia tunayo timu nzuri sana ya *RUWASA* kwa maana ya Mkurugenzi *Eng. Kevegalu*, *Eng. Bwire* na *Eng. Maganga* wanajitahidi wanafanya kazi nzuri sana. (*Makoti*)

Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono hoja ya Wizara ya Maji na naunga mkono kwa sababu mwaka jana kwenye bajeti lakini pia wakati wa maswali nimekuwa na maswali mengi sana yanayohusiana na maji lakini pia nilichangia sana bajeti ya Wizara ya Maji. Tulikuwa na miradi miwili ambayo ilikuwa imesimama kwa muda mrefu kule Korogwe; mradi wa maji wa Lusanga wa millioni 687 lakini baada ya kuzungumza na Wizara mradi ule mkandarasi yupo kazini anafanya kazi na unaendelea vizuri, tunaishukuru sana Wizara. (*Makoti*)

Mheshimiwa Spika, pia tulikuwa na mradi wa maji wa Vuga Mlembule ambaao unapeleka maji kwenye eneo la Mlembule lakini pia kuongeza upatikanaji wa maji kwenye Mji Mdogo wa Mombo. Kabla ya *RUWASA* kuamua kutumia

*force account*, tulikuwa tunahitaji bilioni 1.7 kukamilisha ule mradi lakini kwa maamuzi ya kutumia *force account* tumeshuka mpaka kuja kutumia milioni 987.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara kwa uamuzi wa kutumia *force account* lakini pia niwashukuru kwa kuwa tayari mmeshaingiza fedha shilingi milioni 200 na tunavyozungumza sasa wataalam wapo kazini wameanza kufanya maandalizi ya kuanza kufanya kazi. Niwaombe tu *RUWASA* na Wizara kwa kuwa tulikuwa tunahitaji milioni 987 kukamilishmradi huu, milioni 200 bado ni kitu kidogo sana, hebu angalieni namna ya kutuungeza fedha ili kazi hii iende kwa kasi ikizingatiwa kwamba mradi huu ni wa tangu mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, pia niishukuru sana Wizara, tulizungumza mwaka jana niliomba fedha kwa ajili ya miradi ambayo illipata shida kutokana na mafuriko, tunashukuru kwamba Wizara imetupatia fedha zitakazotusaidia kurekebisha miundombinu ya maji ilioathiriwa na mafuriko kwenye maeneo ya Mazinde, Makuyuni, Kwa Shemshi, Kitivo na Kwa Mkole kule Kizara. Tunaishukuru sana Wizara na ndiyo maana ninaunga mkono bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Maji alifanya ziara Korogwe mwaka jana, ulikuta changamoto kubwa tuliyokuwa nayo kwenye kupeleka maji kwenye eneo tunalojenga Hospitali yetu ya Wilaya na vijiji vya jirani na hiyo hospitali. Tunaishukuru *RUWASA* na wewe Mheshimiwa Waziri, Wizara mmetupa milioni 200 na maandalizi ya kazi yameanza kufanyika, tunashukuru kwamba itatusaidia kwa kiasi kikubwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana kwenye mchango wangu nilizungumza sana kuhusu fedha za *PBR* zilichelewa, tunashukuru fedha zile zimekuja na zinatusaidia kufanya marekebisho ya miundombinu ya maji kwenye maeneo yetu mengi ndani ya Jimbo la Korogwe Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kipekee nishukuru kwa 1,065,000,000 mlizotutengea kwenye bajeti, zitatusaidia

kwenda kutatua changamoto za maji kwenye maeneo yetu kwenye vijiji mbalimbali kwenye kata karibu 10 za Jimbo la Korogwe Vijijini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi kubwa inayofanywa na Wizara, wapo wenzetu ambao wanatusaidia kusaidia wananchi wetu kupata huduma ya maji, wenzetu wa *World Vision* na *Islamic Help*. Nitumie nafasi hii na wao kuwashukuru kwa kuwa wamekuwa msaada mkubwa sana kusaidia kupatika kwa huduma ya maji kwenye Jimbo la Korogwe Vijijini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukurani hizi na pongezi nydingi nilizotoa kwa Wizara, nitumie nafasi hii niweze kushauri mambo machache. Jambo la kwanza niombe tu tuongeze *speed* ya utekelezaji, *speed* ya kufanya maamuzi lakini pia na *speed* ya kutekeleza miradi yetu. Haifai sana tunapeleka maandiko Wizarani yanakaa muda mrefu bila kufanyiwa maamuzi, inatuchelewesha kupeleka huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili; tunao mradi wa Mwanga – Same – Korogwe na mwaka jana tuliusema tena hapa na sisi Korogwe tunavyo vijiji vitano vyta Kata ya Mkomazi ambavyo vinanufaika na mradi huu. Kumekuwa na kuchelewa, natambua changamoto ambazo zilikuwepo kwenye mradi huu lakini bado wananchi wa Korogwe kwenye Kata hii ya Mkomazi hatujui ni lini sasa mradi huu utatufikia ikiwa ndiyo tupo mwishoni mwa ule mradi. Ningombaa Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie tu mradi huu unaendeleaje na tutarajie lini wananchi wale wa Kata ya Mkomazi watapata maji.

Mheshimiwa Spika, pia tulikuwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye ziara pale Mkomazi, hata kama mradi huu bado utachukua muda mrefu basi tuangalie namna ya kuwasaidia wale wananchi wapate maji hata kwa njia ya visima, tunaweza kuchimba visima tukawasaidia wakapata maji tukiwa tunasubiri mradi huu uweze kuwafikia.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni huu mradi wa miji 28; amesema Mheshimiwa Adadi kwamba mradi huu unawanufaisha watu wa Muheza, unakwenda mpaka Pangani na wenzetu wa Mji wa Korogwe lakini chanzo cha maji cha Mji huu wanachukua kwenye eneo ambalo kuna chanzo cha maji cha mradi ule wa *HTM* unaopeleka maji kwa wenzetu wa Wilaya ya Handeni. Tulifanya ziara pale na Naibu Waziri na Naibu Waziri kwenye chanzo kile cha maji kuna vijiji 4 vya Jimbo la Korogwe Vijiji vya kwenye Kata ya Mswaha ambavyo vinapakana, vipo karibu kabisa na kile chanzo.

Mheshimiwa Spika, na tuliomba kwamba kwa kuwa mnachukua maji pale kuwapelekewa wenzetu, na vijiji vile pia viweze kukumbukwa vipate huduma ya maji, Mheshimiwa Naibu Waziri ulituahidi kwamba hilo linawezekana lakini nakuhakikisha nimechunguliachungulia huko kwenye maandiko yenu na taarifa zile za usanifu sijaona.

Mheshimiwa Spika, naomba utakapokuja kufanya majumuisho Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri mtusaidie kwamba ni kweli mmekubali wale wananchi watanufaika na huu mradi? Itakuwa ni dhambi kubwa sana kuchukua maji kupeleka maeneo mengine, ni ndugu zetu hatukai na lazima yaende na ndio nchi yetu lakini itakuwa ni dhambi kuchukua maji kupeleka Handeni, Muheza na Korogwe Mjini na kuacha vijiji hivi vya karibu na chanzo cha maji vikibaki kuwa na huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ni kwa upande wa *RUWASA*, tumesema *RUWASA* inafanya kazi nzuri. Niiombe sana Wizara na *RUWASA* wenyewe tuangalie namna ya kuboresha mfumo wa manunuzi kwa watu wa *RUWASA*, bado tunayo changamoto ya manunuzi kwa upande wa *RUWASA*. Bodi ya manunuzi ipo makao makuu lakini kule mikoani na wilayani kuna kazi nydingi sana, mfano mzuri ni fedha za *PBR* zilitoka mwaka jana mwezi wa tisa lakini tumekuja kuzitumia mwaka huu mwezi huu wa pili na wa tatu. Na changamoto yake kubwa ni kwamba hatukuwa na bodi kwa ajili ya kuweza kufanya manunuzi. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mzava, sasa kama nilivyosema kabla Mheshimiwa Moshi Suleiman Kakoso kule Msekwa utafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Mbarouk ambaye yupo Msekwa pia, Mheshimiwa Kakoso tafadhalii.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nitoe shukrani za dhati kwa kunipa nafasi hii kuwa mionganii mwa wachangiaji kwenye Wizara hii muhimu ya Maji. Nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya kusukuma maendeleo pamoja na wasaldizi wake Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwa kulisimamia Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri Mheshimiwa Mbarawa na Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu kwa jitihada ambazo anazifanya za kusukuma miradi ya maendeleo hasa kule Jimboni kwangu Wilaya ya Tanganyika. Kwa ujumla tumeona Mheshimiwa Waziri akihangaini na Naibu wake karibu kila sehemu ya pembe ya nchi yetu umefanya ziara za mara kwa mara kwenda kuangalia miradi ya maendeleo ambayo inaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Jimboni kwangu nina miradi ya maendeleo ya maji mingi yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 6, kati ya hiyo upo mradi wa Kijiji cha Ifukutwa wenye thamani ya shilingi bilioni moja ambao unapeleka maji kwenye Kijiji cha Igala, Mchakamchaka na Kamtimbo. Mradi huu ulishaanza kutoa maji lakini kwenye vile vijiji viliviyolengwa bado miundombinu hajafika. Niiombe Serikali kupitia kwake Waziri na wataalam wake waharakishe ili miradi ambayo walilenga ipelekwe, ifanyiwe kazi na bahati nzuri fedha zipo, waisimamie kwa kina na wawasimamie wale wataalam.

Mheshimiwa Spika, mradi mwiningine ni wa Mwese, bahati nzuri Waziri tulienda naye ziara ya pamoja alishuhudia huo mradi, ule mradi unapeleka maji kwenye Kijiji vya Rwega na Lugenesi; pale Mwese ulishaanza kutoa maji. Tunaomba msukumo mkubwa wa Wizara kuhakikisha ule mradi unakamilika ili uwasaidie wananchi waweze kupata huduma ambayo walikusudiwa.

Mheshimiwa Spika, tunao mradi mwiningine wa Kijiji cha Kabungu wenyе thamani ya shilingi milioni 700, mradi ule ulishaanza kutoa maji kasoro kijiji kimoja ambacho ni Kijiji cha Kasinde. Tunaomba mradi huo uongezewe nguvu kwa ajili ya usimamizi ili uweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, tuna mradi wa Kijiji cha Kamjela wenyе thamani ya shilingi milioni 800, ulishaanza kutoa maji. Tunaomba miundombinu iweze kuongezwa kwenye maeneo yale ili wananchi wanufaike.

Mheshimiwa Spika, kati ya vitu ambavyo ninaipongeza sana Serikali ni mradi wa Kijiji cha Ikola ambapo Mheshimiwa Rhoda alikuwa anasema hakuna maji. Mradi ule unafanya kazi kubwa na tulishapata fedha kwa ajili ya kusukuma mradi wa kupeleka maji eneo la Kijiji cha Mchangani lakini Mheshimiwa Waziri alipofika Kalema alitoa fedha shilingi milioni 180 ambazo zinaanza kutekeleza mradi wa maji ambaa ulikuwa umechelewa kwasababu ya uzembe wa watumishi, hayo tunaipongeza Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa wizara ni kuharakisha ule mradi wa maji mkubwa ambaa ni wa Ziwa Tanganyika, mradi ule utasaidia sana Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda na mimi nitanufaika nao kwasababu unatoka Jimboni kwangu.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali, ule mradi uwekewe kipaumbele ili uweze kwenda kuwanufaisha wananchi wa Mkoa wa Katavi kwa ujumla. Mradi ule utanufaisha vijiji vipatavyo 10; Kijiji cha Ikola, Kijiji cha Itetemya, Kapala, Msenga, Kaseganyama, Kasekese, Nkungwi,

Sibwesa, Ikaka na vijiji ambavyo vitakuwa na uelekeo wa kwenda Mpanda Mjini. Kwa hiyo, naamini ule mradi utatusaidia sana wananchi kwa ujumla. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, upo mradi mwengine wa visima, nimeshapata visima 20, tunaomba kwenye eneo la Mishamo wafanye ukarabati wa vile visima vilivyochimbwa na Shirika la wakimbizi kipindi kile. Tuna visima vingi ambavyo vikipewa fedha tu kiasi, tunaamini tatizo la maji kwenye maeneo yale itakuwa limekamilika na itakuwa hadithi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni ushauri kwa Serikali, hasa kwa Wizara. Serikali inatenga fedha nyingi na kwa bahati mbaya sana timu ya wataalamu huko wilayani na mikoani kwa ujumla, kwanza hawana vitendea kazi. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali inapopeleka fedha iangalie na usimamizi wa wale watu ambao wanaenda kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, la pili ni uhaba wa watumishi. Kati ya Wizara ambazo hazina watumishi kabisa, Wizara ya Maji ni mionganini mwao ambapo watumishi wake ni wachache na fedha mnapeleka za kutosha. Kwa hiyo, naomba hili mliangalie. Naamini tukilifanyia kazi, Serikali itanufaika kwa kuwa na mchango mkubwa sana wa maeneo ambayo yatatolewa fedha kwa wingi lakini na wananchi watanufaika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naipongeza sana Serikali.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Moshi Kakoso. Sasa ni Mheshimiwa Mussa Mbarouk kutoka kule Msekwa pia.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Labda nami kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunijaalia afya njema nikaweza kuchangia katika Wizara hii ya Maji ambayo ni Wizara muhimu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea mbele, nitoe pole kwa chama changu kwa kuondokewa na Katibu Mkuu

wetu, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa ambaye pia alikuwa ni Mbunge wa Jimbo la Gando kwa takriban vipindi vine. Namwomba Mwenyezi Mungu amsamehe makosa yake na amweke mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nami nitakuwa ni mchoyo wa fadhila kama sikutoa pole kufuatia janga hili la *Corona* ambalo limeingia katika dunia, nchini na hata katika mikoa yetu na Majimbo yetu tulikotoka. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kwanza kuwapa pole ndugu zangu wa Tanga ambao zipo taarifa nimezipata kwamba wapo watu wamekufa kutokana na maradhi haya. Nawapa pole familia ambazo zimeondokewa na wapendwa wao. Nawataka watu wa Tanga waendelee kuchukua tahadhari kwa sababu haya maradhi siyo masihara, maradhi haya yapo na watu wameendelea kuteketea. Kwa hiyo, niseme waendelee kuchukua tahadhari za kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nizungumze kwamba maji ni bidhaa adimu au maji ni uhai na maji ndiyo uhai wetu ambao tunatumia au tunatumia maji katika kuendesha shughuli mbalimbali za uhai wetu na katika kitabu chetu kitakatifu cha *Quran*, Mwenyezi Mungu amesema kwamba *Wajalnaa Imai Kulishain-hai* kwamba, anasema Mwenyezi Mungu ametujaalia sisi maji kuwa ni uhai kwa kila kitu.

Mheshimiwa Spika, ukitazama katika mazingira yaliyotuzunguka ni kwamba maji ni kwa afya kwa kunywa, lakini maji kwa mazingira, maji kwa kunyweshea, hata katika vyombo vya usafiri tunatumia maji na hata kwenye janga hili la *Corona*; ili uwe salama, basi lazima unawe mikono kwa maji yanayotiririka. Haikuambiwa utumie *diesel* au *petrol* au mafuta ya taa, ni maji.

Mheshimiwa Spika, ipo kila haja ya kufanya bidii kwa nchi yetu kuhakikisha kwamba tunafanya mipango mizuri kwa kutenga bajeti kubwa ya maji na pia kuwafikishia wananchi wetu huduma hii bora ya maji. Wamesema waliosema kwamba baada ya miaka 58 ya uhuru, lakini mpaka leo

wenzetu wa vijijini maji hawana na katika baadhi ya maeneo madimbwi yale yale wanaokunywa wanyama maji na binaadamu wanatumia maji hayo hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa hii ni hatari kwa nchi kama Tanzania ambayo Mwenyezi Mungu ametujaalia rasilimali zote, ametupa aina mbalimbali za madini ya thamani ya vito lakini na madini pia yanayotumika viwandani. Vito kama *Road Light*, *Alexander Light*, *Red Garment*, *Grinto Marline* na kadhalika. Ukiija kwenye Almasi na Dhahabu ndiyo usiseme, tuna mpaka *Uranium*. Tunashindwaje sasa kutumia rasilimali hizi tukazipeleka katika masoko tukapata fedha tukapeleka maji vijijini?

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ilione suala la maji ni jambo muhimu. Maji ni uhai kama ninavyosema. Kwa hiyo, tusilete siasa wala masihara katika masuala ya maji. Wapo baadhi ya wenzetu, mtu anakuwa anaanza kwa kupongeza halafu akija mwisho naye anaomba maji kwenye Jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Kitwanga, jana wakati akichangia alisema, pamoja na kwamba ye ye ni Mbunge kutoka Chama Tawala lakini kwa suala la maji ikibidi atapiga kura ya hapana kwenye bajeti. Amesema hivyo kwa sababu ana mradi ambaao amekuwa akizungumzia miaka nenda rudi, watu Jimboni kwake hawana maji. Nami niseme, mimi Tanga sina shida kubwa ya maji kwa maeneo ya mjini; vijijini kuna miradi michache tu ambayo nitaitaja hapa ndiyo ambayo kidogo inasuasua.

Mheshimiwa Spika, tukianza kupongeza, tusipolelekeza Serikali vile inavyotakiwa, kuna hatari wataalamu wa maji wakaona si tumepongezwa Bungeni bwana! Mambo yako safi, tusemeni ukweli, tusiogope kusema ukweli, tuiambie Serikali ukweli. Wenzetu ndiyo watafanya bidii kuona kwamba kumbe Wabunge hili jambo linawakera.

Mheshimiwa Spika, tukianza kupongeza, tukiingiza siasa kwenye maji, wengine nawaapia Mungu na hii ni Ramadhani, hamtarudi humu kwa sababu ya kero ya maji.

Wananchi wakiona unazungumza kwa uchungu kuhusu suala la maji kwa sababu maji ni tatizo, wataona kumbe Wabunge wetu wanatutetea katika Bunge. Tukianza kuleta dana dana za kisiaza humu, kwa kweli ni hatari.

Mheshimiwa Spika, siipongezi sana Wizara ya Maji kwa sababu ni wajibu wake kufanya. Nami kwenye Kamati yetu ya PAC tumewahi kufika katika maeneo ya Jimbo lako la Kongwa, tumeona kuna mradi wa maji kule unaendelea vizuri, matenki yanetengenezwa. Pia tumefika Kondoa, tumeona maji yapo, sasa mimi niseme masuala ya maji...

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk pokea taarifa toka kwa Mheshimiwa Mlata.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Naam.

## TAARIFA

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayeendelea kuongea kwa sababu ye ye anatambua pia hata maneno matakatifu yanasema: "Zielezeeni neema za Mwenyezi Mungu kwa kushukuru." Yeye ametoka kuongea hapa kwamba hata ye ye anayo maji mjini Japokuwa bado ana changamoto. Hivi kwa nini huwezi kushukuru kwa kile ulichokipata ili uweze kuongezewa hata pale ambapo utahitaji?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, anapozungumza habari ya Mheshimiwa Kitwanga kusema Mheshimiwa Kitwanga amezungumza habari ya Jimboni kwake na Wabunge wanaoshukuru wanashukuru kwa Majimbo yao. Kwa hiyo, ye ye aache kuwaunganisha Wabunge kwamba wanashukuru au kupongeza pasipo kuwa na sababu. Wana sababu kwa kuwa wamepata maji Majimboni kwao na bado wanaendelea kuomba kwenye maeneo ambayo hawajapata. Hii ni kwa sababu haijawahi kutokea kwa Serikali hii mambo ambavyo yameenda kwenye Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Spika, naomba azungumze kwenye habari ya Jimbo lake lakini wote tukumbuke: "Zielezeeni sifa za Mwenyezi Mungu na riziki zake ili uweze kuongezewa."

**SPIKA:** Ahsante, inatosha kwa taarifa. Mheshimiwa Mussa Mbarouk pokea taarifa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, labda Mheshimiwa hakunielewa, hiyo taarifa yake siipokei. Kwa sababu nimesema napongeza kwenye Jimbo langu kwamba maji yapo. Labda kuna tatizo na kasoro ndogo ndogo. Kwa mfano, kwenye Jimbo langu tatizo kubwa ni bili za maji hazilipiki. Wananchi wangu wanashindwa kulipa bili za maji kwa sababu bei ya maji imekuwa ikipanda kila uchwao. Hata alipokuja Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe Mosi Machi, nilipata nafasi ya kuongea na nikaeleza kwamba Tanga maji yapo lakini bill za maji hazilipiki.

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe binafsi nilishaletewa bili ya maji kwa mwezi shilingi 400,000/=. Sasa ikija bili ya shilingi 400,000/= wakati *unit* moja ya maji ni *drum* tano; mapipa makubwa yale ya maji matano, ambapo bei yake ni shilingi 1,666/=. hivi kuna nyumba ambayo hata ina watu 30 wanaweza kumaliza mapipa matano makubwa ya maji?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaishauri Serikali bei ya maji ipunguzwe. Hata Mheshimiwa Waziri Mkuu kabla hajaja Tanga alizionomba Mamlaka za Maji zipunguze bei za maji kwa sababu pamoja na kwamba maji ni biashara, lakini pia maji ni huduma. Leo baadhi ya Wabunge waliochangia tangu jana na hata mimi hapa na wengine tunasema kutokana na hili suala la *Corona*, tunaiombia Serikali ipunguze gharama za bili za maji kusudi wananchi wetu waweze kunawa mikono vizuri, waweze kuoga vizuri na maji yatumike vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, sehemu nyiningine watu wanakwenda katika biashara hakuna maji, inabidi wakanunue maji. Sasa ikiwa mtu hawesi kununua maji, ina

maana hatoweza ile ndoo na *sanitizer* ya kusafishia mikono, tutakuwa hatupambani na *Corona* na *Corona* tutaiongeza. Kwa hiyo, natoa wito kwa Serikali tupunguze gharama ya bili za maji ili wananchi wetu watumie maji vizuri katika kipindi hiki cha janga la *Corona*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niendelee kuchangia kwenye miradi ya maji vijiji 10 kila Halmashauri. Kwenye Jiji la Tanga nashukuru; Mheshimiwa Mlata unanisikia nikishukuru! Nashukuru kwamba sasa kuna miradi ya vijiji 10 kila Halmashauri Tanga, tuna miradi miwili, mmoja uko upande wa kusini mmoja uko kaskazini.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mussa Mbarouk kwa kushukuru, ahsante sana. Anafuatia Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate, Mchungaji; hayupo popote. Basi naivusha hiyo nafasi inaenda kwa Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii ya Maji. Pia nianze pia kuipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufulsi kwa jinsi ambavyo inafanya kazi kwa umakini na umahiri mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nimemwona Waziri wa Afya na pia Waziri Mkuu yupo hapa, nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Afya na Naibu Waziri wa Afya kwa jinsi mnavyosimamia suala zima la kutafuta mbinu za kupambana na ugonjwa wa *Corona*. Hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye Wizara husika ya Maji. Wizara hii kwa muda mrefu sana imekuwa ni Wizara ambayo inapokea lawama nydingi sana kutookana na jinsi baadhi ya wataalamu ambavyo walikuwa hawatekelezi

wajibu wao. Nataka nikuthibitishie kwamba Prof. Mbarawa na Naibu wake wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mabadiliko makubwa sana na Mheshimiwa Awesu anamsaidia sana Profesa kwa kazi ambazo anazifanya. Baada ya kuanza kwa shughuli za RUWASA kumekuwa na utendaji bora na wenye ufanisi wa hali ya juu sana chini ya uongozi wa Eng. Tibegalo na pia chini ya usimamizi mkuu wa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara kwamba iendeleze mapambano hayo waliyoyaanza sasa. Kwa wasiomjua Mheshimiwa Prof. Mbarawa na Jumaa Awesu, kwa kweli hawa ni wakali sana kwa Wakandarasi na tumethibitisha jinsi wanavyofanya kazi hasa wanapotutembelea katika maeneo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Prof. Mbarawa aendelee kukaza uzi na Naibu wake na watu wa Wizara kuhakikisha upungufu mwingi ulikuwa Wizarani unaondolewa kwa jinsi ambavyo Wabunge wengi wamekuwa wakilalamika. Naamini baada ya uteuzi wake na kuingia Wizarani kumekuwa na mabadiliko makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naishauri RUWASA kwamba pamoja na kazi ilioanza lakini kasi iongezeke. Kwa mfano, sasa hivi kuna miradi ya *P4R* na miradi ya *BVR*. Miradi hii inachelewa sana kutekelezwa kwa sababu bado suala zima la manunuizi limekuwa haliendani na kasi mpya ya kutumia *Force Account*; bado hamjajipanga vizuri. Kwa mfano, mabomba ambayo yametakiwa kununuliwa sasa na RUWASA Makao Makuu na kusambazwa nchi nzima, bado kuna ucheleweshaji wa upatikanaji wa mabomba hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba sana mabomba haya yaharakishwe kupelekwa vijijini ili mradi huu wa *P4R* na *BVR* iweze kufanikiwa ili wananchi waondokane na tatizo kubwa la maji.

Mheshimiwa Spika, nina mfano katika Jimbo ambalo utekelezaji wa kazi za maji umefanyika vizuri sana na tuna miradi ya zaidi ya shilingi bilioni 11 katika Jimbo la Lulindi. Tulipata mfano, mkipata wataalamu wazuri wasimamie miradi hiyo vizuri na kwa 70% miradi hiyo inaendelea kutekelezwa vizuri. Nami nampongeza sana Mheshimiwa Prof. Mbarawa, Waziri wa Maji kwa maamuzi yake, pale alipoona ucheleweshaji wa Wakandarasi na kuamua kuiagiza RUWASA ikamilishe utekelezaji wa miradi hiyo iliyobaki.

Mheshimiwa Spika, namwomba tena Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba maamuzi yale waliyoyafanya yasimamiwe ili miradi ile iweze kukamilika. Pia nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri wa Maji kwamba kwa mfano katika Jimbo langu la Lulindi kuna tatizo kubwa sana katika vijiji vinne ambavyo Mheshimiwa Prof. Mbarawa nilishampa taarifa; na nihaendelea kukumbusha kwenye vijiji vile vya Mchoti, Utimbe, Mhata pamoja na kile cha Nyololo ambao hawana maji kabisa na mitandao hii ya maji haiwafikii kabisa. Naomba sana kupitia RUWASA vijiji hivyo viweze kupatiwa visima hivyo ili wananchi waweze ku-*enjoy*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Profesa Mbarawa anakumbuka Mheshimiwa Rais alipofika, wananchi kupitia kwangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Lulindi tuliiomba Wizara na Serikali kwa ujumla kujenga matenki manne muhimu sana katika miradi hii ambayo inatekelezwa hivi sasa ili kuhakikisha wananchi wale wanapata maji kwenye Kijiji cha Mkululu, Mbululu, kwenye Kijiji kile cha Mpeta, pamoja na kile Kijiji cha pale cha Mkangaula.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Naibu wake Mheshimiwa Aweso, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Maji nawatachia utendaji wa kazi wa hali ya juu wenyewe ufanisi wenyewe mabadiliko ili Watanzania waondokane na tatizo kubwa la maji linalowakabili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bwanausi. Sasa naomba Mheshimiwa Jitu Soni uongee kwa muda wa dakika tano tu kutoka kule Msekwa.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia siku ya leo. Naomba nichukue fursa hii kwanza kuipongeza Serikali lakini pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yao nzima kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe pamoja na Mheshimiwa Chenge kwa kipindi kile kunipa moyo na kunisaidia kuhakikisha kwamba suala hili la kutumia *Force Account* linaingizwa katika sheria na sasa tumeona mafanikio makubwa katika miradi mbalimbali ya Serikali kutumia mfumo wa *Force Account*. Naishukuru Wizara ya Maji kwa kukubali kutumia *Force Account* katika miradi yake mbalimbali na sasa naamini kabisa italeta tija kubwa.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba, kuna maeneo machache niweze kuishauri Serikali na hasa Wizara ya Maji. Moja, nilikuwa naomba Serikali iangalie namna ya kuweka mfumo ule wa takwimu. Leo hii takwimu inachukuliwa kwamba *point* moja ya maji inahudumia watu 250 katika eneo moja.

Sasa kama utaweka *point* nyingi kwenye eneo moja na idadi ya watu ikawa ni chache, ukichukua kwa ujumla kwamba idadi ya *points* zinazotoa maji kwenye Jimbo labda ni *point* 2000 na idadi ya watu ni kiasi fulani, unapata asilimia kubwa ya watu ambao wanapata maji. Hiyo inadanganya kwa upatikanaji wa asilimia ya maji.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba Wizara imekubali itaifanya kazi ili irekebishwe kwa sababu, hiyo inaathiri pia kwamba Jimbo lako kama linaonekana lina *points* nyingi za maji, lakini idadi ya *population* mahali maji yako ni chache, inafanya bajeti yako isipewe maji kipindi hicho; mwenzako anaonekana hana bajeti. Kwa hiyo, Wizaraimeahidi kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, pia naiomba Serikali iangalie namna ya kuondoa kodi katika mitambo ya kuchimba maji na mabwawa ili gharama hizo za uchimbaji ziendelee kuwa ndogo na tuweze kuchimba mabwawa na visima vya maji kwa bei nafuu zaidi. Hapo hapo pia *pump za solar* zikiwa za umwagiliaji hazina kodi, ikiletwa kama kawaida, miradi ya maji huwa inatozwa kodi.

Mheshimiwa Spika, tukiondoa kodi itasaidia miradi mingi ambayo Wabunge wengi wamelalamikia katika maeneo mbalimbali. Tunapotumia umeme wa kawaida gharama za uzalishaji wa maji inakuwa kubwa, lakini tutakapofunga *pump za solar*gharama zile zitakuwa ndogo. Ile gharama ya mwanzo ya kufunga itakuwa ni kubwa, lakini baada ya hapo running cost itakuwa hakuna, itapunguza zile gharama na wananchi watapata maji kwa bei nafuu zaidi.

Mheshimiwa Spika, niishukuru Wizara kwa kuwa imekuwa karibu na Kamati na imepokea ushauri mwingi wa Kamati lakini niishukuru pia Serikali kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha Mradi wa Maji wa Minjingu Darakuta. Pia kwa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Magugu kwa kutoa milioni 500 na zaidi ya hapo miradi mingi katika jimbo sasa inaendelea kuboreshwa na fedha zinaendelea kutoka.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuiomba Serikali na nishukuru kwamba, katika ile tulishauri kwamba zile taasisi za kusimamia maji ndogo ndogo zile Bodi za Maji zimeunganishwa sasa kuwa katika Bodi moja. Naendelea kuishauri Serikali waangalie maeneo mbalimbali ambayo kuna Bodi ndogo ndogo ambazo zinapandisha gharama, basi ziunganishwe kuwa Bodi moja kubwa ili ziweze kufanya kazi vizuri kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo *RUWASA* tuangalie namna ya kuiongzeza bajeti ili iweze kufanya kazi vizuri zaidi, kwa kutumia huu mfumo wa *Force Account* naamini kabisa kwamba miradi yetu mingi itaendelea

kuboreshwa kwa gharama nafuu na maeneo mengi yatapata maji.

Mheshimiwa Spika, ombi langu lingine ni kwamba, mabonde haya tuendelee kuwapa bajeti ya kutosha, ili waweze kuongeza vifaa na watalaam ili waendelee kushauri katika maeneo yao kupima maji na kupata maji safi na salama. Pia kushauri wananchi mahali pa kuchimba visima.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jitu Soni. Sasa nikuombe Mheshimiwa Charles Kitwanga kwa dakika tano, baada yake Mheshimiwa Naibu Waziri Maji na Mheshimiwa mtoa hoja atafuatia.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza nianze kwa kuishukuru Serikali yangu ambayo ni sikivu. Kwa leo niseme naunga mkono hoja asilimia mia moja, yale ambayo niliyasema jana Mheshimiwa Mbarawa ambaye alikuwa bosi wangu wakati nakuwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, tumeongea tumekubaliana na ataongea kuelezea jinsi ambavyo nyuma kulikosewa, lakini yeye mwaka 2017 hakuwepo maskini wa Mungu. Sasa haya yametokea na kwa vyovyyote vile yeye sasa hivi anajitahidi sana kurekebisha. Mheshimiwa Aweso nimekwenda naye Misungwi amefanya kazi kubwa sana kama miezi michache iliyopita na vilevile Mradi wa kutoka Ihelele Mbalika hadi Misasi anaendelea kuufuatilia kwa karibu kama alivyoahidi na kwamba maji yataanza kutiririka kama alivyokuwa ameahidi.

Mheshimiwa Spika, vilevile wananchi wa Usagala pamoja na kusubiri mikataba, lakini kuna *alternative* ya kuhakikisha maji yanatoka sasa kutoka Buhongwa yatiririke mpaka yafike Usagala sasa ukishapewa si ushukuru tu. Uendelee kulalamika na sasa hivi wale waliokuwa wananchukulia mimi ni kama hoja, imekula kwao. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na naomba sasa nimkaribishe aje aweke jiwe la msingi kwenye Makao Makuu ya Halmashauri yetu ya Misungwi. Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles Kitwanga, habari ndiyo hiyo, mliokuwa mnachekelea imekula kwenu. Ahsante sana Mheshimiwa Kitwanga. (*Kicheko*)

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara ya Maji, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenyе ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka minne, Serikali kupitia Wizara ya Maji imetekeleza miradi mingi ya maji. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya imetekeleza kwa ufanisi mkubwa miradi ya vijiji vya Mbawi, Jojo, Swaya, Lupeta, Haporoto, Idimi, Horongo, Itimu, Mwamplala, Izumbwe, Iwindi, Mwashiawala na pia mradi mkubwa katika Mji Mdogo wa Mbalizi. Miradi yote hiyo imetekeliza katika kipindi hiki cha Awamu ya Tano, hata hivyo kuna miradi inayoendelea kuboreshwa katika Kata za Inyala, Illembu, Maendeleo, Mshewe na Mjele ikiwemo miradi ya ilokuwa ya DANIDA.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo makubwa, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya bado kuna changamoto kubwa ya maji salama kwa wananchi.

Pamoja na kuwepo kwa vyanzo vingi vya mseleleko (*gravity*), asilimia kubwa ya vijiji havina maji salama. Napendekeza Serikali itekeleze miradi ya maji kwa mpango wa *force account* ambao umeonesha mafanikio ya kupunguza gharama za miradi na pia utekelezaji ni wa haraka na kwa ufanisi mkubwa. Katika kipindi hiki tunapopambana na janga la *corona virus (covid-19)*, tumejifunza umuhimu wa maji hasa kwenye zahanati, vituo vya afya na mashulenii na hivyo Serikali iongeze msukumo wa kupeleka maji hasa kwenye maeneo haya ya huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto za tabia nchi, kumekuwepo na uharibifu mkubwa wa mazingira na ongezeko la upungufu wa vyanzo vya maji. Uharibifu unaotokana na shughuli za kibinadamu umepelekea misitu mingi kuharibiwa na uchomaji moto, ukataji mkaa na hata kilimo kwenye vyanzo vya maji. Napendekeza Serikali longeze msukumo wa Wizara za Maji, Kilimo, Maliasili na Mazingira kufanya kazi kama timu moja ili kukabiliana na janga hili kubwa ikiwemo ujenzi wa mabwawa makubwa katika maeneo yanayokumbwa na mafuriko. Ziwa Rukwa linaathirika sana na kujaa mchango na udongo unaosombwa na mito kutokana na mmomonyoko wa udongo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, nianze na suala la maji Mbarali. Kulikuwa na mradi wa maji na kwa muda mfupi chujio liliharibika na kusababisha wasiwasii wa kutokupata maji salama kwa wananchi wa Mbarali. Maji yamekuwa ni shida hasa Mkoa wa Mbeya sehemu yenye vyanzo vingi vya maji hivyo wananchi mpaka sasa hawana maji salama ya bomba.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Mpandapanda Wilaya ya Rungwe wananchi walijichangisha na kuweka miundombini ya mabomba na kujenga tanki bila msaada wa Serikali, ninaomba sehemu iliyobaki wananchi hawa wapewe fedha na kumaliziwa mradi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukataji wa maji, tunaamini katika ukusanyaji wa maduhuli ya maji kuwa ni muhimu kwa maendeleo ya nchi lakini kwa wananchi washio vijijiini mfumo wa kulipa maduhuli kwa kutumia mitandao imekuwa changamoto sana kwa watu wengi hasa vijijiini na kupelekea wengi kukatiwa maji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mabomba ya maji naomba Wizara isimamie wakandarasi waweke mabomba imara na wasikwepe gharama na kuweka mabomba yanayopasuka na kupoteza maji njiani hivyo kupoteza maji mengi.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, maji ni uhai, huwezi kujua dhana hii mpaka pale ukose maji. Pamoja na juhudini zilizopo ni lazima Wizara kupitia Serikali kuweka ulazima kwa watu wote kupata maji safi na salama na kwa maana hiyo bajeti uielekeze kutumia maji ya mvua, maji ya maziwa ili kuweza kuhakikisha wananchi wote wanapata maji.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lazima Serikali ishirikishe wananchi kulinda miundombinu ili kuhakikisha maji yanayowafikia wananchi ni salama. Kwa takwimu kila watu 10 basi wanaopata maji ni sita, hii ina maana kwamba watu wanne hawapati maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, kwanza tutumie kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya binadamu na pia kwa kilimo; pili, tutumie maji ya maziwa na ikiwezekana ya bahari kwa kufanya *refinery* ili kuweza kutatua tatizo hilli la maji; tatu, kwa kufanya hivyo kila Halmashauri waweke *plan* ya kuhakikisha watu wake wanapata maji na nne, fedha na miundombinu zinatolewa na wafadhili zitumike vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZAINAB M. AMIRI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mungu kwa kunipa afya njema ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maji zipelekwe kwa wakati ili kuweza kutekeleza miradi hiyo kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iajiri watumishi wa kutosha katika Wizara hii ili kuweza kuwasaidia wananchi katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Pia naishauri Serikali iweke mita za maji zenye viwango ili kuepusha bili hewa za maji wanazoletewa wananchi ambazohaziendani na matumizi halisi yaliyofanywa. Naishauri Serikali kurekebisha miundombinu ili kuepusha upotevu wa maji, maana kuna baadhi ya maeneo yana uchakavu wa mabomba ambayo hupelekea mabomba kupasuka na maji kumwagika.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kutoa elimu kwa wananchi ili kipindi cha masika wananchi waweze kuvuna maji ya kutosha ili kuweza kuyatumia katika shughuli mbalimbali zikiwemo kilimo na matumizi mengine mengi wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwa maeneo ya miji ambayo matumizi ya maji ni mengi kutokana na wingi wa watu na hadi kupelekea mgao wa maji kwenye miji mfano Morogoro Mjini, Serikali itenye fedha za kutosha ili ichimbe visima virefu ambavyo vitasaidia kupata maji kila siku bila mgao.

Mheshimiwa Spika, mwisho naishauri Serikali kuweza kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kutunza vyanzo vya maji ili visiharibiwe.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, tafadhali kumbuka mabwawa sita ya Jimbo la Bunda Vijijini yanayochimbwa kwa lengo la kuwapa wakazi wa kata sita maji safi na salama.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, nampongezo Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa kazi nzuri anayofanya katika sekta ya maji.

Mheshimiwa Spika, tuliuunda *RUWASA* ili wafanye kazi kubwa ya kusambaza maji vijiji. Naomba wapewe fedha za kutosha ili itekeleze miradi ya maji mingi kwa sababu bado kuna uhitaji mkubwa sana wa maji nchini. Miradi mingi inatekelezwa kwa *force account* ambapo hata wanakijji wamepewa baadhi ya kazi wanazozifanya kwenye miradi inayotekelawa huko vijiji. Tatizo wasimamizi na wakandarasi hawa wakilipwa hawawalipi wanakijji ambao walifanya kazi za vibarua au walileta vitu kama maji, mawe, mchanga, tofari na kadhalika, mfano mzuri kuna mkandarasi alitekeleza mradi wa maji Kijiji cha Lukindo, Kata Katoma, Bukoba Vijiji. Alikwishalipwa hadi *certificate* ya mwisho lakini walio-supply vifaa na vibarua hawajalipwa. Naomba Wizara muwasaidie hawa Watanzania ambao wamedhurumiwa.

Mheshimiwa Spika, Bukoba Vijiji ni Halmashauri ambayo upatikanaji wa maji safi na salama ni mdogo sana. Kata nyingine ziko karibu kabisa na Ziwa Victoria lakini hazina maji safi na salama. Bukoba Mjini kuna mradi mkubwa wa maji. Kwa nini Serikali isiongeze bajeti kwenye mradi wa *BUWASA* wa usambazaji maji, wakasambaza maji pia kwenye kata zilizozunguka na ziko karibu na Ziwa Victoria kama Kata ya Nyakato, Katoma, Karabagaine, Kanyangereko, Maruku, Kemondo na Katerero. Wananchi wanaishia maji kuangalia tu kwa macho. Naomba utaratibu ufanywe nao wapate maji.

Mheshimiwa Spika, naomba katika kipindi hiki cha Corona gharama za bili za maji zipungue ili watu wengi zaidi waendelee kuosha mikono kujikinga na huu ugonjwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza viongozi na watendaji wa Wizara hi ikiongozwa na Profesa Mbarawa kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita katika maeneo manne na eneo la kwanza ni Mradi wa Maji Makonde. Mradi huu upo mionganoni mwa miradi ya maji kwa miji 28 ambayo itanufaika fedha za mkopo kutoka Serikali ya

India. Naomba kufahamu shughuli zitakazofanywa katika Halmashauri ya Mji Nanyamba kwa kuwa eneo hili ni miongoni mwa Halmashauri tano zinazonufaika na mradi wa huu wa Makonde.

Mheshimiwa Spika, pili ni *RUWASA*; hiki ni chombo kipya hivyo kiwezeshwe kwa rasimali watu, fedha na vitendea kazi na tatu kuna mradi wa kuchimba visima vidogo 12 kwa Jimbo la Nanyamba na tangu mwaka juzi lakini hadi leo havijachimbwa je, visima hivyo vinachimbwa lini?

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Spika, awali nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi. Pia nawapongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote na watumishi wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoendelea kufanya.

Mheshimiwa Spika, Naipongeza Wizara kwa utekelezaji wa miradi mingi ya maji nchi nzima hususan mradi wa maji wa Dar es salaam na Pwani kwa ufadhilli wa Benki ya Dunia umekuwa na manufaa makubwa kwa wananchi. Kwa Jimbo la Bagamoyo tunashukuru kujengewa tenki la ujazo wa lita milioni sita. Tenki hilo litaondosha uhaba wa maji katika Mji wa Bagamoyo. Naomba Serikali kupitia Wizara ya Maji ituharakishie mradi wa ulazaji wa mtandao wa mabomba ya usambazaji wa maji safi na salama katika Kata za Dunda, Magomeni, Kisutu na Nianjema katika Mji Mkongwe wa Bagamoyo. Ulazaji wa mtandao wa mabomba ya maji utawezesha Kata hizi kunufaika na uwepo wa tenki kubwa Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, pia mradi wa ulazaji mtandao wa mabomba ya maji uharakishwe kwa Kata zilizobaki za Jimbo la Bagamoyo ili nazo ziweze kujikwamua na tatizo la huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, Kata za Fukayosi na Makurunge zina huduma hafifu sana za maji safi. Awali huduma ya maji katika Kata hizo ilikuwa ikitolewa na *CHALIWASA*. Ila kwa miaka kadhaa huduma ya maji katika kata hizi ni sawa na

hakuna. Naiomba Wizara izipatie Kata hizi huduma ya maji toka katika Mto Ruvu. Ruvu ina maji mengi na Kata za Makurunge na Fukayosi zipo jirani na maeneo ya Bagamoyo yanayohudumiwa na *DAWASA* toka Ruvu Chini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Serikali yake ya awamu ya tano kwa kazi nzuri sana ya kuhakikisha miradi mingi ya maji kuanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, niendelee kumpongeza sana Waziri wa Maji, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri sana ya kuhakikisha llani ya Chama cha Mapinduzi inatekelezeka vizuri sana kwa kusimamia Wizara kwa weledi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita katika mambo yafuatayo; kwanza ni uanzishwaji wa *RUWASA*. Nitoe pongezi kubwa mno kwa kuhakikisha Wakala wa *RUWASA* inaanishwa ili kusaidia usimamizi wa miradi ya maji vijijini kama zilivyo wakala nyingine zinazotanya kazi vijijini. *RUWASA* kwa kipindi kifupi toka immeanzishwa imeonesha kufanya kazi vizuri sanalakini kumekuwepo na changamoto kubwa mno ukiwapo mosi. Ni uhaba wa wafanyakazi; pili, uhaba wa vitendo kazi kama magari, samani za ofisi na kadhalika na tatu fedha kwa ajili ya malipo ya makandarasi ili miradi iliyoanzishwa kwa mkakati.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa sasa sababu maeneo mingi sana ya vijijini yanauhaba wa maji, miradi hii ya maji ifanyiwe upembuzi yakinifu ili ile iliyoanzishwa iishe ndipo ianzishwe miradi mipya ili kunusuru kutekeleza miradi kwa bei nafuu na kwa wakati. Vilevile kwa kuwa tunavyanzo vingi sana vya maji katika maeneo yetu kama maziwa, mito na kadhalika, ni vyema sana maji yavutwe kutoka vyanzo hivyo kuliko kuchimba visima ambayo inaonesha kuwa

gharama zinakuwa kubwa zaidi na haina uhakika wa utafiti kama visima vinavyochimbwa kama vinatoa maji.

Mheshimiwa Spika, sheria nyingi za maji zimepitwa na wakati. Ni lini Serikali italeta muswada wa sheria Bungeni ili tuzihushe kwa kuwa sheria nyingi zimepitwa na wakati. Wakati tunapitia Sheria ya Uanzishwaji wa Wakala wa *RUWASA* tuliona sheria nyingi sana zinahitaji marekebisho. Niombe Serikali sasa ione umuhimu wa marekebisho ya sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ucheleweshaji wa pesa za miradi; kutokana na umhimu mkubwa wa maji nchini na sera ya Serikali yetu ya kumtua mwanamke ndoo kichwani ni vyema Wizara hii ikapatiwa pesa ya kutosha na kwa wakati ili miradi ya maji iweze kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Maji Mijini; nipongeze sana Serikali kwa uanzishwaji wa hizi mamlaka kwa ufanisi wa kazi zake na kufanya miji mingi kutokuwa na uhaba wa maji. Niombesana Serikali ijithahidi kufanya maboresho ya mifumo na uchakavu wa mabomba kutokana na kukua kwa haraka kwa miji yetu ili maeneo yote ya mijini yaweze kusambazwa kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ziara tulizozifanya na Kamati niwapongeze sana *DAWASCO*, *IRUWASA*, *DOWASA*, *MWAWASA* kwa kuitendea haki Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, mwisho niwapongeze tena Waziri Mheshimiwa Profesa Mbarawa Naibu Waziri Mheshimiwa Aweso, Katibu Mkuu Profesa Mkumbo, Naibu Katibu Mkuu Bwana Sanga na wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri katika Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Waziri, tatizo la maji bado ni kubwa kwenye Wilaya ya Kongwa. Tunahitaji mradi mpya wa maji mtiririko kuanzia Sagara kuja Kongwa Mjini.

Pili, mradi wa maji mtiririko kuanzia Nghumbi kwenda lyumbwi hadi Pembamoto na vitongoji vyake na hadi Chiwe hadi Vihingo Kijijini. Tatu, tunaomba mradi wa maji kwenye Mji Mdogo wa Mkoka.

Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi kubwa kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara, nashauri kwenye maeneo kadhaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza mradi wa vijiji 33; kumekuwa hakuna mawasiliano ya moja kwa moja kati ya Wizara na watendaji walioko ngazi za chini (Mikoa na Wilaya) hali hii imekuwa inaleta sintofahamu pale taarifa zinapotakiwa. Niombe pamoja na umuhimu wa mawasiliano, mradi huu wa vijiji 33 ukamillike kwa haraka ili wananchi wetu wa Visiwa vya Ukerewe wapate maji na kuwaepusha na maradhi yanayotokana na matumizi ya maji yasiyo safi na salama hasa kutopteka na kuzungukwa na ziwa.

Mheshimiwa Spika, pili ni miradi ya *P4R*; kwa kuwa miradi hii inaelekea kukamilika kwenye Wilaya yetu ya Ukerewe, *RUWASA* Makao Makuu ambao ndio wenyewe jukumu la kusambaza vifaa kama *pump* na kadhalika basi mapema kadri iwezekanavyo vifaa hivyo viweze kuleta ili miradi hiyo iweze kutoa huduma kwa wananchi.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja hii ya Wizara ya Maji. Napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri ambayo imetukumbuka na sisi Wananyangh'wale kutengewa pesa za kuendeleza Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria, kutoka Nyamtuku/Bukwimba. Ombi langu, wakandarasi wapewe fedha kwa wakati ili kazi iende kwa kasi ili wananchi wapate maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, ombi langu lingine ni kuwa, wakandarasi wafuatiliwe kwa karibu sana kwa utendaji kazi

zao. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa uchapaji kazi usiku na mchana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa mchango wangu kwa maandishi kwenye hoja ya bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Rais wangu Dkt. John Joseph Pombe Magufuli na Serikali yake ya Awamu ya Tano kwa uongozi imara na azma kabambe ya kumtua mama ndoo kichwani. Pia nitumie fursa hii kumpongeza Waziri wa Maji, Profesa Mbarawa na Naibu wake, Mheshimiwa Aweso pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayofanya kutekeleza miradi mikubwa na midogo; mijini na vijiji ili kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anapata *access* ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, nitumie pia fursa hii kuishukuru Serikali kwa miradi yote, mikubwa na midogo ya maji iliyotekeliza katika Jimbo langu la Longido katika miaka hii mitano ya Serikali ya Awamu ya Tano. Aidha, nashukuru kwa mradi mkubwa wa maji ya Mto Simba ambao umemaliza kero kubwa ya ukosefu wa maji Mjini Longido na baadhi ya vijiji kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi na shukrani hizo sasa naomba kujielekeza kwenye hoja iliyoko mezani kwa kuchangia kwenye masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, katika hotuba ya Waziri sijaona mahali wanapobainisha kuhusu mwendelezo wa Mradi wa Maji ya Mto Simba kutoka Longido kwenda vijiji jirani hadi Namanga ambapo Mheshimiwa Rais aliwaahidi wananchi kufikiwa na maji safi na salama toka Mlima Kilimanjaro. Pia Mradi huu wa Mto Simba bado usambazaji wake wa maji haujakamilika katika Kata ya Engikaret kwenye Kijiji cha Engikaret chenyewe na Kiserian ambapo hakuna chanzo kingine chochote cha maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa kulikuwa na ahadi ya Serikali ya kuhakikisha kuwa vijiji vinavyopitiwa na bomba la maji ya Mto Simba wanapewa matawi ya maji hayo, naomba niikumbushe Wizara wasisahau kutimiza ahadi hizo kwa Vijihi vya Elerai (Kitongoji cha Imotoon), Vijiji vya Tingatinga, Ngereyani na Sinya.

Mheshimiwa Spika, pia nitumie fursa hii kuiomba Wizara kuelekeza sehemu ya fedha walizotenga kwa ajili ya mabwawa Mkoani Arusha kwenye ukarabati wa mabwawa ya Kimokouwa na Tinga Lesingita pamoja na kuchimba mabwawa mawili yaliyoahidiwa na Serikali tangu mwaka 2016 kwenye Vijihi vya Wosiwosi na Tingatinga/Ngereyani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kufika kwa maji ya Mto Simba, Wilayani Longido kumetatua tatizo la maji kwenye tarafa moja tu katika tarafa nne kubwa na kame za Wilaya ya Longido, naomba Serikali izidi kuwekeza fedha za maji kwenye miradi ya uchimbaji wa visima virefu katika vijiji ambavyo bado hakuna chanzo chochote cha maji safi. Katika ya Vijihi vilivyo katika hali mbaya kwa sasa Wilayani Longido ni pamoja na Wosiwosi, Kiserian, Ngereyani, Karao na Matale B na C.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kuishauri Serikali kuwa, izingatie suala la matengenezo (*maintenance*) ya mashine za maji tulizonazo kwenye visima mbalimbali. Nasema hivi kwa sababu sisi katika Wilaya ya Longido tuna visima kadhaa vilivyo chimbwa na Serikali miaka ya nyuma na kufungwa mashine kubwa na za pesa nyingi kisha kuachiwa wananchi wasio na ujuzi kubeba jukumu la kuvisimamia na kuvienda desha. Matokeo yake mashine zinaharibika kutohana na *poor maintenance* na wananchi kurudiwa na adha ya ukosefu wa maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa visima virefu vilivyokumbwa na changamoto hii ni pamoja na visima vya Vijihi vya Sinonik, Ngosuak, Mundarara na Lesingita. Hivi visima hivyo vinahitaji mashine mpya za kusukuma maji na naomba Serikali wanunue jenereta mpya kwa ajili ya visima hivyo na

waajiri waendeshaji wenye ujuzi kuzisimamia. Katika hili wananchi wako tayari kuchangia kwa kulipia huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, ahsante sana na naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa pongezi nyngi kwa Mheshimiwa Waziri. Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na viongozi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nitoe shukrani kwa Serikali kwa kututengea zaidi ya shilingi bilioni 80 kwa ajili ya kukarabati mradi wa maji mkubwa utakaohudumia vijiji 62 kwa sehemu kubwa Tarafa ya Wanging'ombe. Nataka kujua ni lini wakandarasi wataanza?

Mheshimiwa Spika, pia tuna mradi wa kutoa maji Malangali mpaka Kijombe wa zaidi ya shilingi bilioni 12 ambaa umeanza Julai, 2018 lakini unatekelezwa íwa kasi isiyoridhisha wananchi wetu. Nataka kujua ni m<sup>k</sup>akatiki gani upo na Wizara hii ili mradi huu uwemo kukamilika?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nawatakia mafanikio ya utekelezaji.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mungu kwa kunipa uzima na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na pia kuniwezesha kutoa mchango wangu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Waziri na Naibu wake pamoja na wataalam walio chini yao kwa kazi nzuri waifanyao ya kuhakikisha maeneo mengi wanapata maji ingawa hali bado haijawa vema kwa lengo tulitakalo.

Mheshimiwa Spika, jitihada ya kusambaza maji vijijini, bado vijiji vyta za pembezoni ya Manispaa hazikidhi

mahitaji, akinamama wanahangaika kupata maji safi na salama (Senga, Ntendo, Milanzi, Mollo, Matanga, Kasense na Pito), Kata zilizo pembezoni mwa Ziwa Tanganyika na Ziwa Rukwa hawapati maji safi na salama na katika maeneo hayo kuna wagonjwa ya mlipuko mara kwa mara kutokana na mazingira yao.

Mheshimiwa Spika, tunaona bajeti yao inawajali sana wananchi, lakini haikidhi mahitaji, hivyo wapewe bajeti yote, kama itakavypitishwa na Bunge. Pia tuna upungufu wa Wataalam ambao ni Wahandisi wa Maji, ni wachache kwenye Mkoa. Ushauri kwa Serikali kwamba wataalam wagawanyike vijijiini na mijini kwa gawio lililo rafiki kwa kuzingatiwa mahitaji na mazingira. Nina imani watajiongeza katika ubunifu wa ushindani wa upatikanaji maji ndani ya maeneo yao, hivyo wakikosa chini ya ardhi, watavuna ya mvua.

Mheshimiwa Spika, tunamwomba Waziri aweze kuingilia kati hizi Mamlaka za Maji kuhusu gharama za maji kwa watumiaji ni kubwa ukilinganisha na kipato chao (Mkoa wa Rukwa). Kama ilivyowezekana kutoa muda wa malipo ya gharama ya kuunganisha maji kwenye majumba yetu, huko Dar es Salam, ndani ya miezi sita, hakika ni utaratibu mzuri nan i vema ukawa kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa ustawi wa jamii yetu hususani katika kipindi hiki cha maambukizi ya ugonjwa wa *corona*, Serikali ione umuhimu wa kutatua changamoto za maji mjini na vijijiini.

Mheshimiwa Spika, naomba Mradi wa Maji, Kata ya Mamba, Jimbo la Kavuu, Mkoa wa Katavi ambao mpaka sasa hauna kuelekea watu wameiba pesa zaidi 50km milioni ambazo mpaka sasa hazieleweki ziko wapi. Ni kwa nini mradi huu uko kimya na Serikali imeshindwa kumchukulia hatua Mkandarasi huyu. Manispa ya Mpanda Kata ya Kasokola, Makes, Mwamkulu, Magamba, Kazima, Shane, Mishamo,

Katumba, Inyonga, ni maeneo ambayo mtandao wa maji safi na salama haupo. Mkandarasi wa Mpanda Manispaa bado iko haja ya Serikali kuuangalia mradi huu una wizi ndani yake na kwa nini umesimama? Serikali imeonesha uzembe kwa sababu inatumia muda mrefu kutatua changamoto hizi za maji.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichangie kuhusu Mfuko wa Maji; kama kuna changamoto inayotuzuia kuongeza tozo kwenye petroli/dizeli kufikia sh.100/- kwa lita na Serikali inasema itakuja na chanzo cha kuaminika kuongeza kwenye Mfuko wa Maji ili kuondoa kero ya maji nchini. Nilitarajia hotuba hii ingetuletea mpango mkakati huo ili tuweze kuujadili ipasavyo. Binafsi pamoja na Wabunge wengine wengi tumekuwa tukitoa wazo hili kwa zaidi ya miaka mitatu sasa bila mafanikio. Serikali itueleze nini hasa kinatukwamisha kuongeza kadiri tunavyopendekeza na kama ndivyo tusubiri miaka mingapi mingine kupata mbadala wake ili wananchi tunaowawakilisha waweze kuondokana na kero hii kubwa sana ya maji?

Mheshimiwa Spika, Uvunaji wa Maji; tuanze kuona kwanza mfano kwenye miradi/majengo ya Serikali na taasisi zake zote inayotekelawa sasa. Miradi iwe na *provisions* za kuvuna maji (*Gutters, undergound infrastructure* ya kuhifadhi na kutawanya maji inavyostahili). *We must lead by examples* na kwa kuwa hii ndio Wizara mama ya Sekta ya Maji, tunakwama wapi kuleta mapendekezo ya sheria hapa Bungeni ili kila ujenzi nchini uzingatie takwa hilo na hatimaye kusaidia kuondoa kero ya maji nchini?

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wote wa Taifa letu kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kadri alivyolinda na kuijalia baraka, ulinzi na mafanikio nchi yetu katika muda wa miaka mitano hii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wetu mpendwa na Serikali yetu nzima kwa kutuongoza vizuri sana hadi sasa. Hata hivyo,

nchi yetu imepata mafanikio makubwa sana ktk nyanja mbalimbali za kijamii, kiuchumi, kisiasa na kidplomasia. Jambo linalotupa heshima kubwa sana kimataifa, hakika kitabu cha nyakati hii kimeweka historia kwa Taifa letu, hususan Jimbo langu la Mbulu Mji.

Mheshimiwa Spika, naungana na viongozi wenzangu wote kuwapa pole nydingi sana Watanzania wote walipoteza wapendwa wao kwa namna mbalimbali, waliotangulia mbele ya haki. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu awapokea katika ufalme wake usio na mwisho,Amina.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe mchango wangu wa kuishauri Serikali kupitia hotuba ya bajeti kwa Wizara hii:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Serikali ifanye mapitio ya upangaji wa bajeti ya miradi ya maji ili kuweka uwiano sawia kwa huduma za maji kwenye majiji, manispaa, mji na wilaya kwa nchi nzima ili kuondoa manunguniko ya Waheshimiwa Wabunge kama wawakilishi.

Pili, Serikali kupitia Wakala wa Maji Mijini na Vijiini iangalie mpango wa kuzijengea uwezo Kamati za Maji ili ziweze kusimamia mapato ya ada za maji na kuendeleza mtandao wa maji kuwafikia wananchi wa pembezoni.

Mheshimiwa Spika, tatu, Serikali itoe bei elekezi ya malipo ya maji kwa mita nchi nzima kupitia hotuba yake ya leo na waraka wa wazi. Mfano huo ni Mbulu Mji kuna wanaolipa shilingi 2,500/= kwa *unit* moja wakati huo huo katika Halmashauri hiyo kuna wanaolipa shilingi 540/=, shilingi 1,000/=, shilingi 1,400/= na shilingi 2,500=/. Mheshimiwa Waziri alifika Mbulu mwaka jana, akatoa tamko la Serikali kuwa kiwango hicho ni kikubwa sana, hivyo hadi sasa Meneja wa Wilaya wameshindwa kutekeleza agizo hilo.

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali iangalie uwiano wa Wahandisi wa Wakala wa Maji (*RUWASA*) walipo kwa kuwa kuna upungufu mkubwa sana wa wataalam.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana wafuatao; Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Waziri wa Maji na Mheshimiwa Juma Aweso, Naibu Waziri wa Maji. Pia nimpongeze Katibu Mkuu, Profesa Mkumbo na Naibu Katibu Mkuu *Engineer* Sanga kwa kazi kubwa wanayofanya ili kuwaletea Watanzania huduma ya maji, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa Serikali ya Awamu ya Tano kutuletea maji katika Vijiji vya Ukalawa, Kitole, Kidegembye na usambazaji wa maji umeshaanza katika Vijiji vya Matembwe na Lupembe. Pamoja vijiji hivi kupata maji lakini bado kuna vijiji vingi havina maji navyo ni Kanikelele, Nyombo, Ninga, Matiganjora, Havanga, Isoliwaya, Ikang'asi, Lyalalo, Isitu, Lole, Ilengititu, Kichiwa, Tagamenda, Upami, Kichiwa na Iyembela. Tunaomba fedha kwa ajili ya kusambaza maji katika vijiji hivi nilivyovitaja.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa la wakandarasi kuchelewesha ukamilishaji wa miradi ya maji, lakini pia miradi mingi ina gharama kubwa sana. Nashauri Wizara sasa ianze kutumia wataalam wetu kwa kutumia *force* akaunti. Hii itasaidia kupunguza gharama za miradi ya maji na tutaokoa fedha nydingi sana ambazo zitaenda kutekeleza miradi mingine pia wataalam wetu wataweza kutekeleza miradi kwa muda muafaka kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu nana, lakini Miradi ya Maendeleo imekuwa haipati pesa za kutosha. Fedha zinaidhinishwa na Bunge lakini zinapelekwa kidogo au hazipelekwi kabisa. Naomba kuishauri Serikali ipeleke fedha yote inayoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Njombe umekuwa na tatizo la maji katika maeneo mengi kama vile Njombe Mjini, Wilaya ya Wangingombe, Wilaya ya Ludewa na katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. Naishauri Serikali ipeleke njia mbadala ya kupata maji.

Mheshimiwa Spika, *bills* za maji bado ni kubwa katika Mkoa wa Njombe. Naomba Wizara ifuatilie kwa nini *bill* zinakuwa kubwa. Naomba kuwasilisha.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua fursa hii kuipongeza Serikali pamoja na Rais wetu kwa juhudhi kubwa sana kwa jithada kubwa sana inayofanya ili kuhakikisha wananchi wote wanapata maji safi na salama. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa jithada kubwa sana ya kusimamia Wizara hii ili miradi ya maji ikamilike na wananchi wapate maji.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu, kwanza, nashauri Serikali itenye fedha za kutosha ili kuwekeza katika miradi ya maji ili kukabiliana na upungufu wa maji nchini. Pia fedha kwa ajili ya miradi ya maji zitolewe kwa wakati muafaka ili kuepusha kuongezeka kwa garama za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, pili, nashauri Serikali wizara ipewe kibali cha kuajiri wataalam wa maji ili kupunguza tatizo la upungufu wa wataalam.

Mheshimiwa Spika, tatu, *RUWASA* ijengewe uwezo zaidi ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nne, matumizi ya *prepaid meter* yasambazwe nchini kote ili kuondosha changamoto za malipo ya ankara za maji.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja hii.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa utendaji, wanafanya kazi nzuri sana,

wamezunguka nchi nzima, wanajua miradi, kitu ambacho ni kizuri sana. Pili, wako *sharp* wote, hata usiku wa manane wanajibu meseji, mara kadhaa imekuwa hivyo kwangu. Pia nashukuru sana Mafinga licha ya kuwa ni Halmashauri mpya tumepiga hatua kuwa kiwango kikubwa pamoja na kuwa bado uhitaji ni mkubwa sana. Katika kipindi hiki miradi yote tuliyopewa tumeifanya kwa ufanisi na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, miradi ya ujenzi wa matanki Kijiji cha Maduma tanki la lita elfu 90 na pia Bumilayinga tanki la ujazo wa lita laki moja. Pia mjini tanki la lita laki tano Kinyanambo na sasa tunakamilisha ujenzi wa tanki la lita milioni moja. Hata hivyo Mji wa Mafinga unakua kwa kasi na una viwanda vingi kutokana na mazao ya misitu. Tuna viwanda ambavyo vinazalisha *for export* hivyo kupata mradi ule wa fedha za mkopo wa India itasaidia sana katika suala zima la uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, napendekeza maeneo ambako Serikali inatoa fedha na tunasimamia kwa ufasaha tutazamwe kwa macho mawili. Kuna maeneo miradi inapewa fedha hakuna kitu, kwa nini tunaosimamia kwa umakini tusipewe kipaumbele zaidi.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri; Miradi ya wadau: Naomba wachunguze baadhi ya miradi, utaona umetumia fedha nyingi lakini wanufaika ni wachache. Natoa mfano, *Water for Africa* wametumia milioni 42, wanufaika ni 12,000; *Acacia* wametumia bilioni 4.4, wanufaika ni 63,815; *Life water* bilioni 4.2, wanufaika 7,650, hii ni page 267. Yawezekana kuna masuala ya kiufundi lakini nashawishika kuamini kuwa kuna ujanja wa kimahesabu, nashauri Wizara iangalie miradi hii isije ikaonekana wadau wametusaidia mabilioni kwa maandishi lakini tija yake ikawa ndogo.

Mheshimiwa Spika, *Force Account*; Miradi ya maji ni very *technical*, nashauri baadhi ya maeneo ambako Halmashauri zina *capacity* ya kitaalam ifanyike kwa *force account*, lakini ambako uwezo kitaalam ni mdogo ifanywe na wakandarasi lakini kwa *condition* kuwa wafanye kwa

gharama zilezile ambazo zingefanywa kwa *force account*. Jamani miradi ya maji sio sawa na majengo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, *CBWSO* ukienda kwenye kiambatanisho Na.5 utaona zilipaswa kuwa 6951 lakini zipo 3236 sawa na 46.5%, tatizo nini? *CBWSO* ni mkombozi sana kwa sababu zinaipunguzia Serikali gharama kama vile za usimamizi na ukarabati. Nashauri tutumie kila nyenzo na mbinu ili tuwe nazo kadri ya malengo, ziwe nyngi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri tumekupa robo saa ili ile nusu saa ya Mheshimiwa Waziri ibaki vile vile kwa vile mambo ni mengi ya kuelezea, kwa hiyo jaribu kuitumia robo saa Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema, lakini na kuweza kufanya kazi kwa miaka mitano. Wewe, Naibu Spika na timu yako pamoja na Waheshimiwa Wabunge tunakushukuru sana, Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Spika, nakukubali sana pamoja na timu yako, umetupa ushirikiano mkubwa sana, mimi hiki ni kipindi change cha kwanza katika Bunge hili. Nilikuwa mwanafunzi, lakini nilikuwa mfuatiliaji sana wa Bunge. Mabunge yapo mengi sana, lakini Bunge hili ni la mapinduzi, Mwenyenzi Mungu akubariki sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, najua wapo watakaokubeza lakini nimesimama hapa kukutia moyo. Ukitoma maandiko ya dini yanasema adui akinividhi nami nikisumbuka Mungu huvigeuza vyote kuwa baraka. (*Makofii*)

**MBUNGE FULANI:** Amina.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, umetutendea haki utakumbukwa katika historia kwa kazi

kubwa uliyofanya katika Bunge hili. Tumepitisha miradi mingi na mikubwa ya maendeleo haukuwa kikwazo katika Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza na kumshukuru kwa dhati kabisa Rais wangu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuniamini. Watu zamani walikuwa wakipewa vyeo kwa majina, lakini mimi leo mama ntilie ni Naibu Waziri, si jambo jepesi. Ninachotaka kusema na kuweka *commitment* kwa viongozi wangu wakuu mimi Jumaa Aweso, Naibu Waziri wa Maji sitakuwa kikwazo kwa Watanzania na Waheshimiwa Wabunge kupata maji safi na salama na ya yenye kutosheleza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nimshukuru sana Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu kiukweli amekuwa na sisi, ametupa ushirikiano mkubwa sana, maelekezo yake, ushauri wake umeweza kutusaidia na kufanya kazi kubwa leo Waheshimiwa Wabunge, yapo maeneo ambayo tumeyapatia na yapo ambayo tumeyakosea, lakini wameweza kutushauri, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna kipekee niishukuru sana Kamati yetu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, imefanya kazi kubwa sana mpaka sisi leo tumefika hapa chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Mgimwa tunawashukuru sana, tunawashukuru sana na Mwenyenzi Mungu awabariki sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, nimshukuru Waziri wangu, baba huyu, huyu baba anafanya kazi kubwa sana ndugu zangu. Ni mionganoni mwa Waziri makini sana; Katibu Mkuu, Profesa ni mionganoni mwa watendaji wanaofanya kazi kubwa pamoja na Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi. Mheshimiwa Waziri wangu Profesa Makame Mbarawa pamoja na Uwaziri wake lakini yeye ni baba mlezi, aumenilea vizuri, nimtie moyo, kazi aliyoifanya

itakuja kukumbukwa na ukisoma maandiko ya dini ya biblia, Ezra anasema: "*Inuka hii shughuli ukaitende kwa moyo mkuu na sisi tupo pamoja naye.*"

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wetu wa Maji hajalala hata siku moja na Waheshimiwa Wabunge kama tutakuwa wa kweli, leo hii ni jimbo gani sisi kama Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu hajafika? Tumefika yote, tumefika kwa sababu tulitambua kabisa anayelala na mgonjwa ndiyo anayejua mihemo ya mgonjwa, tulitambua kabisa maji hayawezi kupatikana vijiji, miji kwa kukaa ofisi na kuchezea *computer*.

Mheshimiwa Spika, tulitoka, tulifuatilia miradi na tukaweza kufanya kazi kubwa ili kuisaidia Taifa letu. Kwa namna ya kipekee Waheshimiwa Wabunge nirudie tena, ushauri wenu, mawazo yenu, tumeyapokea na tutaya fanya la kazi sana. Asiyeshukuru kidogo hata kikubwa hawesi kushukuru, tunawashukuru sana kwa ushauri wenu tutaendelea kufanya kazi ila tunaomba ushirikiano wenu, tunaomba mtutie nguvu, tunatambua kabisa unaweza ukawa baba, una mtoto shulen i wakati mwingine alikuwa akifanya vibaya, kama mzazi lazima ujisikie vibaya, lakini mtoto huyo huyo ukimwona sasa anaendelea vizuri mtie moyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunatambua maendeleo ya sekta ya maji kwa maana ya kuwapatia wananchi maji tulikuwa tunatekeleza kuitia Program ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, awamu ya kwanza na sasa hivi awamu ya pili. Nikiri dharti ya moyo wangu Miradi ya Viji 10, Miradi ya *World Bank* ilikuwa miradi ya kichefu chefu. Tulifanya ziara nchi nzima, nilifika na nilikaa na Mheshimiwa Waziri tukasema haiwezekani leo fedha au Wakandarasi wapewe kazi kishemeji shemeji, kiujombaujomba haiwezekani! Tulikuwa tunaona miradi inajengwa lakini chanzo hakuna. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tulienda zetu pale Mwakitolio pale mradi wa 1.4 bilioni, mkandarasi amelipwa fedha, unauliza mbona maji hakuna, anakwambia Mheshimiwa Waziri

naomba nikujibu, unamwambia jibu kwa wananchi, anasema naomba nikunong'oneze, nikamwambia haiwezekani, waeleze wananchi, Serikali imeleta fedha, kwa nini hawapati maji? Miradi hii ya Vijiji 10.

Mheshimiwa Spika, yule mkandarasi anasema Mheshimiwa Waziri sijawahi kuona kijiji wachawi kama kijiji hiki, mabomba usiku yanapaa kama ndege. Sisi kama viongozi wa Wizara hatuwezi kuwavumilia Wakandarasi na Wahandisi wa namna ile, tumeweza kuwachukulia hatua. Tulikuwa tukilia na kulalamika, sisi kama Wizara ya Maji, imani yangu inaniambia kwamba ukiona tatizo katika jamii, unatakiwa ufanye mambo matatu; moja liondoe kwa mkono wako; pili, likemee; na tatu, lichukie. Sisi tumeyafanya hayo mambo yote matatu.

Mheshimiwa Spika, tulifika katika Bunge lako Tukufu tulikuwa tukilalamika sisi kama Wizara, kuhusu muundo wa Wizara katika utekelezaji wa miradi. Haiwezekani sisi tutekeleze miradi ya maji, leo Wahandisi wapo eneo lingine, Wizara ipo kwenye eneo lingine, haiwezekani! Ndiyo maana Bunge lako limekuwa sikivu na la kimapinduzi, tukapitisha Sheria Na.5, ikatupa nafasi ya kuanzisha *RUWASA*. Hili ni jambo kubwa sana kwetu sisi, tunakushukuru sana na Mwenyezi Mungu akubariki sana. Sisi hii kazi tunaiweza na wala hajatushinda, tutaifanya kazi kwa udailifu mkubwa. Niombe sana Waheshimiwa Wabunge tusiingie kwenye mtego.

Mheshimiwa Spika, jana Mheshimiwa Heche hapa alizungumza kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano imewatenga watu wa Mara, dada yangu naye hapa Esther Bulaya amezungumza jana na leo dada yangu Esther Matiko naye amezungumza. Nataka niseme hatujatenga, Serikali ya Awamu hii ya Tano imefanya kazi kubwa, sana. Ukienda pale Musoma wanaosema kwamba tumeutenga Mkoa wa Mara, tumeteleza mradi wa bilioni 45 ili wananchi wa Musoma waweze kupata maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, leo dada yangu Esther Matiko, mimi nilifika katika Jimbo lake wala hakuwepo, mradi ulikuwa

ukisuasua wa Gamasala, tulichukua hatua, mradi umekamilika, sasa hivi tunakwenda kwenye *pressure test*, hivi tufanye nini? Mwenyezi Mungu awape nini au awape donda mfukuze nzi? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa dada yangu Ester Bulaya, tulikuwa na mradi wa miaka zaidi ya 11, hata mimi sikusoma. Mradi ule leo umekamilika, watu wanapata maji, sasa hivi tunatengeneza chujio. Nataka niseme: *Man la yashkuru nnasi la yashkuru Allah* (asiyeshukuru watu hata Mwenyezi Mungu hawezি kumshukuru). (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kubeza kazi kubwa iliyofanywa na Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli. Hatuwezi kubeza kazi kubwa iliyofanywa na Viongozi wetu. Rais kama Dkt. John Pombe Magufuli hapatikani kila mahali, hapatikani kila wakati, tumempata lazima tumtumie. Nataka niwaambie kwa takwimu kwa *Progammme* ya Maendeleo ya Sekta ya Maji tumeweza kutekeleza miradi 2,450 kwa maana ya awamu ya kwanza na awamu ya pili. Rais Dkt. John Pombe Magufuli peke yake ameweza kutekeleza miradi 1,423, mnataka afanye nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tuna miradi 652 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kwa kuanzishwa tu kwa RUWASA tumeaminiwa na Mashirika mbalimbali ya Maendeleo, tumepata billioni 119 kwa ajili ya Halmashauri 86 ikiwemo katika Mkoa huo wa Mara katika zaidi ya Halmashauri 86 kwenda kutekeleza hii miradi ya maji.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema na nataka niwaambie Wataalam pamoja na Wakandarasi, vipo vya kuchezea, ukishiba chezea kitambi au kidevu chako, si miradi ya maji, tutakushughulikia ipasavyo. (*Vigelegele/Makof*)

Mheshimiwa Spika, sisi kama Viongozi wa Wizara, tutaendelea kufanya kazi na kusimamia llani ya Chama cha Mapinduzi. Nataka nikutie moyo Mheshimiwa Spika *seeing is believing*; kuona ni kuamini. Leo nenda Arusha zaidi ya mradi wa billioni 520 tunautekeliza; nenda Tabora, zaidi ya bilioni

600 mradi umekamilika na wananchi wameanza kuyatumia maji; nenda Longido, mradi wa bilioni 16 umekamilika unatakiwa kufunguliwa; nenda Igunga, mradi wa bilioni 24, Iganga – Kasaka leo watu wanapata huduma ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimtie moyo Waziri wangu, baba huyu anafanya kazi kubwa sana. Nimtie moyo Katibu Mkuu na Wakurugenzi, tumefukuza Wahandisi wa Maji 98 katika Wizara yetu ya Maji. Tulikuwa na Wahandisi wababaishaji leo wanafanya hivi, kesho hivi, mpaka ikafikia hatua tukawaambia hivi nyie mngekuwa ni Madaktari si mngeua watu wengi, lakini Serikali ya Awamu ya Tano ipo kwa ajili ya kusimamia na Mheshimiwa Rais ametuamini. Hiyo kazi tunaiweza tutaifanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninachotaka kukisema ni kwamba, Taifa letu lipo katika mapambano ama vita ya ugonjwa huu wa *corona*. Sisi kama Wizara ya Maji tunatambua ili kuweza kukabiliana na tatizo hili lazima kuwe na matumizi makubwa sana ya maji. Tumetoa maelekezo kwa Wakurugenzi wetu wa Mamlaka za Maji; moja kuhakikisha wanatengeneza vizimba ili wananchi waendelee kunawa katika maeneo yao. Pili, tunajua kabisa kipindi hiki matumizi yatakuwa ni makubwa sana. Ni marufuku kwa Wakurugenzi wa Mamlaka za Maji kuwabambikizia wananchi bili za maji. Vile vile operesheni zile zisizokuwa na kichwa wala miguu za kukatia watu maji zikome. Tumelisimamia hilo katika kuhakikisha Watanzania wanaendelea kupambana na matatizo haya. Kupitia mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan hili gonjwa litapeperushiwa mbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, tunatambua kabisa jukumu la kuwapatia maji ni jukumu letu Wizara ya Maji, lakini mwananchi naye ana wajibu wa kulipia bili za maji. Pamoja na kulipia bili hizo za maji zisiwe bambikizi, Serikali hii ya Awamu ya Tano imeweka utaratibu mzuri sana wa kuhakikisha wananchi hawa wanapata maji kwa gharama nafuu. Kwa lugha nyepesi kabisa, maeneo mengi *unit* ya maji ni 1,800/=

au gharama kubwa ni 2,000/=. Unaposema *unit* moja ya maji maana yake ni lita 1,000 na unaposema lita 1,000 maana yake ni ndoo 50, kwa hiyo hebu tuchukulie mathalani kwa *unit* moja 2,000/=. Maana yake mwananchi huyu anatakiwa kwa ndoo 20 anatakiwa awe na ndoo 50 na kila ndoo 50/=.

Mheshimiwa Spika, hivi kwa mwananchi wa kawaida anaweza kumaliza ndoo 50 kwa siku? Ina maana haiwezekani. Moja yawezekana kuna matumizi yasiyo sahihi ya maji, leo mtu anapiga mswaki lakini amelifungulia bomba zaidi ya dakika tano. Achana na hilo yawezekana pia kuna ubambikiazi mkubwa wa bili za maji na ndio maana tulwaita Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Maji na tukawaagiza asiyeweza kazi aondoke. Serikali hii imeweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha mwananchi anapata maji, si maji tu, ni kwa maana ya maji kwa njia rahisi na kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge, hii kazi tunaiweza na niwaagize *EWURA*, jukumu lao ni kudhibiti bei za maji na Mamlaka za Maji. Wakishindwa kusimamia hizi Mamlaka za Maji, basi sisi tutachukua hatua ya kuwachukulia na kuwashughulia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso. Tunashukuru sana kwa *compliments* zako na kuwajibu Waheshimiwa Wabunge hoja zao mbalimbali. *Insha Allah* Mwenyezi Mungu atakurudisha, naona hata Mheshimiwa Ester Bulaya amekubali, maana kwenye mchango wake jana hakugusa tena ule Mradi wa Bunda, jana ameongelea mengine tu. Ule mradi wa siku zote umeshashughulikia tayari. (*Kicheko*)

Sasa naomba nimwite Mtoa Hoja, Mheshimiwa Waziri Profesa Makame Mbarawa, karibu sana. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi

Mungu, mwangi wa rehema kwa kutujalia kupata fursa hii ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa uwezo na umahiri mkubwa unaoonyesha katika kuliendesha Bunge letu Tukufu. Nichukue nafasi hii kukupongeza wewe kwa dhati na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kuizungumzia hii hoja iliyoko mbele yetu. Wabunge waliochangia hoja yetu ni 27; kati ya hao Wabunge 19 wamechangia kwa kuzungumza na Wabunge nane kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, michango ya Waheshimiwa Wabunge ni mizuri na ni muhimu sana. Hata hivyo, sitaweza kuyapitia hapa kwa pamoja kwa sababu muda wenyewe ni mfupi lakini nitaendelea kujibu kwa pamoja ili kuona maeneo gani nitayazungumza.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii tena kumshukuru sana Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais wakati aliponiteua kuja Wizara ya Maji niliona kama ni Wizara ambayo ina changamoto kubwa lakini leo nasimama baada ya kumaliza miaka miwili nimejifunza vitu vingi na nimeweza kutenda vitu vingi kuwasaidia Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameendelea kunifunza kila siku na mara yangu ya mwisho Mheshimiwa Rais alinifunza pale nilipokuwa Njombe. Mtakumbuka siku nilipokuwa Njombe Mheshimiwa Rais aliniambia kwamba niende nikavute bangi ya Njombe. Mimi ni mtu ambaye sijawahi kuvuta bangi lakini maneno yale yaliingia sana akilini nikajua kuna tatizo la muhimu kwenye Wizara ya Maji linatakiwa litatuliwe. Kuanzia siku ile nilianza kujuliza maswali kuanzia Njombe mpaka kufika Iringa, kwa nini Mheshimiwa Rais aliniambia maneno haya.

Mheshimiwa Spika, palikuwa na mradi wa maji pale wa karibu shilingi bilioni 300 na haufanyi kazi. Nikapiga simu kwenye viwanda vyta mabomba na kwa wataalam wangu

nikaona kuna udanganyifu mkubwa kwenye miradi ya maji. Kuanzia pale ndiyo nikaanza kujifunza kuendesha Wizara ya Maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijaenda kuzungumzua Wizara ya Maji, naomba kipekee sana nimshukuru sana Mheshimiwa Kitwanga. Mheshimiwa Kitwanga kwangu ni mtu *special* katika maisha yangu. Wakati nimeanza kufanya kazi Wizara ya Mawasiliano kwa mara ya mwanzo kuchaguliwa Mbunge na kuwa Waziri yule ndiyo alikuwa mwalimu wangu.

Mheshimiwa Spika, alikuwa mwalimu mzuri yeye akiwa Naibu Waziri mimi nikiwa Waziri siku hizo ndiyo *fresh* natoka *South Africa* Mheshimiwa Kitwanga ndiyo alikuwa ananionesha njia, ananiongoza na nakushukuru sana Mheshimiwa Kitwanga kwa kazi nzuri sana uliyofanya. Siku zote na maisha yangu yote nitaendelea kumheshimu Kitwanga na hata nitakapoandika kitabu changu Mheshimiwa Kitwanga atachukua nafasi muhimu katika maisha yangu. Mheshimiwa Kitwanga nakushukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji ilikuwa na changamoto kubwa sana. Kama nilivyosema mwaka jana ndiyo tulianza kujua nini tatizo la Wizara ya Maji. Tatizo kubwa la Wizara ya Maji ambalo kwa muda mrefu lilikuwepo na hakuna mtu ambaye alikuwa anazungumza waziwazi tatizo ni nini, kulikuwa na udanganyifu mkubwa kati ya wakandarasi na wafanyakazi wenyewe wa Wizara ya Maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tatizo lile lilianzia kutoka Halmashauri likaenda Mkoani likaja Wizara ya Maji, *entire system* ya Wizara ya Maji ilikuwa na shida. Hata kama tungeipa bilioni au trilioni 10 kwa *system* ile tusingewenza kutatua tatizo la maji. Leo Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema na wengi wameshukuru kwa kazi kubwa tulioifanya kuanzia mwezi Julai mwaka jana mpaka mwezi Machi mwaka huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Wizara ya Maji kulikuwa na changamoto nyingi. Changamoto ya kwanza ya Wizara ya Maji ni usanifu mbovu wa miradi ya maji. Mtaalamu yeote anayefanya usanifu mzuri haiwezekani maji yashindwe kutoka lakini Wizara ya Maji ilikuwa kila mahali miradi ya maji inatengenezwa lakini haitoi maji kwa sababu usanifu mbovu, usanifu ambao umejengwa kwa maslahi ya watu wachache wapate fedha. Ilikuwa ni aibu mradi unajengwa, mahali pa kuwekwa bomba la *plastic* watu wanaweka bomba la chuma kwa sababu walikuwa wanatafuta kutafuta fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitawapa mfano, kuna mradi kule Namtumbo, mradi ule ultakiwa kuwekwa bomba la chuma lenye kipenyo cha milimita 250 lenye *pressure* 25, gharama ya bomba hilo ni shilingi bilioni 1.56. Nimeenda pale kwenye mradi ule nikauliza kwa nini hapa mnaweka bomba la chuma wakati maji haya yanatoka kwenye *tank* yanakwenda kwa wananchi? Kwa sababu *pressure* imepungua, kulikuwa hakuna majibu ya msingi. Matokeo yake nikawaambia fanyeni mahesabu leo usiku mlete jibu bomba gani la *plastic either HGPE* au mengine tutaweza kuweka hapa.

Mheshimiwa Spika, imefanywa hesabu usiku nimeletewa jibu Mheshimiwa tunaweza kuweka bomba la *plastic* na gharama yake ni shilingi milioni 560. Kutoka shilingi bilioni 1.5 mpaka shilingi milioni 560. Hata kama tungeweka *trillions* Wizara ya Maji tusingetatua tatizo la maji. Mainjinia na wahandisi wapo kila mtu anapitisha. Siyo nia yangu kumlaumu mtu yeote lakini tujifunze kwa makosa yaliyotokea. Tukiendelea kusimamia na tukifanya vitu sahihi naamini tutaleta mabadiliko makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatukuishia hapo tu, kulikuwa na ujanja mwingu unaendelea hata kwenye kulipa *certificate* na ndio sababu kwa kiasi kikubwa zikija *certificate* tunaziangalia kwa makini sana. Nitawapa mfano, kuna mradi kule kwa Mheshimiwa Keissy Namanyere, mkandarasi alileta *certificate* ya shilingi milioni 456. Baada ya kupeleka wataalam kufanya *actual measurement* yaani kupima kila

mahali, zege kiasi gani, *certificate* ile ilikuwa ni ya shilingi milioni 253 na tumeshailipa.

Mheshimiwa Spika, nitawapa mfano mzuri wa Arusha. Mradi wa Arusha una majengo mbalimbali ikiwepo na Ofisi za Kanda. Tumepeleka pale wataalam kuititia *certificate* zilizoletwa tukakuta tumeopoteza karibuni shilingi milioni 440. Mkandarasi anawaletea kwamba hapa ameweka zege tani kumi kumbe ameweka zege tani tatu. Sasa Wizara ya Maji inatakiwa iangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, tumeamua kwamba sasa *certificate* tunazipitia moja baada ya nyingine kuangalia *value for money*. Tumeigwa vya kutosha na tumedanganywa vya kutosha hatuwezi kuendelea namna hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kulijua hili tulifanya maamuzi magumu ya kuanzisha *Force Account*. *Force Account* kwa kweli Wizara ya Maji ilikuwa haipendwi na hata leo kuna watu Wizara ya Maji hawapendi *Force Account*, wanassema tunamsubiri tu Mpemba aondoke biashara inakuja palepale lakini tunawaambia Mwenyezi Mungu yuko pamoja nasi na tutafika mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumeanzisha utaratibu wa *Force Account* ambao tumeona faida kubwa sana. Kuna miradi mingi tumetekeleza ambayo faida yake imanza kuonekana. Miradi ya *Force Account* inachukua muda wa miezi mitano mpaka sita tu wakati ukimpa mkandarasi anachukua miaka miwili. Mradi unaojenga kwa *Force Account* kwa shilingi bilioni moja mkandarasi anakupa shilingi bilioni 2.3. Ubaya zaidi vifaa anavyoleta yeye viko chini ya viwango kwa sababu akishatandika bomba huwezi kuona ametandika nini chini ya ardhi. Mabomba tunayonunuua sisi tunanunuua viwandani moja kwa moja matokeo yake tunapata *value for money*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitatoa mifano tu, tunao mradi wa Manyara kule Mbulu Mjini, mkandarasi mradi huo alitaka

shilingi bilioni 1 sasa mradi huo umejengwa kwa kutumia *Force Account* kwa shilingi milioni 480. Mradi umekamilika na wananchi wanapata maji asilimia mia moja. Kuna mradi tena Manyara, mradi wa maji wa Alhash kule Mbulu, mkandarasi aliomba kwa kazi hiyo shilingi bilioni 2.7 kwa kutumia *Force Account* tunajenga kwa shilingi bilioni 1.35. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunao mradi kule Mbeya Mbalizi, Mheshimiwa Rais wakati tumetoka Malawi alinisimamisha kuhusu mradi huu. Mradi ule wakandarasi walikuwa wanataka karibuni shilingi bilioni 5.2 sisi tunaujenga kwa shilingi bilioni 3.5 na umefikia asilimia 85. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Njombe Makete kuna mradi wa Matamba - Kinyika. Mkandarasi aliomba shilingi bilioni 4.269 sisi tunajenga mradi huo kwa shilingi bilioni 2.4 na wananchi wameshaanza kupata maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna mradi huko Rukwa wa maji Kirando, Mheshimiwa Keissy ameuzungumzia sana. Wakandarasi wali-quote mradi huo kwa shilingi bilioni 4.6 sisi tunaujenga mradi huo kwa shilingi bilioni 2.9 na umefikia asilimia 85 na umechukua miezi kidogo tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna mradi wa *Muze Group*, mkandarasi mradi huu ali-quote kwa shilingi bilioni 2.68 sisi tunajenga kwa shilingi bilioni 3.19. Vijiji vya Kalumambezi A na B tayari vinapata maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukitaka tutatue matatizo ya maji lazima twende na utaratibu wa *Force Account*, hakuna njia nyingine. Hatuwezi kusema miradi yote tutafanya sisi kwa *Force Account* lakini tunaamini kwa asilimia kubwa tunaweza kuifanya, ile ambayo hatuna uwezo nayo *definitely* tutawapa wakandarasi. Hatuwezi kuwanyima kila kitu lakini bado miradi mingi tujenge kwa *Force Account*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulianza na miradi 23 ambayo gharama yake ilikuwa ni shilingi bilioni 43.61 kama tungetumia wakandarasi lakini kwa kutumia wataalam wetu wa ndani

miradi hiyo tumejenga kwa shilingi bilioni 27.51, Serikali imeweza kuokoa takribani shilingi bilioni 16. Wizara mpaka sasa hivi tunavyozungumza inajenga miradi 192 Tanzania nzima kwa kutumia *Force Account*. Gharama yake ni takribani ni shilingi bilioni 163.77 lakini kama tungempa wakandarasi gharama ingetoka kuanzia shilingi bilioni 250 mpaka shilingi bilioni 300 na ukamilishaji wake ungechukua miaka miwili au mitatu. Vilevile ingekuwa pengine miradi yao yenyeWE haijajengwa kwenye viwango vinavyostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, majibu ya changamoto za maji ni utaratibu wa *Force Account*, hakuna suala lingine. *Force Account* kwanza zina changamoto kubwa vilevile lazima tukubali.

Changamoto ya kwanza kabisa wahandisi wenyeWE hawataki kwa sababu na wao walikuwa ni sehemu ya wakandarasi, *is a part and parcel* ya wakandarasi. Sasa ukileta *Force Account* wahandisi wanaanza kupigapiga chenga. Kwa upande mwingine, kuna wahandisi wadogo wadogo ambao wamebadilika sana na wanafanya kazi kubwa. Hiyo ni changamoto ya kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, changamoto ya pili ni kwa Maafisa wa Manunuzi, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge wa Muheza kwamba kuna ucheleweshaji mkubwa. Wanachelewesha kwa sababu hiyo hiyo walikuwa wanafaidika sana kwenye kandarasi lakini tumechukua hatua. Yule Afisa Manunuzi wa Tanga tumempeleka Morogoro na wengine tumewahamisha kuhakikisha kwamba hakuna mtu yejote ambaye ataweza kutuzuia tusifanye utaratibu huu wa miradi. Kwa sababu nia yetu ni kuwasaidia Watanzania ili waweze kupata huduma ya maji safi na salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumeanzisha *RUWASA* kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri na kila mtu aliyechangia ameonesha kwamba *RUWASA* inafanya kazi nzuri. Kweli *RUWASA* tumeanza kupeleka fedha kwa mfano

tumepeleka kwanza takribani shilingi bilioni 29.66 kutoka *DFID* kwa ajili ya miradi ya *PbRna* matokeo yameanza kuonekana maeneo mengi ya nchini kwetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuna changamoto vilevile *RUWASA* kwa sababu kwanza taasisi yenyewe ni mpya, ina miezi kama sita hivi. Pia Maafisa wa Manunuzi bado hatujawapata wa kutosha. Sasa tumeleta utaratibu mzuri na *World Bank* imetupa kibali cha kuajiri Maafisa Manunuzi mbalimbali ambao watasaidia kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto hizi za *RUWASA*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, *RUWASA* vilevile, tumepeleka takribani shilingi bilioni 300 kwa ajili ya miradi ya *PfR* ambayo sasa imeanza. Tunaamini baada ya kumaliza tatizo la Afisa Manunuzi itaweza kufanya kazi vizuri sana. Kwa vile *RUWASA* tunaendelea kuishughulikia na tunaamini huko tunapokwenda kwenye suala la maji vijiji *RUWASA* ndio itakuwa mwarobaini mkubwa. Nashukuru sana viongozi wa *RUWASA* wanafanya kazi, wanajitoa sana ili kutatua matatizo ya maji kwa ajili ya Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, leo watu wengi wanazungumza lakini naamini miaka miwili, mitatu inayokuja tutazungumza hadithi tofauti kwenye Wizara ya Maji. Mimi leo naondoka Wizara ya Maji lakini nikiwa nimefurahi na nimeridhika sana kwa sababu nimekaa katika Bunge hili miaka kumi kila siku Wizara ya Maji ilikuwa ni maneno makali, kila siku ilikuwa bajeti ya Maji ni maneno makali lakini tokea jana nimefarijika sana tumewasikia Wabunge wengi wanaizungumzia vizuri sana Wizara ya Maji. Waheshimiwa Wabunge, Watanzania wenzangu, naomba niwahakikishieni kwamba hatutawaangusha, tutaongeza kupambana kuhakikisha kwamba Wizara ya Maji inaendelea vizuri sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia Mradi wa India. Mradi wa India Miji 28 ni muhimu sana na tumeuanza mwaka jana. Tulipata changamoto nydingi hasa taratibu za manunuzi kwa Mtaalam Mshauri lakini mwisho wake tulimpata na sasa hivi

ameshamaliza kazi zile za kufanya usanifu pamoja na kuandika *tender document*. Sasa kazi inayofuata ni kuwapata wakandarasi na tangazo la zabuni kwa ajili ya kuwapata wakandarasi lilitolewa *Exim Bank* tarehe 24 mwaka huu na siku ya mwisho wa kupeleka zabuni hiyo ilikuwa tarehe 21 Aprili, 2020.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Exim wanategemea kufungua zabuni hiyo tarehe 12 Mei, 2020. Tunategemea watakamilisha mchakato huo tarehe 19 Mei, 2020. Tunategemea itakapofika mwisho wa mwezi Julai tayari wakandarasi watakuwepo kwenye *site*. Pia tunategemea mradi ule utakapokamilika wataweza kuwashudumia wananchi wapatao milioni sita mpaka milioni saba mwaka 2040. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo mengine kwamba baadhi ya miradi inachelewa. Ni kweli inachelewa lakini miradi mingi inayachelewa ni ile ambayo tulikuwa tumewapa wakandarasi. Kuna wakandarasi hawa ambao wamefanya kazi lakini wengine kwa muda mrefu sana hawako kwenye *site*. Hata leo ukimlipa mkandarasi anachukuwa fedha anapeleka sehemu nyiningine. Baada ya kumlipa fedha kwa ajili ya kufanya kazi ye ye anaichukua fedha ile anaipeleka sehemu nyiningine. Sasa tumeamua kwamba mkandarasi tukimpa fedha kama hatakwenda tunampa muda halafu tunamfukuza.

Mheshimiwa Spika, tumewafukuza wakandarasi wengi na tutaendelea kuwafukuza wakandarasi hao. Kazi hizo mara baada ya kuwafukuza wakandarasi tunawapa watu wetu wa *RUWASA* na wanaendelea kufanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge sana kwamba miradi ya maji sasa imepata mwarobaini na tutahakikisha kila mwananchi anapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, mimi kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri tuna ugonjwa huu sasa ambao unatusumbua sana na maji ndiyo muhimu. Kama nilivyosema jana kwamba nazitaka Mamlaka zote za Maji zihakikishe maji yanapatikana saa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki. Wasitafute visingizio vya kuwakatia wananchi maji. Kila Mtanzania sasa hivi anahitaji huduma ya maji kwa sababu maji na sabuni ndiyo dawa ya *Corona* ambayo tunayo kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya mwisho kabisa, naomba tena nikushukuru wewe, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mweshimiwa Rais kwa kunipa heshima hii. Naomba tu Watanzania wenzangu tuendelee kujikinga na gongwa hili la *Corona* na Mwenyezi Mungu atatunusuru na atatupa maisha marefu, ahsanteni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa na mimi naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maji Prof. Makame Mbarawa kwa ufanuzi huo mzuri kabisa na kwa umahiri mkubwa sana, ahsante sana.

### **HOJA ZA KISERA**

**SPIKA:** Sasa tunaingia kwenye awamu ile ya mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Sina hakika nani yuko Msekwa au yuko hapa basi nikikutaja utasema kama upo upande gani, tuanze na Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuokoa muda, kwanza napenda kuishukuru na kuipongeza Serikali katika Mradi wa Miji 28 ambapo mwanzoni ilikuwa Miji 17 lakini Serikali ikafanya utaratibu na ku-review na kuona inufaike Miji 28, ni jambo la kupongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo ambayo ametoa Mheshimiwa Waziri, kwa sababu tumeshalieleza sana hata kwa wananchi wetu, ningeomba atuongezee kwa kuwaeleza kwa msisitizo ili waweze kupata *confidence* kwamba lini anadhani wakandarasi watakuwa *site* kwa sababu kidogo ni jambo la muda mrefu.

**SPIKA:** Ufafanunzi Mheshimiwa Waziri, utakapoona inafaa unaweza kumuachia Mheshimiwa Naibu pia, karibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba mchakato unaendelea na tunategemea mwisho wa mwezi wa saba mwaka huu Makandarasi watakuwepo *site*. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Pauline Phillipo Gekul ufanuzi.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru, langu ni moja, Mheshimiwa Waziri kwa unyenyekevu mkubwa, naomba nizungumzie kuhusus bili za maji kuwa juu. Mheshimiwa Naibu Waziri umesema kwamba kuna bili zinabambikizwa, lakini maeneo mengi bili hazibambikizwi, bili zimepanda zilikuwa miaka mitatu mfululizo hazikupanda, lakini mwaka jana bili zikapanda zikaruka zile *rates* za miaka inayofuata mpaka zikaenda kwenye viwango ambavyo wananchi wanashindwa kulipa.

Mheshimiwa Spika, lakini hizi bili Mheshimiwa Waziri ukiangalia kwa nchi nzima hazifanani, najua kuna masuala ya maeneo mengine wanasukuma kwa umeme maji, mengine mtiririko. Lakini nikupe mfano Kiabakari wanalipa kwa *unit* moja shilingi 350, Mbeya walikuwa wanalipa chini ya shilingi 1000, sasa hivi wanalipa 1200, Moshi wanalipa shilingi 1000, lakini Chalinze wanalipa 3048, Bukoba shilingi 2206, Bariadi shilingi 690, Mheshimiwa Waziri sisi tunalipa 1800, kutoka shilingi 1200, wananchi wa Babati wameshindwa kulipa bili za maji, na kipindi hiki cha corona pia.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa mtupatие ufanuzi baada ya kusema kwamba *EWURA*, wata-review, mme-review kwa kiasi gani mshushe hizi bili za maji? ahsante.

**SPIKA:** Ufanuzi wa jambo hilo muhimu sana ni kweli mambo ya bili za maji kwa Waheshimiwa Wabunge ni mtihani mkubwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, lakini ukimuona mtu mzima analia ujue kuna jambo. Lakini la pili nalotaka kusema mtitiriko huu wa bili inategemeana na namna gani mamlaka inavyotoa huduma *either kwa pumping* au kwa mseleleko. Kwa mfano Moshi pale wanapata kwa *gravity*. Kwa hiyo, gharama inakuwa ni nafuu ukilinganiasha na maeneo ambapo tunafanya *pumping* kwasababu ya ulipaji wa umeme. Lakini Mheshimiwa Mbunge na mimi tuko hapa Dodoma ninafikiri kesho ungekuja Wizarani tukae na watu hawa pamoja ili tuangalie jambo la Babati tuweze kulitatua, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya nyongeza Mheshimiwa Profesa Mbarawa.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa kipindi hichi kwa vile maji ndio dawa muhimu na sabuni, tumeamua mamlaka zote za maji haziwezi kupandisha bili yoyote ya maji, hilo la kwanza, la pili tutakaa *tu-review* tupitie upya hasa katika kipindi hichi kuangalia uendeshaji wa mamlaka zenyewe kuhakikisha kwamba watananzania wote wanapata huduma ya maji safi na salama hasa katika kipindi hichi cha corona.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Maji tunashukuru ahadi hiyo tunaichukua na tunaitunza mpaka wakati wa bajeti ni eneo ambalo ni muhimu sana kuliangalia kwa *gesture* nyingi ambazo zimekwishakuelezwani kweli watu wengi tunalipia wapiga kura bili za maji maana yake zimeshakuwa juu sana, Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka.

Hayuko Msekwa wala hapa, hayupo si vizuri kujandikisha wakati wewe hutakuwepo ni usumbufu, inatulia muda inawanyima nafasi wale ambao tayari wameshajipanga, Mheshimiwa Richard Philip Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi, *concern* yangu ni kuhusiana na miradi ambayo bado haijakamilika na kwenye hotuba yake Mheshimiwa Waziri ameweza kujieleza pamoja na kuweka asilimia ambazo tayari miradi hiyo imekwishafanyika.

Mheshimiwa Spika, sasa kutokana na umuhimu sana wa kutimiza sera ya maji ya mwaka 2002 pamoja kufikia malengo ya wastani wa asilimia 85 Vijijini wapate maji, ningombwa Serikali iangalie namna gani ambavyo wanaweza wakatenga fedha kwa miradi hii ya mwaka huu wa fedha 2019/2020 kufikia mwezi Juni unapoisha mwaka wa fedha ili iende ikakamilike na isiathiri bajeti inayofuata ya 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, tumeona miaka mingi kutokana na kuanzishwa kwa RUWASA taratibu za manunuzi zilichelewa na kuamisha miradi toka halmashauri kuja RUWASA pia iliweza kuchelewa na halmashauri nyingi bado hazijaleta fedha za madeni. Kwa hiyo, *concern* yangu ni Serikali kufanya bajeti ya *allocation* ili miradi hiyo ikamilike kwa fedha ambazo ziliikuwa za mwaka huu wa 2019/2020.

**SPIKA:** Ufanuzi wa jambo hilo hili Mheshimiwa Waziri mwenyewe.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba miradi yote tulioianza tutajitahidi kama inavyowezekana tuimalize mwaka huu, na tutajitahidi kwamba fedha tunaweka ili tuweze kumaliza miradi hiyo kwasababu nia ya serikali ni kuhakikisha kwamba miradi inaazwa na inamalizika kwa wakati.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Kivuli.

**MHE. ZUBEDA H. SAKURU:** Mheshimiwa Spika, nashukuiru sana nahisi ambacho tunashindwa kuelewana na Serikali ni kitu kimoja tunafahamu kwamba hizi *measures* ambazo wanataka kuzichukua ili kukabiliana na corona kwa mfano kuchimba visima ili kuhakikisha wananchi wanapata maji muda wote, ku-control mamlaka kuacha kubambikia wananchi ankara za maji bili za maji pamoja na kutokata maji *these are support to be permanent measures* katika Wizara ya Maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho tukisisitiza toka jana, tunajua kwamba wananchi wengi wamekuwa *retrenched*, vilevile wananchi wengi wameshindwa kutoka majumbani kuijendeleza na shughuli za kiuchumi, biashara zimeendelea kudorora, uchumi umekuwa hautabiriki na sasa tunaona kwamba matumizi ya maji majumbani, viwandani yamekuwa makubwa kama *one of the measures* ya ku-combat covid 19. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa sisi ambacho tumekuwa tunaitaka ni Serikali kutoa *commitment* tumeona majirani zetu Kenya wao wametoa *grace period* ya miezi mitatu ya kufuta kabisa bili za maji, Chad wamefanya hivyo hivyo wamefanya *grace in period* ya miezi sita ya kufuta ankara za maji, Ghana wamefanya *the same thing*, lakini wao wametoa *grace period* ya miezi mitatu; na vilevile DRC Congo wametoa *grace period* ya miezi miwili ya kufuta ankara za maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa sisi ambacho tunakitaka na tunataka Waziri atolee ufanuzi ni kwanini Wizara ya Maji inasita kutoa hauweni kufuta bili za maji kipindi ambacho matumizi ya maji yameendelea kuongezeka kayika kukabiliana *covid 19* nchini. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ufanuzi wa jambo hilo Mheshimiwa Waziri wa Maji Profesa Mbarawa.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, hatuwezi kwanza kufanya hivyo kwasababu kila nchi inautaratibu wake. Halafu Mamlaka za Maji lazima zijiendeshe, lazima kuwe na fedha

ambayo tutalipia ya umeme, tutalipia madawa na kila kitu. Ni muhimu sisi kuhakikisha kwamba maji yanapatikana hilo ndiyo ndiyo jambo muhimu sana katika kipindi hichi. (*Makof*)

**SPIKA:** Waziri Kivuli.

**MHE. ZUBEDA H. SAKURU:** Mheshimiwa Spika, sijaridhika na maelezo aliyoyatoa Mheshimwia Waziri jana tumesema na nimenukuu katika hutuba yangu maneno ambayo aliwahi kusema Linkon kwamba *A Government is of the people by the people for the people.* (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa tunaposema leo kwamba wananchi wanachindwa kupewa *grace period* na Serikali na tutambue kwamba tunalipa kodi na siyo kwamba hili janga limekuja kwa kujitakia *this is one of the most challenging time* ambayo tumejua kwamba kila *authority* Tanzania inachangamoto hiyo *COVID19*na measures ambazo serikali mnazisema ni zile zile za kuendelea kunawa kwa maji yanayotiririka. Sasa sijui ni kwanini Waziri anasema huu siyo wajibu wa Serikali na tunafahamu kwamba mamlaka zinatakiwa zijiendeshe *well and good*, lakini *what is the commitment* ya Wizara katika kuhakikisha wananchi wanapata kile wanachokistahili. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Mbarawa.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba tuelewe kwa siku wewe unanawa maji mara, tuseme mara kumi unatumia maji kiasi gani. Sasa haitokuwa kwamba sasa hivi wewe kutokana na hili tuanze kufuta, tuanze kusimamamisha wananchi wasilipe bili za maji, matokeo yake hata hayo maji yatakuwa hayapo. Kama tutasema tunatoa inamaana tutashindwa kulipa umeme, tutashindwa kulipa madawa na matokeo yake mwisho wa siku tutakuwa hatuna hata hayo maji ya kunawa. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana, naomba tuskilizane hilo ni jambo endelevu Mheshimiwa Waziri ninahakika hili utakutana nalo sana, japo tunambana sana Waziri wa Maji hapa, lakini huko

mbele utakutananalo sana akiwepo na Waziri wa Afya, si wazo bay a sana kufanya kitu fulani, *something*, hatuwezi kusema ni kitu gani, lakini ni *something* lakini la Waziri wa Fedha zaidi, Mheshimiwa mama Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba kwa heshima kabisa Mheshimiwa Waziri wa Maji utuhakikishie kama Urambo tumo katika ile Miji 28 kutokana na shida kubwa ya maji tuliyonayo, ahsante.

**SPIKA:** Nadhani hapa ungeweza kurudia tu Profesa kwa kuitaja ile Miji 28 ili kila mtu kama unaweza ukakumbuka hapo ili wanaohusika waweze kulifahamu vizuri, ya mradi wa ziwa Victoria. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, tutasambaza lakini naomba nimuhakikishie Mheshimiwa mama Sitta Urambo ipo Kaliua ipo Igala na mengine tutaleta tu baadaye kwenye *pigeon hole*. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa, Dkt. Hadji Hussen Mponda yupo..

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, nipo Msekwa.

**SPIKA:** Tafadhali ni wakati wako sasa.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kupata nafasi ya kupata ufanuzi. Hotuba ya Waziri ukurasa wa 26 umeelekeza suala la umbembazi, utafiti wa rasilimali ya maji na usambazaji. Lakini katika houtuba nzima na ukiangalia hata randama na viambatanisho ambavyo vimewekwa havionyesi uwiano kati ya hizo kazi za uchimbaji wa visima ambavyo ni vyanzo vya maji na usambazaji ili wananchi watumie hayo maji. Labla kwa mfano raisi ili nieleweke Wilaya ya Malinyi kwa bajeti ya 2018/2019 tumechimba visima 20 na visima hivyo vimebainika vina maji ya kutosha, lakini kwenye bajeti hii tulitegemea sasa

tungepata pesa ya usambazaji wa hayo maji. Je Waziri anamaelezo gani kwenye hili? nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ufanuzi tafadhalii.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kawaida tukichimba kisima tunaanza na utafiti, tunachimba kuangalia uwingi wa maji, tunachimba na baadae tunajenga miundombinu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshachimba visima hatua inayofuata sasa ni kujenga mfumo wa usambazaji ili wananchi waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

**SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge tumefikia mwishoni mwishoni sasa ili tuweze kukamilisha kazi yetu baada ya utaratibu mzima kukamilika sasa ni wakati wa kutenda ile kazi yetu ya Kibunge ya kuitendea haki na kuiamulia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maji ya kwamba mkubali sasa kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 Waheshimiwa Wabunge kura mmekwishapiga na mimi ninazo hapa ninaziona zote kila mtu amepigaje kwa jina na kwa hakika walio sema ndiyo wameshinda.

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Wizara ya Maji kwa mwaka 2020/2021 yalipitishwa na Bunge kama ifuatavyo:-**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

Fungu 49 - Wizara ya Maji.....Sh. 28, 275,145,000

### **MPANGO WA MAENDELEO**

Fungu 49 - Wizara ya Maji.....Sh.705,008,930,000

**SPIKA:** Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji Mheshimiwa Prof. Mbarawa Naibu

wa Maji Mheshimiwa Aweso, Katibu Mkuu na timu yote ya Wizara hii ya Maji pamoja na yote yaliyosema kwa siku mbili hizi msivunjike moyo ni changamoto tu tunatambua jinsi ambavyo mkiangaika kuzunguka nchi nzima kupigana na jambo hili kla kuwapatia maji watanzania. (*Makofii*)

Nakushukuru sana Mheshimiwa Profesa katika kuhitimisha wewe mwenyewe umeeleza wazi kwamba kwa kutumia maneno yako ya *entire system* ya Wizara ya Maji ilikuwa na shida kubwa sana kuianzia kwenye halmashauri kwenye mikoa na mpaka wizarani. Ilikuwa ni *chainya* upigaji hilo ni kweli kabisa sisi tunakubaliana nawe, Wahandisi walikuwa ni sehemu ya Makandarasi na baadhi ya makampuni yalikuwa ni ya Wahandisi wenyewe. (*Makofii*)

Kwa mfano wakati wa miradi ya *World Bank* ile tullyoanza nayo mwanzo ile ilipoanza miradi ile hapakuwa na Makandarasi wa maji. Kwa hiyo ilikuwa ni timu zile zile za Makatibu Wakuu walistaafu, Wakurugenzi waliostaafu, au Watumishi wa Wizara ya Maji waliokuwa basi wale ndiyo wakaunda makapuni ya kwanza na ikawa ni mfumo mzima sasa wa wenyewe kwa wenyewe; upigaji mkubwa sana umefanyika hata Mheshimiwa Naibu Waziri Aweso ameeleza jinsi miradi ya Benki ya Dunia ile ya mwanzo ilivyokuwa kichefuchefu mabilioni ya shilingi yalienda hakuna kilichofanyika kwa sababu ya hiyo *chainna chain* hiyo ikawa imetengenezwa tangu mwanzo na imeendelea, wakandarasi ni wao wasanifu ni wao, nawaihdinishaji huku ni hao hao wa maji hao hao walioajiriana wao kwa wao na hivo. (*Makofii*)

Kwa hiyo, mfumo ule ulikuwa na shida sana kwa kweli ultakiwa uvunjwe ule na nafikirui mmejitahidi sana kuribu kuvunja mfumo huo wa ujanja ujanja na wizi. Nakubaliana nawe kama ulivyosema kwamba tumepigwa vyta kutosha tumedanganywa vyta kutosha. (*Makofii*)

Kwa hiyo, pia tunawaunga kwenye kuelekea kwenye *force account* hebu tujaribu na utaratibu huu tuone utatusogeza kiasi gani. Na kwa kweli ndiyo maana Wabunge

wamekuwa wakisema na sisi kupigia mstari kwamba jamani kwenye Wizara hii mabilioni ya shilingi yamepelekwa, lakini ukitazama matokeo yake ndiyo hivo tena na ninyi wenyewewe mmeeleza na tunatambua na tunajua kazi nzito iliyoko hapo.

Ni ukweli ukipewa kazi ya kuwa Waziri wa Maji katika nchi yetu umepewa mapambano makubwa si jambo rahisi, na ziko Wizara zingine za namna hiyo lakini Wizara ya Maji ni shughuli pepu Wizara nydingine ukipewa nayo ni balaa kwa maoni yangu ni Wizara ya Fedha, ukipewa kuwa Waziri wa Fedha ukakaa miaka mitano kama rafiki yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango basi mniamshukuru Mungu lakini hutoki salama hapo utatoka na mapresha, magonjwa ya moyo nakadhalika, kawaida Mawaziri wa Fedha miaka miwili unaondoka kidogo unaweza uka-*survive* kidogo baadhi ya haya maradhi. (*Makofii*)

Kwa hiyo, tunakupongeza kukaa miaka mitano na wewe pia usichukulie *personally* hizi Wizara ni ngumu kwasababu ni mahali pa kugawa rasilimali, sasa ukiwa unagawa rasilimali bwana lazima tu wengine watasema hapa vipi hapa namna gani hata ugawe namna gani lakini basi ujitalidi hivo hivo tutafika safari yetu. Kwa hiyo, tunawapongezeni sana ninyi wa Wizara hizi ambazo wakati huu wa kugawa rasilimali mnapata changamoto msife moyo ni sehemu ya kujua wapi pana *pinch* wapi pa kurekebisha, pakufanya nini lakini mwisho wa siku tuko pamoja kabisa tunatambua kazi zenu, tunatambua mizigo mizito ambayo kuitia upendo wa Mheshimiwa Rais amewateua lakini tunajua mizigo mizito ambayo mnaibeba mkiwa kama Wabunge wenzetu na hali halisi kule *sit* ilivyo.

Ni kweli kabisa mimi Mbunge wa miaka 20 naenda kwenye Kijiji ambacho nimeenda kwa miaka 20 nikiwaambia jamani tulieni mtapata maji na hawajawai kupata maji naenda kichofuata hawajawahai kupata maji, kinachofuata najiuliza hivi kesho naenda kudanganya nini, yaani nitatumia lugha gani kwasababu tukishatoka hapa sisi ndiyo tuobeба Wizara zote, ukishafika kule huna kisingizio, wewe kama Mbunge lazima utafute namna gani ya kutoka pale na

kuwapa moyo wananchi ili waendelee kuiamnini Serikali yao ni kazi kubwa sana. (*Makofi*)

Kwa hiyo, wakati mwingine mtuelewe unapoona mtu amekasirika ni jambo la kuelewa mambo magumu ambayo tunakumbana nayo kama Wabunge kwenye maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, keki ndogo tunayoipata tukigawana gawana hivi kidogo tunaweza tukawambia jamani si mnaona wenzenu wamepata na ninyi inakuja watu wanaridhika kidogo. Kwa hiyo, tunawashukuruni sana sana na poleni kwa yote na tunawatakia kila la kheri.

Sasa mwisho hapa natumaini Waheshimiwa Wabunge tayari mnafahamu nyote kwamba msiba umetokea wa Jaji Mkuu Mstaafu Jaji Augustino Ramadhani usiku wa kuamkia leo, nichukue nafasi hii kumtumia salamu za rambirambi Jaji Mkuu na Muhimili wa Mahakama kwa ujumla kwa pigo hili kubwa ambalo wamelipata la kuondokewa na mtumishi mwaminifu, mtumishi wa muda mrefu mwanasheria mahili, Jaji Mstaafu Augustino Ramadhani tunamuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

Basi Waheshimiwa Wabunge bahati nzuri siku ya leo tumemaliza kazi zetu mapema kidogo ni jambo jema kwa wale waliofunga tunawatakia futari njema, siku za nyuma tumekuwa tukialikana katika futari mbalimbali sasa leo nilikuwa nimemuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu safari hii mbona umenyamaza sana Mheshimiwa hatuoni kadi ya mwaliko futari vipi, akaniambia Mheshimiwa si unajua corona, nikamuambia lakini Mheshimiwa futari ya kwenye bahasha inaruhusiwa na Spika ile haivunji kanuni. (*Makofi*)

Kwa hiyo na Waheshimiwa wengine mlizozoea kutualika alika jamani tulishazoea sasa mtuekee tu kwenye bahati futari zile ili utaratibu wetu mazoea yetu yaendelee maana yake *miss* kweli kweli futari safari hii, niwaambie wenzangu tulizozoea futari za kualikwa safari hii tutulie majumbani nikiwa pamoja na mimi mwenyewe. Kwa hiyo, tuisiwalaumu wenzetu wala tusizitafute tujaribu tu kutumia kwa

sababu ya hali halisi na mazingira yalivyo na msisitizo ambao tunaambiwa na Serikali yetu kwamba tusiwe katika makundi makundi tufuate taratibu tunazoambiwa kuhusu hali halisi ilioyopo. (*Kicheko*)

Kama nilivyoeleza kabla, kesho tuna Wizara ya Afya, na kwa kuwa mambo ya leo yamekamilika yote basi naomba nichukue fursa hii kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho Saa Nane Kamili Mchana.

*(Saa 11.43 Jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatano,  
Tarehe 29 Aprili, 2020 Saa Nane Mchana)*